# USAWIRI WA JINSIA KATIKA LUGHA YA MASHAIRI: MIFANO KUTOKA MASHAIRI YA SHAABAN ROBERT

**BADREDDEN MOHAMED SALEM**

**IMEWASILISHWA KAMA SHARTI PEKEE LA KUHITIMU SHAHADA YA UZAMILI (M.A) YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2013**

## ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo: **“Usawiri wa Jinsia Katika Lugha ya Mashairi: Mifano kutoka Mashairi ya Shaaban Robert”,** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

__________________________

**Prof. Emmanuel Mbogo**

(**Msimamizi**)

**Tarehe**: __________________

## HAKI MILIKI

Haki ya kunakili tasinifu hii inalindwa na Mkataba wa Berne, Sheria ya Haki ya Kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali za kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya Tasnifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea, au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# IKIRARI

Mimi Badredden Mohamed Salem, nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu ya halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Digrii yoyote.

**Saini ________________________**

**Tarehe ________________________**

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu walionizaa, wakanilea, wakanitunza, wakanisomesha na kunijulisha baya na zuri. Wao ndio walimu wangu wakuu, walionipa elimu kabla hawajaniweka katika ulimwengu.

## SHUKURANI


Kwanza kabisa kabla sijasema neno lolote, napenda nitoe shukrani zangu zisizo na ukomo kwa Allah Subhanahu Wataalah kwa sababu yeyé ndiye mkuu na anayepaswa kushukuriwa kwa hatua yoyote ya maisha ya mwanadamu. Ninamshukuru kwa kunijaalia afya njema kipindi chote cha masomo yangu, kunipa nguvu, uwezo, akili, busara na maarifa. Nasema kwa unyenyekevu, Alhamdulillah Rabbilaalamina.

Pili, ninawashukuru sana wazazi wangu kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, na kunifunza kuhusu malimwengu na ulimwengu. Nakiri kuwa mapenzi yao hayana kifani.

Tatu, napenda kumshukuru kwa dhati na kwa upekee Msimamizi wangu Prof. Emmanuel Mbogo kwa kunilea kitaaluma na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili. Sina neno linalofaa kutoa shukrani zangu kwake bali namuombea afya njema na maisha marefu ili aendelee kutoa msaada wa kitaaluma kwa wanafunzi wanaohitaji maarifa zaidi.

Nne, napenda kuwashukuru wahojiwa wangu wote walioshiriki katika utafiti huu kwa ukarimu na ushirikiano walionipa kipindi chote nilichokuwa uwandani. Nitakuwa mchahe wa fadhira nisipotoa shukrani zangu kwa watanzania wote walionifunza Kiswahili nikaweza kuishi bila shida Tanzania. Namshukuru Bi. Hadija Jilala kwa kunifunza lugha ya Kiswahili na kunipa ushauri juu ya fasihi na nadharia za fasihi. Pia nawashukuru wanaidara wote wa idara ya lugha na fasihi kwa maoni na miongozo yao hadi leo nimefanikiwa.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu Usawiri wa Jinsia Katika Lugha ya Mashairi: mifano kutoka katika mashairi ya Shaaban Robert. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa jinsia katika lugha ya mashairi ya Shaaban Robert katika kazi zake za fasihi za *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* ili kuonyesha jinsi lugha inavyotumika kujadili suala la ujinsia. Utafiti huu ulitumia mbinu nne za ukusanyaji data ambazo ni; maktaba, usaili, dodoso na majadiliano ya vikundi. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya; madhumuni maalum, kimfumo na uteuzi wa nasibu takabishi.

Utafiti huu umegundua kuwa, tamathali za semi zilizotumika katika mashairi ya Shaaban Robert ni: Sitiari, takriri, tashihisi, tasifida na tashibiha. Aidha utafiti huu uligundua kuwa tamathali za semi husawiri swala la ujinsia kwa kuonyesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume. Kwa kutumika tamathali za semi mwanamke husawiriwa kama kiumbe dhaifu, tegemezi na asiye na maamuzi binafsi ukilinganisha mwanaume ambaye huonekana kuwa ni jasiri, hodari, shupavu na mwenye maamuzi binafsi. Vile vile, utafiti huu uligundua kuwa, matumizi ya tamathali za semi husawiri nafasi ya mwanamke katika jamii. Kwa kutumika tamathali za semi nafasi ya mwanamke inajibainisha katika: mwanamke katika asasi ya ndoa, mwanamke katika kufanya maamuzi, mwanamke katika elimu, mwanamke katika uzazi na malezi, mwanamke katika mapenzi, mwanamke katika utamaduni, mwanamke katika dini na mwanamke kama kiumbe muhimu katika jamii.

# YALIYOMO

**ITHIBATI** .......... **ii**

**HAKI MILIKI** .......... **iii**

**IKIRARI** .......... **iv**

**TABARUKU** .......... **v**

**SHUKURANI** .......... **vi**

**IKISIRI** .......... **vii**

**ORODHA YA VIELELEZO** .......... **xii**

**SURA YA KWANZA** .......... **1**

**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA** .......... 1

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Tatizo .......... 1

1.3 Tatizo la Utafiti .......... 3

1.4 Malengo ya Utafiti .......... 3

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti .......... 3

1.4.2 Malengo Mahsusi .......... 4

1.5 Maswali ya Utafiti .......... 4

1.6 Umuhimu wa Utafiti .......... 4

1.7 Mipaka ya Utafiti .......... 5

1.8 Matatizo ya Utafiti .......... 5

**SURA YA PILI** .......... **6**

**2.0 MAPITIO YA MAANDIKO TANGULIZI** .......... **6**

2.1 Utangulizi .......... 6

2.2 Vipengele vya Lugha .......... 6

2.1.1 Tamathali za Semi ........ 6
2.2 Mapitio ya Maandiko Kuhusu Ujinsia kwa Jumla ........ 11
2.3 Mapitio ya Machapisho Kuhusu Ujinsia katika Ushairi ........ 18
2.4 Tafiti Kuhusu Kazi za Shaaban Robert ........ 26
2.5 Mwega wa Kinadharia ........ 26
**SURA YA TATU ........ 29**
**3.0 MUUNDO NA MBINU ZA UTAFITI ........ 29**
3.1 Utangulizi ........ 29
3.2 Mkabala wa Utafiti ........ 29
3.3 Eneo la Utafiti ........ 31
3.4 Kundi Lengwa ........ 32
3.5 Sampuli na Usampulishaji ........ 34
3.5.1 Sampuli ya Watafitiwa ........ 34
3.5.1.1 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu ........ 35
3.5.1.2 Usampulishaji wa Kimfumo ........ 37
3.5.1.3 Usampulishaji Nasibu Tabakishi ........ 38
3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data ........ 40
3.6.1 Usaili ........ 40
3.6.2 Dodoso ........ 42
3.6.3 Mbinu ya Maktabani ........ 43
3.6.4 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi ........ 44
3.7 Uchambuzi wa Data ........ 44
3.8 Zana za Kukusanyia Data ........ 46
3.8.1 Matini ........ 46

3.8.2 Kompyuta na Notibuku ........ 46

3.8.3 Kinasa Sauti ........ 46

3.8.4 Kamera ya Kawaida ........ 46

3.8.5 Dodoso/ Hojaji ........ 47

3.8.6 Usaili ........ 47

3.9 Hitimisho ........ 47

**SURA YA NNE ........ 49**

**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ........ 49**

4.1 Utangulizi ........ 49

4.2 Tamathali za Semi katika Mashairi ya Shaaan Robert ........ 49

4.1.1 Sitiari ........ 50

4.1.2 Tasifida ........ 53

4.1.3 Tashihisi ........ 55

4.1.4 Tashibiha ........ 55

4.1.5 Takriri ........ 56

4.3 Tamathali za Semi na Usawiri wa Ujinsia ........ 57

4.4 Tamathali na Semi Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke ........ 80

4.3.1 Mwanamke Katika Asasi ya Ndoa ........ 80

4.3.2 Mwanamke Katika Kufanya Maamuzi ........ 81

4.3.3 Mwanamke Katika Elimu ........ 83

4.3.4 Mwanamke Katika Uzazi na Malezi ........ 86

4.3.5 Mwanamke Katika Mapenzi ........ 88

4.3.6 Mwanamke Katika Utamaduni ........ 88

4.3.7 Mwanamke Katika Dini ........ 92

4.3.8 Mwanamke Kama Kiumbe Muhimu Katika Jamii ........................................ 95

4.5 Hitimisho.......................................................................................................... 98

**SURA YA TANO ........................................................................................ 100**

**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO............................ 100**

5.1 Utangulizi........................................................................................................ 100

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ............................................................... 100

5.3 Hitimisho........................................................................................................ 102

5.4 Mapendekezo ................................................................................................ 104

**MAREJELEO ................................................................................................ 105**

**VIAMBATISHO ............................................................................................ 113**

## ORODHA YA VIELELEZO

Jedwari 3. 1: Mgawanyo wa Watafitiwa kwa Kuzingatia Kitengo na Umri ........... 34

Jedwari 3.2: Mchanganuo wa Sampuli ya Utafiti ................................................... 39

Jedwari 4.1: Idadi ya Tamthali za Semi Kiulinganshi (Asilimia)........................... 50

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi ambayo inabainisha na kuelezea juu ya usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti ambayo utafiti huu ulikusudia kuyajibu na umuhimu wa utafiti. Aidha, sura hii inaelezea kuhusu mawanda ya utafiti na matatizo tuliyokumbana nayo katika utafiti.

## 1.2 Usuli wa Tatizo

Fasihi simulizi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo (Mulokozi na Sengo, 1995). Kwa kutumia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi tunaweza kubadili mielekeo, mitazamo, tamaduni, imani, mila na desturi za jamii husika katika muktadha na wakati mahsusi. Fasihi simulizi inaweza kutumiwa kuzuia au kuchelewesha maendeleo na mapinduzi. Fasihi simulizi inasaidia kujifunza utamaduni wa umma; kuelewa msimamo, itikadi na mahitaji yao, na kuwasaidia kuitumia fasihi yao kuendeleza mapambano dhidi ya mazingira yao. Hivyo ni wazi kuwa fasihi simulizi huweza kuibua masuala mbalimbali yanayoibuka katika jamii na kuleta athari kwa jamii kwa haraka zaidi (Mulokozi, 1982).

Fasihi simulizi ni utanzu wa fasihi ambao una tanzu nyingi. Moja wapo ya tanzu za fasihi simulizi ni ushairi. Shairi ni utungo unaotumia lugha ya mkato wenye mnato na mvuto katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii Mulokozi na Kahigi, (1979).

Ushairi una tanzu nyingi ambapo mashairi ya bongo fleva ni moja ya utanzu wa ushairi (rej. Omari (2009). Bongo fleva ni utanzu ambao umeibuka miaka ya 80 na umeshamiri na kupendwa sana na vijana wa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla. Kwa kutumia nyimbo hizi vijana wanaelezea hisia zao, matamanio yao, matarajio yao, kukata tamaa na uzoefu wao katika jamii yao Senkoro, (2003).

Utafiti huu ulihusu usawiri wa jinsia katika lugha ya mashairi kwa kutumia mifano kutoka mashairi ya Shaaban Robert. Lugha ina nguvu na uwezo wa kuonesha mahusiano ya kijamii, mifumo ya utawala, mgawanyo wa mali, mila na desturi na huonesha aina ya mahusiano baina ya wanawake na wanaume katika jamii yoyote. Uteuzi wa maneno wakati wa mazungumzo huonesha aina ya mahusiano pia baina ya wahusika wa mada ya mazungumzo. Mathalani, mazungumzo kati ya meneja wa kampuni na mfanyakazi wa kada ya chini yatapambanuliwa na aina ya maneno watakayotumia katika mazungumzo yao ukilinganisha na uteuzi wa maneno baina ya marafiki au watu wa kada moja mahali pa kazi (Taz. Msanjila na wenzake, 2009).

Hivyo, ni jambo linalotarajiwa kuwa usawiri wa kijinsia baina ya mwanamke na mwanaume utabainishwa na aina ya lugha anayotumia mshairi. Ili kufikia lengo la utafiti huu, mtafiti alichunguza na kubainisha tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert katika vitabu vya *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, kujadili jinsi tamathali hizo zinavyosawiri mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme, kufafanua nafasi ya mwanamke kama inavyosawiriwa na tamathali za usemi za mashairi ya *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*.

Utafiti huu unachunguza usawiri wa jinsia katika lugha ya mashairi kwa kutumia mifano kutoka mashairi ya Shaaban Robert. Kimsingi lugha ina vipengele mbalimbali ambavyo hutumiwa na wasanii wa kazi za sanaa katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Utafiti huu ulichunguza kipengele cha tamathali za semi tu. Hivyo basi, kwa kutumia utafiti huu tuliweza kuchunguza kipengele hiki na jinsi kinavyosawiri suala la ujinsia katika mashairi ya Shaaban Robert ambayo ni *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* na *Pambo la Lugha*.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Suala la jinsia ni suala ambalo limekuwa likijadiliwa na wataalamu mbalimbali (Sanger, 1937; Standt, 1976 na Senkoro, 1982) na pia kupigiwa kelele na wanajamii, wanaharakati wa masuala ya kijinsia. Hata hivyo bado inaonekana kuwa kuna haja ya kuchunguza kwa kina ni kwa jinsi gani wanafasihi wanalizungumzia suala hili hasa katika mashairi. Tatizo la utafiti huu lilikuwa ni jinsi gani tamathali za semi kama kipengele cha lugha kinatumika kusawiri suala la ujinsia. Je tamathali za semi zinazotumika katika mashairi zinaonyesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume? Hivyo basi, utafiti huu umechunguza jinsi kipengele cha tamathali za semi kinavyotumika katika kusawiri suala la ujinsia katika mashairi ya Shaaban Robert ya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* na *Pambo la Lugha.*

## 1.4 Malengo ya Utafiti

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa jinsia katika lugha ya mashairi ya Shaaban Robert katika kazi zake za fasihi za *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na*

*Baada ya Miaka Hamsini* ili kuonyesha jinsi gani lugha inavyotumika kujadili suala la ujinsia.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

Utafiti huu una malengo mahususi matatu.

i) Kubainisha tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert katika *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*.

ii) Kujadili jinsi tamathali hizo zinavyosawiri mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme.

iii) Kujadili nafasi ya mwanamke kama inavyosawiriwa na tamathali za usemi za mashairi ya *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini.*

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kujibu maswali yafuatayo;

i) Ni tamathali zipi za usemi zinazojitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert ya *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*?

ii) Tamathali hizo zinasawiri vipi mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme?

iii) Mwanamke anapewa nafasi gani katika tamathali za semi zilizotumika katika mashairi ya *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu nne; kwanza, utafiti huu utawasaida wanafunzi wa elimu mitindo, wanaisimu na wanafasihi kuelewa jinsi na

upekee wa mwandishi katika uteuzi wa vipengele vya lugha kiisimu katika ujenzi wa kazi za fasihi hususani katika mashairi. Pili; utafiti huu utawasaidia wanafunzi na watafiti wengine kupata marejeo na pia ni changamoto kwa watafiti kufanya tafiti zaidi katika kazi za fasihi simulizi. Tatu; utafiti huu ni malighafi, kwani utatoa mchango katika historia ya fasihi simulizi hasa katika ushairi na hatimaye utatajirisha maktaba ya chuo. Utafiti huu utatoa mchango wa maarifa katika taaluma ya elimu mitindo na suala la jinsia kwa ujumla. Hivyo basi, utatumika kama marejeo kwa watafiti wengine.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza tamathali za semi kama kipengele kimojawapo katika lugha. Ieleweke kuwa mashairi yaliyotungwa na kuandikwa na Shaaban Robert ni mengi hivyo mashairi yaliyochunguzwa ni mashairi ya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* na *Pambo la Lugha*.

## 1.8 Matatizo ya Utafiti

Mtafiti alikukumbana na matatizo kadhaa: kwanza ni suala la pesa, mazingara na ugeni wa mtafiti katika nchi ya Tanzania. Kwa kuwa mtafiti anatokea Libya, mazingira ya Tanzania yalikuwa magumu kwake na pia kuelewa mila na desturi za Watanzania na jinsi ya kuyakabili hayo yote katika utafiti ili kupata data zinazofaa.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA MAANDIKO TANGULIZI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandiko tangulizi kuhusu mada iliyofanyiwa utafiti. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza inahusu tamathali za usemi, sehemu ya pili ni ujinsia kwa ujumla, sehemu ya tatu ni mapitio kuhusu ujinsia katika ushairi, sehemu ya nne ni tafiti kuhusu kazi za shaaban Robert na sehemu ya tano ni mwega wa kinadharia.

## 2.2 Vipengele vya Lugha

Lugha ina vipengele mbalimbali ambavyo hutumiwa katika kazi za fasihi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Vipengele vya lugha ni pamoja na tamathali za usemi, vina na mizani, na lugha ya mkato, jazanda nakadhalika.

### 2.1.1 Tamathali za Semi

Tamathali za semi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza, au kuubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), tamathali ya (za) usemi hutumiwa kuelezea fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa tamathali za semi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa kutmia dhana nyingine toafuti au zinazofana nazo ambazo

hutumiwa kwa lengo la kupanua, kupuuza, kubadilisha maanma za dhahiri au za kawaida ili kuwasilisha ujumbe na maana iliyokusudiwa kwa hadhira wa jamii mahususi. Senkoro (2012) anaainisha tamathali za semi kuwa ni sitiari, tashibiha, metonomia, tashihisi, majazi, ishara, taashira na kejeli. Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa tamathali zinazotumika zaidi katika ushairi ni tashibiha, tashihisi, kejeli, metonimia na sitiari.

Utafiti huu ulichunguza na kuzibainisha tamathali za semi katika mashairi ya vitabu teule vya shaaban Robert kama zilivyoainishwa na senkoro (2012). Utafiti huu ulichunguza namna tamathali hizo za semi zinavyotumika kuibua suala la ujinsia katika amshairi ya Shaaban Robert. Sehemu ifuatayo inazijadili tamathali za semi ili kuonesha maana na namna zilivyo kimuundo na kidhima.

#### 2.1.1.1 Tashibiha

Tashibiha hujulikana pia kama tashibihi. Hii ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Kwa hakika, tashibiha ni usemi wa kimlinganisho utumiao maneno-viungio kama vile *mithili ya*, *kama kwamba*, *kama*, *kama vile*, *tamthili ya*, *sawa* nakadhalika. Kwa mfano, mweusi kama mkaa, mweupe mithili ya theluji na mrefu kama twiga. Mifano hii ni tashibiha kwa sababu inalinganisha vitu kwa kutumia viunganishi.

#### 2.1.1.2 Tashihisi

Ni usemi ambao sifa ya uhai huwa imehamishiwa kwenye kitu kisicho na uhai au dhana dhahania (pengine tashihisi huitwa uhaishaji). Aghalabu, tashihisi ni tamathali

za usemi ambapo vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Wamitila (2003) anaeleza kwamba tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visovyokuwa hai au na uhai huwasilishwa au husawiriwa kwa namna sawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi sawa na afanyavyo binadamu.

Tashihisi hutumiwa zaidi na washairi ambao kwa mfano hawasiti kusema kimya hakishi kunena, kitakapo kusimamia, fedha huita wazuri wakaitika labeka, maji baridi yaliubusu mwili wake mwororo. Katika mifano hii, kimya kimepewa sifa ya kibinadamu ya kunenea na kusimamia, fedha imepewa sifa ya kuita na maji yamepewa sifa ya kubusu. Hivyo neno kimya, fedha na maji vimetumika kama tashititi kwa kupewa uhai. Yaani sifa za vitu vyenye uhai zimehamishiwa kwenye maneno hayo.

#### 2.1.1.3 Taashira

Ni tokeo la uhamishaji wa maana ambao kwao neno fungu huwakilisha kitu, mtu au dhana nyingine yenye uhusiano nalo (Senkoro, 1982). Hii ni aina ya tamathali ya usemi ambapo jina la sehemu ya kitu hutumiwa kuwakilisha kitu kamili au kingine kinachohusiana nacho. Mfano neno ikulu kwa kuwa linahusiana na uraisi hutumika kuwasilisha dhana ya urais, jembe hutumika kuwakilisha mkulima, ukulima au kilimo chenyewe.

Vilevile, tunaposema kuwa mgonjwa ameongezewa chupa nne za damu hatumaanishi kuwa ndani ya mwili wake kumeingizwa chupa nne zenye damu bali damu ya ujazo wa chupa nne ndiyo iliyoongezwa mwilini mwa mgonjwa anayerejelewa. Kanga inaweza kuwakilisha mwanamke.

### 2.1.1.4 Ishara

Ni neno au usemi wenye maana inayowakilisha dhana nyingine kwa kuhusiana nayo. Yaani neno,au usemi huo huwa na viwango viwili vya maana. Katika fasihi dhana ya ishara inatumika kuelezea kitu fulani ambacho huwakilisha kitu kingine. Maana ya moja kwa moja na maana ya kitamathali. Ishara inaweza kuwa na msingi wa kisitiari kama taa mwenge ambayo hutumika kuwakilisha utambuzi, ujuzi n.k au inaweza kuwa na msingi wa kitaashira kama kaburi, jeneza, fuvu amabyo hutumika kuwakilisha mauti (Senkoro, 1982).

### 2.1.1.5 Sitiari

Kahigi (1994) anafasili sitiari kuwa ni uhamishaji wa maana toka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vikoa vya maana vinavyohusika katika uhamishaji huu huwa vinatofautiana angalau kwa sifa ya kisemantiki moja ya msingi. Kinachohamishwa ni tabia au umbo au kazi ya kitu kwa kuihusiha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine (Lakoff & Johnson, 1980). Ili kuielewa dhana ya sitiari, tutumie mfano huu: *Hamisa ni ua*. Katika mfano huu hatumaanishi kuwa *Hamisa* amegeuka kuwa *ua* yaani sehemu ya mmea; bali sifa za *ua* zinahamishiwa kwake.

Yaani, *ua* lina sifa ya uzuri. Kwa hiyo, uzuri unaonasibishwa na ua unahusishwa na *urembo* (*uzuri*) wa *Hamisa*. Muundo wa sitiari una vipengele vitatu: kizungumzwa, kifananisho na kiungo (Lakoff & Johnson, 1980; Kahigi 1994). Kizungumzwa ni kitajwa, ambapo katika mfano wetu ni *Hamisa*; kifananishi ni kitu kinachohusishwa na kizungumzwa na katika mfano wetu ni *ua*, na kiungo ni tabia au sifa zinazounganisha kizungumzwa na kifananishi hapa ni uzuri.

Hivyo basi kwa kuzingatia tamathali za semi zilizobainishwa na Senkoro (2012), utafiti ulichunguza vipengele vya lugha ambavyo vimejikita katika uhamishaji wa maana kutoka katika dhana moja kwenda katika dhana nyingine ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.

#### 2.1.1.6 Tafsida

Ni aina ya tamathali ya usemi na aina anuwai za tasfida. Aina hizo ni: tasifida nasibishi au tasifida tata, tasifida matamshi, tasifida uelekeo, tasifida hifadhi, tasifida nahau na tasifida majina. Tutazijadili aina hizi za tasifida kwa kifupi katika sehemu inayofuata.

Tasifida nasibishi au tasifida tata ni zile zinazotumia maneno ambayo yananasibisha na au kuleta undugu. Aghalabu, maneno haya huweza kuleta utata. Mathalani, haja ya kujisaidia, kulala kwa kufa, kujamiiana kwa kufanya mapenzi, kushiba kwa kula, kufurahi kwa kulia na kadhalika. Tasifida uelekeo hubeba dhana ya uelekeo au mahali. Kwa mfano, kwenda haja. Tasifida matamshi hutokana na kupindisha matamshi yanayotakiwa kwa lengo la kupunguza makali. Kwa mfano, katika Kiswahili tunaweza kuwa na tasifida matamshi kama *umak* badala ya neno *kuma*, *ombo* badala ya neno *mboo*, na kadhalika.

Tasifida hifadhi hutumia maneno yanayoonesha hali ya kitu au jambo kuwa si mbaya sana lakini wakati huo huo ikimaanisha kuwa ni mbaya. Kwa mfano, badala ya kusema kuwa *amesema uongo* tunaweza kusema *nadhani hasemi kweli sana*. Tasifida nahau ni zile zinazoundwa kwa matumizi ya lugha ya kinahau. Kwa mfano,

ametoa rushwa-*amezunguka mbuyu*. Tasifida majina hutumia majina ya watu kumaanisha dhana fulani. Mathalani, *nduli* kumaanisha *mtu katili* na *pilato* kumaanisha *hakimu*. Katika utafiti huu tulibaini kuwa tafsida imetumika kama moja ya tamathali za semi katika mashairi ya shaaban Robert.

## 2.2 Mapitio ya Maandiko Kuhusu Ujinsia kwa Jumla

Senkoro (1982) anasema suala la ujinsia halijashughulikiwa vya kutosha katika uhahakiki wa kifasihi hususan katika fasihi za Kiafrika ikiwa ni pamoja na fasihi ya Kiswahili. Senkoro (keshatajwa) anaeleza kuwa waandishi na wahakiki wengi wa fasihi za Kiafrika wanakumbana na wanawake waliojipamba, wanaonukia manukato makali, waliovalia nguo zinazolenga kuwavutia wanaume ili wawape pesa na kushirikiana nao kimwili lakini wanakwepa kuchunguza na kuhakiki waziwazi ufusika kama sura ya mwanamke katika miji mingi mikubwa baraniAfrika. Aidha, kinachojitokeza hapa ni kwamba waandishi wengi wanamchora mwanamke kama kahaba lakini wengi wao wanafanya hivyo katika kazi za tamthiliya na riwaya.

Oculi (1968) na p’Bitek (1971) wanajadili ujinsia kwa kumchora mwanamke kwa mtazamo hasi kuwa kazi yake nyakati za usiku baada ya kuyakimbia makazi yake ya kijijini na kuingia mjini ni kujiuza ili apate pesa kwa ajili ya matumizi yake. Hali hii inamsukuma Senkoro (1982) kudai kuwa:

*sasa nimeamua kushughulikia usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiafrika iliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza na Kifaransa baada ya kuona kuwa mwanamke kama kahaba na kiumbe duni amejitokeza kama mhusika*

*anayejirudiarudia kwa picha hiyohiyo na amekuwa motifu kuu katika kazi nyingi za fasihi za Kiafrika.*

Sifa ya aina hii inapatilizwa kwa mwanamke na Larson (1973) anaposema; sehemu kubwa ya jamii ya Kenya imejaa wasichana wauza baa wanaotumia muda wao mwingi kuwaliwaza wanaume kwa kuuza miili yao baada ya kazi ya kuuza pombe. Kinachobainika hapa ni kwamba kuna mtazamo potofu uliozaliwa na asasi za kijamii za kumwona mwanamke kama chanzo cha uovu wote wa kijamii bila kuchunguza kwa jicho pevu nafasi ya mwanaume katika kumfanya mwanamke aoneshe tabia zisizofaa. Kitendo cha wanaume kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja hakichukuliwi kuwa ni tatizo katika jamii nyingi za Kiafrika matokeo yake ni kwamba kwa kuwa fasihi ni mtumishi wa jamii, nayo inajikuta inayasawiri mahusiano baina ya wanaume na wanawake na hususan nafasi ya mawanamke katika jamii kwa mtazamo potofu vivyo hivyo. Hivyo basi, kutokana na mawazo hayo, utafiti bhuu ulichunguza ni jinsi gani ujinsia unaibuka katika mashairi ya shaaban Robert kupitia tamathali za semi. Kwa kufanya hivi tuliweza kuona ni namna gani tamathali za semi zinatumiwa katika kuonyesha mahusiano baina ya mwanamke na mwanamme katika jamii.

Wataalamu mbalimbali wameandika machapisho mengi kuhusu mwanamke akiwemo Fleming (1978), mwanakatuni wa Uingereza ambaye alianza kuchora katuni kuhusiana na ufeministi mwaka 1978. Fleming (1978) katika mahojiano hayo, anaeleza kwamba wakati wote wanawake walichorwa vibaya katika vyombo vya habari. Anasema kwamba kwa wanawake hazikuwa habari za kuvutia kabisa kama mwanaume anavyoona vibaya kwa mwanamke kumfanya asiwe na uwezo wa

kuzalisha watoto. Hata hivyo, madhumuni ya mahojiano hayakuchambua nafasi ya mwanamke katika jamii kama mhusika katika mashairi ya Kiswahili, bali kutaka kujua nafasi ya mwanamke mwandishi na mtazamo wa kifeministi. Ijapokuwa mahojiano hayo hayakuchambua nafasi ya mwanamke katika fasihi ya ushairi lakini yalimsaidia mtafiti kuelewa kwa haraka nafasi ya mwanamke na jinsia katika mashairi ya Shaaban Robert inavyochorwa na wasanii wa kike au wa kiume.

Naye Rosalind (2010), mwanamama mcheshi katika makala ya "Ack! Cartoonists and Feminsts Quarrel Over Demise of Cathy" (yaliyochapwa tarehe 20/8/2010) anafafanua kwamba, katika magazeti ya katuni ya miaka ya 1975, wanaume tu ndio waliochorwa kwa mtazamo chanya lakini wanawake walichorwa kama akina mama wa nyumbani au wasichana wauza baa au hoteli. Anamsifu Cathy na kusema ni mwanakatuni mfeministi aliyefungua ukurasa mpya kwa kuanza kumchora mwanamke kwa mtazamo chanya. Anaeleza kwamba wanawake waandishi walipewa nafasi ya pili katika kuhariri katuni lakini wanawake hawakujali ndipo wakaamua kuandika na kuchora kupitia wavuti na tovuti.

Kwa hakika Rosalind hakujadili nafasi ya mwanamke kiundani ila aliandika tu makala kuhusiana na nafasi ya mwanamke katika fani ya uandishi na uchoraji. Hakuchambua nafasi ya mwanamke mhusika kama alivyochorwa katika mashairi hususani mashairi ya Kiswahili ya Shaaban Robert. Hata hivyo kazi ya Rosalind ni muhimu katika kupata ufafanuzi wa nafasi ya mwanamke katika ushairi na pia ilitoa mwanga wa kuwaelewa wanawake na jinsi wanavyoielezea nadharia ya kifeministi ambayo ndiyo iliyotumika katika kuongoza tasnifu. Mapitio haya pia ijapokuwa

hayakujadili nafasi ya mwanamke katika katuni lakini bado yanatoa ufafanuzi mzuri juu ya katuni za ramsa ambazo zinabeba ujumbe kusudiwa kwa njia ya kejeli katika jamii. Tofauti na makala haya, utafiti huu ulichunguza tamathali za semi kama zinavyojitokeza katika vitabu vya mashairi vya shaaban Robert vilivyoteuliwa katika utafiti huu ili kuchunguza namna tamathali hizo zinavyosawiri mahsuiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanaume. Vile vile utafiti huu ulichunguza na kuibua nafasi ya mwanamke kama inavyosawiriwa katika matumizi ya tamathali za semi.

Penguin (1975), IDAF na UNESCO (1988) wanajadili umuhimu wa katuni kwa kuonesha katuni za historia ya Marekani na katuni za kupinga ubaguzi wa rangi Afrika ya Kusini. Kazi hizi tunazitumia katika tasnifu hii kwa sababu hata kama hazihusishi suala la nafasi ya mwanamke moja kwa moja, kwa vile zinashughulikia ubaguzi basi kwa njia moja ama nyingine zinatusaidia kiulinganishi katika kuliangalia suala la usawirishwaji wa mwanamke katika kazi za fashi nchini Tanzania.

Muombwa (1993) katika kazi yake ya “Public Opinion on Political Cartooning in Tanzania” aliangalia mawazo ya umma kuhusu katuni za kisiasa nchini Tanzania. Pia alijaribu kuangalia uhuru wa mwanakatuni; ambapo aliona kuwa 54% ya watu aliowafanyia utafiti Dar es Salaam na Zanzibar walihitaji uhuru wa uchoraji wa katuni za kisiasa uendelee kwa kuwa unafikisha ujumbe kama wafanyavyo waandishi wa habari. Wale waliopinga uhuru wa wanakatuni ambao ni 46% walidai kuwa katuni ziko kinyume cha maadili ya jamii. Kwa ujumla, Muombwa (keshatajwa) anaisaidia kazi ya mtafiti kwani ijapokuwa hakuchunguza nafasi ya

mwanamke katika sanaa hii, lakini anajaribu kubainisha mwitikio wa wanajamii kuhusiana na kazi mbalimbali za fasihi, suala ambalo mtafiti analichunguza hasa katika kipengele cha usawiri wa mwanamke.

Munyogwa (1998) katika tasinifu yake ya "Dhima ya Vikatuni Katika Jamii" amechambua katuni na kueleza dhima zake katika jamii ya Tanzania, kama vile kuelimisha, kuonya, na kuadilisha ikiwa ni pamoja na kuleta burudani ya ucheshi. Hata hivyo, kipengele cha nafasi ya mwanamke hajakigusia wala hakufafanua ujumbe unaobebwa na wahusika hao. Tasinifu imeliziba pengo hilo kwa kiasi kikubwa kwa kuwa utafiti ulichunguza usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili hususan ushairi wa Shaaban Robert.

Wanafasihi mbalimbali wameangalia na kuelezea jinsi lugha ya katuni ilivyo, na matumizi yake katika nyanja mbalimbali, hasa uwanja wa siasa bila kuelezea jinsi wahusika walivyo muhimu katika sanaa ya katuni. Wataalamu hawa wameziangalia katuni kwa jicho la jamiilugha zaidi na sio kifasihi. Hii ndio sababu hawakuweza kuelezea nafasi ya mwanamke katika jamii inavyojidhihirisha katika fasihi picha ya katuni. Hata hivyo kazi zao zina mchango katika kuangalia kipengele cha ucheshi na kejeli katika tasnifu hii kama mbinu mojawapo ya kusawiri mwanawake katika jamii hasa zinazotawaliwa na mfumo dume.

Masoud (2002) katika maoni yake kupitia Chama cha Wanakatuni wa Tanzania, PACT (The Popular Association of Cartoonists in Tanzania), anaeleza jinsi jamii na serikali ilivyozichukulia katuni hapo mwanzo wakati zinaanza na kwa kipindi hiki.

Pia anaeleza athari hasi na chanya za katuni katika jamii ya Tanzania. Masoud anaelezea kwamba kikwazo kikubwa anachokutana nacho ni vikwazo vya wahariri ambao wakati mwingine hawachapishi katuni zake kwa kuwa zinawagusa watu moja kwa moja, hususani wanasiasa ambao hawapendi kukosolewa. Maoni ya Masoud (keshatajwa) yanaijenga kazi hii katika mtazamo chanya wa fasihi ya ushairi, na kuitambulisha kama kazi mojawapo ya kifasihi kwa kuwa inafikisha ujumbe kwa njia ambayo haileti migogoro ndani ya jamii.

Mickey (2002) ambaye pia ni mwanakatuni wa PACT anafafanua kwamba katuni zina vikwazo vingi kwa sababu zinaigusa jamii moja kwa moja, kwa kueleza ukweli. Mfano katuni za Mtume Mohammed, zimeleta mgogogro mkubwa sana miongoni mwa wanajamii wa Kiislamu, kwani inadaiwa kwamba waliozichora ni Maimam walioasi dini na kupoteza muelekeo hivyo na wao wanataka wawapotoshe Waislamu safi. Halikadhalika Mickey (keshatajwa) hakueleza nafasi ya mwanamke katika sanaa hii ya katuni na anahusishwaje katika kufikisha ujumbe kwenye jamii husika jambo ambalo tasnifu hii imekusudia kulifanya.

Jose, Nicholas (2005) ni alihakiki fasihi ya watu wa Australia. Alidai kwamba fasihi ya Australia inachanganya katuni na tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile riwaya, ushairi na tamthilia. Alitoa mfano wa Michael Leuning aliyechanganya ushairi na katuni. Uhakiki wa Jose umemsaidia mtafiti kuchambua data zake ambazo sasa zimethibitisha ukweli kwamba katuni ni fasihi picha na inaweza kuchambuliwa kama tanzu nyingine za fasihi, kwani ni kazi halisi ya kifasihi na inayopaswa kutazamwa kwa jicho la kifasihi.

Senkoro (2008) ametazama lugha ya katuni inavyotumiwa kisitiari. Hata hivyo alieleza tu jinsi katuni zinavyotumiwa na wasanii katika kuielewesha jamii juu ya umuhimu wa lugha yao ya Kiswahili. Mfano:

***Mke:*** *Mume wangu, yaani kusikiliza kipindi cha bunge mpaka umeze panado?*

***Mume:*** *Wabunge wanachanganya sana lugha wananiumiza kichwa*.

Sio wanakatuni tu waliomjadili mwanamke bali hata waandishi wengine ambao wameandika riwaya, tamthilia na ushari. Waandishi hao ni pamoja na Mwanakupona binti Mshamu aliyeandika *Utenzi wa Mwanakupona* uliochapwa na kuhaririwa na Nabhany (1972). Mshamu katika utenzi wake anasisitiza maadili mema na jinsi ambavyo mwanamke anavyotakiwa kuishi na mumewe. Anatakiwa awe mnyenyekevu, mwelekevu na msikivu pale mwanamume anaposema au kutoa amri fulani. Utendi huu umeleta mwanga katika tasnifu hii hasa katika vipengele vya maadili, utamaduni na dini. Kazi hii kubwa ya Mshamu imeleta mwanga hasa katika utamaduni na dini, ambazo ni asasi kongwe zilizomuonea, zilizomtweza na kumnyanyasa mwanamke.

Waandishi wengine ni pamoja na Nawal El Saadawi aliyeandika riwaya ya *Woman at Point Zero* (1983), Elieshi Lema aliyeandika riwaya ya *Parched Earth* (2001), na Ama Ata Aidoo aliyeandika riwaya ya *Changes* (1991). Hawa ni waandishi wanawake waliomchora mwanamke kama jamii ilivyomhesabu. Hata hivyo, mwanamke katika riwaya hizo anaonesha harakati za kujikomboa na kujitoa katika kunyanyaswa, kuonewa na kuwa tegemezi kwa mwanaume, anaondoka na kujitafutia

maisha ya uhuru wake yeye mwenyewe. Kazi za wanawake wanafasihi hawa, zimeijenga tasnifu hii katika kushadidia data za msingi ambazo zilichunguza usawiri wa mwanamke katika ushairi wa Shaaban Robert.

Kwa upande wa tamthilia Penina Mhando ameandika tamthilia nyingi zilizomchora mwanamke kwa namna tofauti tofauti lakini akiwa katika harakati za kujikomboa. Mfano ni tamthilia ya *Nguzo Mama* ambayo inamchora mwanamke anavyotaka kujikomboa lakini anashindwa kufanya hivyo kwa sababu ya kukosa msaada kutoka kwa mwanaume. Tamthilia hiyo ya *Nguzo Mama* imeleta mwanga wa kuona kwamba kumbe mwanamke hata katika tamthilia anachorwa kama mtu anayetaka kujikomboa kutoka katika vifungo vya kunyanyasika, kuonewa na kufanya kazi ambazo hazina mshahara. Jambo la kuvutia kuhusu usawiri wa mwanamke katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* na kwamba Penina Mhando anaonesha pia kuwa ukombozi wa mwanamke na usawiri chanya wa mwanamke unakwamishwa pia na wanawake wenyewe kukosa umoja.

## 2.3 Mapitio ya Machapisho Kuhusu Ujinsia katika Ushairi

Suala la ujinsia katika mashairi limesughulikiwa na wataalamu mabalimbali (Brossard, 1977 na Holmes na Meyerhoff (2003) ambao wanaonesha kuwa kipashio **-e** katika mashairi ya Kifaransa husimamia jinsia ya kike katika vivumishi vyote. Hali hii inajitokeza pia kwa kipashio hiki kinapoambikwa katika nomino kwa lengo la kutofautisha jinsia. Kinachobainika hapa ni kwamba vijenzi mbalimbali vya lugha vinaweza kutumika kubainisha au kutambulisha ujinsia katika ushairi na matumizi ya lugha kwa ujumla. Hivyo, aina ya lugha inayotumiwa na mshairi inatambulisha

aina ya mahusiano na mgawanyo wa majukumu kijinsia baina ya wazungumzaji wa lugha fulani.

Abu-Lughod (1986) anachunguza mashairi yaliyokuwa yanaimbwa na wanawake wa Kibedouin katika muktadha na mazingira ya siri kubwa ili wanachokiwasilisha kisijulikane kwa wanaume. Mashairi yenye mwelekeo huu yalikuwa na lengo la kusambaza mafunzo kwa wanawake ili waweze kupamabana na kupinga ukandamizwaji wao uliofanywa na wanaume. Ukandamizaji huu ulipigiwa chapuo na mashairi yaliyoimbwa na wanaume yakimhimiza mwanamke kuwa mtiifu kwa mwanaume.

Ujinsia ulijibainisha katika mashairi yaliyoimbwa na wanawake na wanaume wa kabila hili kwa kutumia msamiati ulioashiria heshima, mamlaka na chuki ya kutawaliwa na kunyanyaswa. Utafiti huu haukuchunguza tamathali za semi na miundo ya sentensi katika kusawiri nafasi ya mwanamke kwa njia ya ushairi na haukuhusu jamii ya Waswahili wanaopatikana katika upwa wa Afrika Mashariki. Vilevile, utafiti wa Abu-Lughod (keshatajwa) haukushughulikia nafasi ya tamathali za semi katika kusawiri nafasi ya mwanamke katika jamii ya Waswahili. Pengo hili ndilo ambalo utafiti huu ulitarajia kuliziba kwa kuibua nafasi ya mwanamke na namna ilivyosawiriwa katika mashairi ya shaaban Robert.

Feld (1982) na Briggs (1992) wamechunguza hali mbalimbali zinazoonesha namna wanawake walivyotumia nafasi ya matukio kama kifo ambapo wakati wa mazishi walipewa nafasi ya kuimba nyimbo za maombolezo na kuzigeuza kuwa jukwaa la

kutoa malalamiko dhidi ya unyanyasaji wa wanaume dhidi ya wanawake kupitia shughuli za kisiasa na kiuchumi. Kufuatia unyanyasaji wa wanawake uliofanywa na wanaume, Sherzer (1987), alibaini pia kuwa wanawake wa Kiwarao walikuwa wakilalamikia vitendo kandamizi vilivyofanywa dhidi yao na wanaume kama ilivyoelezwa na Feld na Briggs (weshatajwa). Briggs (1992) anafafanua kuwa wanawake wa Kiwarao mara kwa mara walitumia nafasi adimu ya kuonesha ngoma za maombolezo mbele ya umma kupaza sauti za kupinga ukiritimba wa kijamii na sera zilizowapa fursa wanaume kuwanyanyasa wanawake. Vilevile, Hirsch (1998) anaeleza kuwa wanawake Waisilamu katika maeneo mengi ya Kusini mwa Afrika walitumia fursa adimu kuimba mashairi na kutongoa hadithi katika mahakama za Kiisilamu kama njia ya kupaza sauti dhidi ya wanaume. Tunachojifunza hapa ni kwamba lugha ya kishairi imekuwa ikitumika kwa namna mbalimbali kumkandamiza na kumkomboa mwanamke vilevile. Hivyo, suala la ujinsia katika ushairi lina historia ndefu.

Aidha, Coplan (1987) naye alibaini kuwa wanawake wa Lesotho walipinga kunyanyaswa na wanaume kwa kutumia mashairi. Mantiki ya kutambua tofauti za kiitikadi kwa kuzingatia jinsi imesababisha kuwepo kwa mijadala ya kiitikadi kuhusu tofauti kati ya wanawake wenyewe na tofauti baina ya wanaume na wanawake kwa kutumia tanzu mbalimbali za fasihi ikwa ni pamoja na ushairi. Tunachojifunza kutokana na utafiti Coplan (keshatajwa) ni kwamba wanawake wanatofautiana katika kuufasili ulimwengu kutegemeana na nafasi yao katika jamii. Tofauti na Coplan, utafiti huu ulichunguza mashairi ya shaaban Robert ili kuona ni namna gani suala la ujinsia linasawiriwa kupitia tamathali za usemi.

P'Bitek (1974) na Akivaga na Odaga (1982) katika tafiti zao kuhusu mashairi na michezo ya watoto wanaishia kuonesha tu kuwa jinsi zote mbili zina nafasi ya kushiriki katika kuimba mashairi. p'Bitek (keshatajwa) anaeleza kuwa katika mchezo wa kutafutana, watoto wote huimba na kwamba kila mmoja bila kujali jinsia yake anaweza kuwa kiongozi. Kwa upande wake, Odaga (keshatajwa) anauchukulia ushairi wa watoto kuwa ni nyimbo na michezo ya watoto na kwamba kila mtoto ana fursa ya kuwa mwimbashaji wa shairi bila kujali jinsia yake. Watafiti hawa wanapuuza ujinsia unaojitokeza katika ushairi wa Kiafrika ambapo kwa muda mrefu mwanamke amekuwa akiathiriwa na mifumo kandamizi inayosawiriwa katika ushairi huo ikiwa ni pamoja na ushairi wa Kiswahili.

Alembi (1991) anatofautiana na p'Bitek (1974) na Odaga (1985) kwa kueleza kuwa kuna usawiri wa mahusiano ya kijinsia katika ushairi wa michezo ya watoto katika jamii nyingi za Kiafrika. Anatoa mfano wa ushairi wa watoto wa jamii ya Maragoli ambapo watoto hubebana mgongoni, mtoto aliyebebwa mgongoni huimba shairi akiuliza anakopelekwa na motto mwenzake aliyembeba. Mtoto aliyembeba mwenzake huimba akimweleza mwenzake kuwa anampeleka kwa wakwe zake kwani amekwishaolewa. Ujinsia unajitokeza waziwazi katika ushairi wa watoto wa jamii ya Maragoli kwani wasichana huandaliwa kwa kutumia ushairi huu wa michezo ya watoto kuwa siku moja wataolewa na wazazi wao watapewa mahari ya ng'ombe, mbuzi au kondoo wanane.

Ujinsia unajitokeza pia hata kati ya watunzi wa mashairi katika sehemu mbalimbali ulimwenguni (Wolkoff, 2011). Mathalani, mashairi ya Atwood yamekabiliwa na

kukataliwa na jamii ya Canada na maeneo mengine kwa sababu tu kwamba yametungwa na mwanamke. Kwa hiyo, suala la ujinsia linakwenda mbali zaidi ya usawiri wa mwanamke kwa kutumia lugha katika mashairi. Nafasi ya mwanamke katika medani ya ushairi imekabiliwa na upinzani pia. Kwa vyovyote vile, lugha inayotumika kumchora mwanamke kati ushairi ni chanzo cha kukataliwa pia kwa mashairi yaliyotungwa na washairi wanawake katika kipindi cha miaka ya 1930-1940. Kwa hiyo, usawiri wa mwanamke katika mashairi mengi miongoni mwa jamii za Waswahili si suala la bahati mbaya bali ni la kimfumo kwani mila, desturi, siasa, uchumi na utamaduni vimempuuza mwanamke kwa karne nyingi na hii ndiyo sababu ya kusawiriwa kwa mwanamke kwa mtazamo hasi na washairi wengi. Utafiti huu umefanyika kwa lengo la kuchunguza ni namna gani tamathali za semi kama vipengele vya lugha zinatumika kumchora mwanamke na kumweka mwanamke katika nafasi inayompa heshima na uwezo wa kutenda sawa na wanaume katika kazi mbalimbali ushairi ukiwa miongoni mwazo.

Momanyi (2007) anaeleza kuwa katika jamii kama ya Waswahili kuna sera au itikadi zinazohalalisha ukiritimba wa wanaume unaoegemezwa kwa kutumia kaida za kiutamaduni, dini na tofautimza kijinsia ambazo zinajidhihirisha pia katika uchambuzi wa tanzu za fasihi kama ushairi. Kwa muda mrefu, wanaume katika jamii ya Waswahili wamekuwa watawala wa utamaduni kupitia mfumo dume ambapo lugha inatumika kufasili ujinsia kama tofauti iliyopo baina ya wanaume na wanawake. Kimsingi, tofauti hizi katika jamii nyingi zinatumiwa kwa hila kijamii na kiutamaduni na mifumo dume kunakojumuisha unyanyapaa unaotetewa na wanaume kwa kuzingatia tofauti za kijinsia. Kinachoonekana katika jamii mbalimbali ni

kwamba nafasi ya wanawake ni kuunga mkono itikadi za wanaume na wameamilia hali hii na kitu kinachovutia zaidi ni kwamba hali hii imekuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku. Momanyi (keshatajwa) anaeleza pia kuwa tofauti na jamii nyingine, jamii ya Waswahili imekuwa ikitumia vipengele na miundo ya kifasihi kutetea *u-ume* ili kulinda nafasi kandamizi ya wanaume.

Momanyi (2007) ameshughulikia kwa kina ujinsia unaojitokeza katika ushairi wa Kiswahili kwa kuteua mashairi matatu: *Wananambia Mchafu* (Said Ahmed Mohamed, 1983), *Mwanakupona* na *Al-Inkishafi* lililoandikwa na Sayyid Abdalla bin Ali bin Nassir (1720-1820). Uchunguzi wa kina umeonesha kuwa Momanyi (keshatjwa) katika uchambuzi wake wa ujinsia katika ushairi hakuchambua mashairi ya Shaaban Robert.

Wahakiki wengine kama Njozi (1990:63), Senkoro (1988) na Mulokozi (1982) nao wamechambua ujinsia katika ushairi kwa kutumia mashairi haya matatu. Kinachobainika pia ni kwamba utafiti wao ulijielekeza kuihakiki taasisi ya dini ya Kiislamu jinsi inavyomkandamiza mwanamke katika jamii ya Waswahili. Utafiti huu utajipambanua na tafiti zilizotangulia kwa kuchunguza tamathali za semi na nafasi yake katika kubainisha ujinsia na namna unvyosawiriwa kupitia tamathali za semi zilizotumika katika mashairi ya Shaaban Robert.

Khatibu (1985) anafafanua kuwa lugha ya ushairi inayombeza na kumdunisha mwanamke inaathari kubwa katika masuala mbalimbali ya kijamii kama haki ya wanawake kurithi ardhi na fursa ya kwenda shule. Anaendelea kueleza kuwa utenzi

wa Mwanakupona ni utenzi wenye sumu katika majaliwa ya mwanamke. Hii ni kutokana na lugha yake inayohalalisha unyanyasaji na utumwa wa wanawake katika jamii. Momanyi (1998) anasisitiza kuwa matumizi ya lugha ya kishairi inayoendeleza mfumo dume ni matokeo ya uchumi uliotegemea pesa ambapo wamiliki wake waliweza kumiliki kila kitu ikiwa ni pamoja na fasihi. Kwa kuwa fasihi ni mali ya jamii, ililazimika kuwasilisha hali halisi ya mahusiano baina ya wanawake na wanaume katika jamii. Uchumi, siasa na fasihi vilimilikiwa na wanaume kwa muda mrefu na wanawake waliponyimwa fursa ya kuumiliki walilazimika kukimbilia mijini na kuwafanya baadhi yao waanze kufanya ukahaba ili waweze kupata pesa za kukidhi mahitaji yao ya msingi.

Low (2011) anachunguza mashairi ya muziki wa kizazi kipya yanayohusu UKIMWI. Katika utafiti wake amechunguza aina ya lugha inayotumika katika kuibua dhamira mbalimbali. Tofauti na utafiti huu, utafiti wa Low (keshatajwa) haukuchunguza jinsi matumizi ya lugha yanavyosawiri ujinsia katika ushairi wa Kiswahili. Hivyo, utafiti huu unalenga kuchunguza athari za lugha ya kishairi katika kusawiri ujinsia katika mashairi ya Shaaban Robert.

Jilala (2010/2012) katika makala yake ya lugha na ujinsia katika ushairi, alijikita katika kuchunguza kipengele kimoja tu cha tamathali za semi ambacho ni sitiari. Uchunguzi wake ulizingatia sitiari za UKIMWI na mapenzi katika mashairi ya bongo fleva. Katika makala yake anajadili kuwa sitiari zinazomrejelea mwanamke zimebeba dhana tano ambazo zimeundwa kitaswira kumuashiria mwanamke na nafasi yake katika jamii. Dhana hizo ni uzuri, utamu, tahamani, mvutio na utoto

ambazo hutumika kitaswira kumdhalilisha na kumdunisha mwanamke kwa kumpa dhima hasi katika jamii. Katika makala yake anahitimisha kuwa sitiari zinazotumiwa katika muziki wa kizazi kipya huonyesha uhusiano hasi baina ya mwanamke na mwanaume. Sitairi zinazomrejelea mwanamke zimeundwa kitaswira na kumchora kitaswira kwa kumpa dhima na nafasi inayomdunisha na kumdhalilisha wakati mwanaume hubeba taswira ya uhodari, ushujaa na mwenye maamuzi binafsi. Tofauti na makala ya Jilala, ambaye alijikita katika kuchunguza sitiari peke yake, utafiti huu utapanua wigo na kuchunguza kwa kina tamathali zingine na sitiari ikiwemo ili kuona ni jinsi gani tamathali hizo zinasawiri suala la ujinsia katika mashairi ya Shaaban Robert.

Kwa upande wake, Mulokozi (1996) anajadili aina mbalimbali za nyimbo zinazojitokeza katika fasihi simulizi ya Kiafrika. Zaidi ya kutaja aina, Mulokozi (keshatajwa) anabainisha dhima ya kila aina ya nyimbo anazotaja. Katika utafiti wake, Mulokozi anasema kwamba nyimbo zina nguvu kubwa katika kuelimisha na kuburudisha. Anabainisha jinsi mbinu za kifani ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha ya kisanaa zinavyosaidia kuibua maudhui. Aidha, utafiti wa mwanazuoni huyu hauzungumzii kwa kina jinsi matumizi ya lugha yanavyobainisha ujinsia hususan nafasi ya mwanamke katika jamii kwa kutumia tamathali za semi. Vilevile, utafiti wa Mulokozi haukuchunguza matumizi ya lugha katika mashairi ya Shaaban Robert na nafasi yake katika kusawiri ujinsia katika jamii. Kutokana na pengo hili, mtafiti alivutiwa kufanya utafiti kuhusu matumizi ya tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert kwa lengo la kuchunguza nafasi yake katika kusawiri ujinsia.

## 2.4 Tafiti Kuhusu Kazi za Shaaban Robert

Baadhi ya watafiti wamefanya tafiti kuhusu maandiko ya Shaaban Robert, watafiti hao ni kama vile Ponera (2010) alifanya utafiti kuhusu ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert, katika utafiti wake alihitimisha kuwa nathari za Shaaban Robert zimetumia mbinu ya ufutuhi kama mbinu ya kisanii ya kuwasilisha ujumbe katika jamii. Hata hivyo, Ponera hakushughulikia suala la ujinsia suala ambalo utafiti huu umelishughulikia kwa kina. Kwa upande mwingine Chua Chua (2010) alifanya utafiti kuhusu itikadi za maandiko ya Shaaban Robert. Katika utafiti wake alihitimisha kuwa Shaaban Robert ametumia itikadi ya kifalsafa katika kuzungumzia masuala ya kijamii. Utafiti wa Chua Chua (keshatajwa) ni tofauti na utafiti huu kwa sababu utafiti huu ulijikita katika masuala ya kijinsia katika mashairi ya Shaaban Robert tofauti na Chua Chua ambaye alijikita katika masuala ya itikadi katika kazi za Shaaban Robert. Kwa upande mwingine Momanyi (2001) alichunguza masuala ya kijinsia katika nathari za Shaaban Robert na kuhitimisha kuwa Shaaban Robert anaendeleza mfumo dume na anatumia kazi za fasihi kumkandamiza mwanamke. Utafiti huu utachunguza kazi za mashairi tofauti na makala ya Momanyi ambaye alishughulikia nathari. Vile vile, utafiti huu umechunguza endapo Shaaban Robert anatumia pia mashairi kukandamiza mwanamke kama alivyogundua Momanyi katika utafiti wake wa nathari.

## 2.5 Mwega wa Kinadharia

Kuna nadharia mbalimbali ambazo hutumika kuchambua lugha katika kazi za fasihi. Makala hii inatumia nadharia ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike (*Feminist Psychoanalytic Theory*). Hii ni nadharia iliyoibuka kutokana na kazi

zilizoasisiwa na Jacques Lacan (1977) kama alivyonukuliwwa na Momanyi (2001). Nadharia hii inahakiki matini katika misingi ya uchanganuzi nafsia. Huzingatia kuweko kwa nafsi bandia au nafsi isiyo halisi iliyojengwa kutokana na mielekeo ya kiuana, utaratibu fiche wa kisaikolojia pamoja na taasubi za kiume.

Katika utaratibu fiche, maumbo halisi ya kiisimu katika akili ya mwanamke hughubikwa na badala yake maumbo ya kidhahania huimarishwa. Maumbo haya yasiyo na uhusianao wowote na uhalisia wake kama binadamu ndiyo yanayobainika hususan kupitia lugha na tabia yake. Utaratibu huu ambao ni wa kiishara ndio unaoashiria tofauti za kiuana zinazopatikana katika utamaduni wa jamii.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, nafasi ya mwanamke imefungamana na lugha inayomzungumzia, lugha inayoashiria uana wake. Nafasi hii hufinyangwa na jamii kupitia asasi mbalimbali za kijamii kama vile ndoa na dini ili aweze kukubalika katika utaratibu huo wa kiishara. Uchanganuzi nafsia katika mtazamo wa kike basi, ni nadharia bia ya uumbaji wa nafsi katika misingi ya uana.

Sababu ya kuteua nadharia hii ni kwamba inaweza kutumika kuonesha utambulisho wa uana wa wanawake kutokana na matumizi ya lugha katika mawasiliano yao wanapohusiana na wanaume. Vilevile, nadharia hii inafaa kuchunguza lugha inayotumiwa na wanaume katika kuwatambulisha wanawake katika mahusiano mbalimbali ya kijamii. Wapo watafiti ambao pia wametumia nadharia hii katika kuchambua mahusiano ya mwanamke na mwanamume katika kazi za fasihi, mathalani, Momanyi (2001). Na hatimaye nadharia hii iliweza kuwafikisha kwenye

mafanikio katika kuibua suala la ujinsia katika fasihi. Hivyo nadharia hii inaweza kutumika katika kuchambua ujinsia, suala la ujinsia linavyosawiriwa na lugha katika mashairi ya Shaaban Robert.

Katika muktadha wa uchambuzi wa matini za mashairi ya Shaaban Robert, nadharia hii ilitumiwa kwa kuzingatia kwamba lugha haiwakilishi uhalisia bali ni utaratibu wa kiishara. Hivyo, taswira za wanawake katika fasihi aghalabu haziwakilishi uhalisi wao bali ni taswira bandia zilizosheheni ishara za uana, hususani katika matumizi ya lugha. Aidha, uhakiki huo una wajibu wa kuzingatia kuwepo kwa taasubi za kiume zilizoimarishwa ndani ya utaratibu wa kiishara katika mfumo wa kuumeni. Taasubi hizo ndizo zinazomdunisha mwanamke na kumweka katika kitengo maalumu kijamii (Momanyi, (2001). Nadharia hii ilitumika pia kujadili jinsi lugha ya kiishara inavyotumika kuonesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanamume katika jamii.

Kwa kutumia nadharia hii tuliweza kuonyesha ni jinsi gani mwanamke anachorwa kiishara kwa kutumia tamathali za semi katika mashairi ya vitabu teule yaliyotungwa na Shaaban Robert. Aidha, nadharia hii ilitusaidia katika kujadili ishara ambazo zinaibuka kutokana na lugha iliyotumika katika mashairi ya Shaaban Robert.

# SURA YA TATU

# 3.0 MUUNDO NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muundo na mbinu za utafiti zilizotumika katika mchakato wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Sura imegawanyika katika sehemu kuu saba. Sehemu ya kwanza inaelezea mkabala wa utafiti, sehemu ya pili ni eneo la utafiti, sehemu ya tatu ni walengwa wa utafiti, sehemu ya nne sampuli iliyotumika katika utafiti, sehemu ya tano ni mbinu za ukusanyaji wa data, sehemu ya sita ni mbinu za uchambuzi wa data, sehemu ya saba ni hitimisho.

## 3.2 Mkabala wa Utafiti

Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza matumizi ya tamathali za semi katika kusawiri ujinsia kama zilivyotumika katika mashairi ya Shaaban Robert yanayopatikana katika vitabu vyake vya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* na *Pambo la Lugha*. Mtafiti alichunguza tamathali za semi zinazopatika katika vitabu teule, nafasi ya tamathali katika kusawiri ujinsia na mchango wa tamathali katika kuonesha nafasi ya mwanamke katika jamii. Malengo ya utafiti huu yamefikiwa kwa kutumia mikabala ya uwandani na kimaelezo.

Mkabala wa uwandani unafasiliwa kuwa ni mchakato ambao mtafiti hujenga mahusiano ya namna mbalimbali kwa muda mrefu na jamii ya watu watakaotafitiwa katika mazingira yao ya asili kwa lengo la kuweka uelewa wa kisayansi kuhusu jamii hiyo (taz. Lofland na Lofland, 1984). Katika mkabala wa uwandani, mtafiti

anatakiwa kwenda katika eneo la utafiti kuchunguza jambo linalotafitiwa katika hali yake halisi.

Trochm (1999) anaeleza kuwa mkabala wa uwandani humwezesha mtafiti kukusanya data za kutosha zinazomwezesha kufanya majumuisho ya matokeo ya utafiti wake na kueleza uhalisia uliopo. Ubora wa mkabala huu unatokana na ukweli kwamba unatoa nafasi kwa mtafiti kushughulikia kwa kina masuala anayoyatafiti katika jamii. Kwa hiyo, kuna nafasi kubwa kwa mtafiti kukusanya data pana ambayo inafaa kujibu maswali yake ya utafiti baada ya kuchambua data hizo. Kwa kutumia mkabala huu wa uwandani mtafiti alikusanya data kwa sampuli ya watafitiwa iliyoteuliwa.

Mtafiti alitumia pia mkabala wa kimaelezo. Kothari (1990, 2004) anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo unazingatia umuhimu wa kufafanua namna watu wanavyofikiri kuhusu hali, kitu au jambo fulani na kutathmini hisia za watu juu ya hali, kitu au jambo hilo. Kwa hiyo, mkabala huu ulitumika kueleza tabia na hisia za mtu, kundi au jamii fulani ya watu na kufafanua hali iliyopo kwa wakati huo. Mkabala huu umefaa katika utafiti huu kwa sababu umesaidia kufafanua taarifa mbalimbali zinazohusu silka, hulka, mwenendo, mitazamo, tabia, mawazo, maoni, imani na masuala mengine ya kijamii hasa yale yanayohusu taratibu za maisha ya kila siku miongoni mwa wanafasihi na wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili. Mkabala huu ulitumika kuelezea tamathali za semi, aina za tamathali za semi, usawiri wa ujinsia kwa kutumia tamathali za semi na nafasi ya tamathali katika kuonesha nafasi ya mwanamke katika jamii.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu wa matumizi ya tamathali za semi na usawiri wa ujinsia katika mashairi ya Shaaban Robert ulifanyika katika jiji la Dar es Salaam hususan katika shule za Sekondari za Shaaban Robert, Jangwani na Tambaza. Vilevile, utafiti huu ulijielekeza katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Slaam (TATAKI) na shuke za sekondari za Shaaban Robert na Jangwani.

Mtafiti alivutiwa kufanya utafiti katika eneo hili kwa sababu ni rahisi kupata data zinazohusu mashairi ya Shaaban Robert kwa kuzingatia kuwa Mkataba Kuu ya Taifa iko katika jiji hili na kwamba kuna shule moja ambayo imepewa jina la msanii huyu kama njia ya kumuenzi yeye binafsi na kazi alizowahi kutunga. Aidha, katika jiji hili kuna taasisi nyingi zinazojishughulisha na ufundishaji, utafiti na ushauri wa fasihi ya Kiswahili kwa kiwango cha juu. Hivyo, ni rahisi kupata taarifa nyingi kuhusu historia ya msanii huyu na maendeleo yake katika uandishi wa ushairi; taarifa ambazo ni muhimu katika kuhusisha historia na athari yake katika mlengo wa uandishi wa kazi zake za ushairi.

Aidha, sehemu hii ina mchanganyiko wa wazungumzaji, washairi, walimu na watafiti wa ushairi wanaotoka katika jamii mbalimbali. Uchunguzi binafsi umeonesha kuwa kuna wanafunzi wengi wanaosoma fasihi ya Kiswahili katika vyuo mbalimbali katika jiji la Dar es Salaam kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Mchanganyiko huo wa wanafunzi na wanazuoni unatokana na lugha ya Kiswahili kuwa kivutio na ni lugha ya mawasiliano na lugha rasmi katika nchi za Ukanda wa

Maziwa Makuu. Hivyo, watu wengi wanavutiwa kujifunza fasihi ya Kiswahili ili waweze kujua utamaduni wa Waswahili kupitia fasihi yao.

## 3.4 Kundi Lengwa

Kulingana na Cooper (1989) and Vans (1990) kundi lengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti (Kothari, 2004; Bryman, 2004; Komba na Tromp, 2006). Walengwa waliohusishwa katika utafiti huu ni walimu na wanafunzi wa fasihi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hususani idara ya fasihi na uchapishaji iliyoko chini ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wanafunzi wa shule za sekondari Shaaban Robert na Jangwani ambao wanasoma fasihi ya kiswahili.

Kundi lengwa la utafiti huu liliteuliwa kulingana na sifa na umuhimu wa kila kundi katika utafiti huu. Kwa mfano, wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam waliteuliwa kulingana na sifa ya kuwa ni wanafunzi wanaosoma fasihi, wana maarifa na uzoefu katika uchambuzi wa kazi za fasihi na pia wana ujuzi na maarifa katika matumizi ya nadharia na mbinu za uhakiki wa kazi za fasihi. Hivyo basi, utafiti huu uliliona kundi hili kuwa ndilo lenye uwezo wa kutoa data juu ya ujinsia katika mashairi. Vile vile kigezo cha kuwa wanafunzi hawa wanasoma ushairi wa Kiswahili kilimfanya mtafiti aweze kuliona kundi hili kuwa ni raslimali ya kutosha katika utoaji wa data za utafiti huu. Sifa nyingine iliyowafanya wanafunzi wa fasihi Chuo Kikuu cha Dar es salaam wateuliwe kuwa walengwa wa utafiti huu ni

kwa sababu: pamoja na kuwa mtafiti ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria lakini aliona wanafunzi wa fasihi Chuo Kikuu cha Dar es salaam walifaa kutumiwa katika utafiti huu tofauti na wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria kwa sababu wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria si rahisi kuwapata kwani wanasoma kwa njia ya elimu masafa. Hivyo hakuna sehemu mahsusi ambayo mtafiti angeweza kuwapata kwa urahisi. Wakati huo huo ilikuwa rahisi kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwa sababu wanasoma darasani na kuna eneo mahsusi unaloweza kuwapata na kuwatambua kuwa hawa ni wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi, sababu hizi ndizo zilizomfanya mtafiti kuchagua wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaamu kuwa wahojiwa wake katika utafiti huu.

Kwa upande mwingine, wahadhiri wa fasihi wa muda mrefu walionekana kuwa ni kundi muhimu katika utafiti huu kwa sababu wao ndio wanaofundisha kozi ya fasihi, wana ujuzi na maarifa katika nadharia na vitendo kuhusu fasihi ya Kiswahili na uhakiki wa kazi za fasihi kwa ujumla.

Kutokana na mwingiliano huu wa jamii mbalimbali, mtafiti alionelea kuwa huenda wakawa na mitazamo tofautitofauti kuhusu matumizi ya tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert. Hivyo, utafiti huu ulichunguza matumizi ya tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert zilivyotumiwa na msanii huyu kwa kuchunguza maoni, mtazamo na uelewa wa wadau wa fasihi ya Kiswahili kutoka Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), Shule ya Sekondari ya Shaaban Robert na Shule ya Sekondari ya Jangwani. Jedwali namba 1 linaonesha mgawanyo wa watafitiwa kwa kigezo cha umri.

**Jedwari 3.1**: **Mgawanyo wa Watafitiwa kwa Kuzingatia Kitengo na Umri**

| Eneo | Taasisi | Vijana | Watu Wazima | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Jiji la Dar es Salaam | Walimu wa fasihi TATAKI | 5 | 5 | **10** |
| | Wanafunzi wa fasihi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | 10 | 10 | **20** |
| | Shule ya Sekondari Shaaban Robert | 15 | 15 | **30** |
| | Shule ya Sekondari Jngwani | 15 | 15 | **30** |

***Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti***

## 3.5 Sampuli na Usampulishaji

### 3.5.1 Sampuli ya Watafitiwa

Kwa mujibu wa Kothari (1990, 2004) sampuli ya watafitiwa ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili kutoa majumuisho ya utafiti wake. Watafitiwa ni dhana inayotumiwa katika taaluma ya utafiti kurejelea watu au vitu vinavyoteuliwa na kuchaguliwa na mtafiti kwa ajili ya kufanyia utafiti wake kwa kuzingatia aina na malengo ya utafiti anaokusudia kufanya. Usampulishaji ni mchakato unaohusisha mbinu mbalimbali za uteuzi wa watafitiwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa kwa lengo la kumpatia mtafiti taarifa ambazo atazitumia kutoa majumuisho yanayowakilisha kundi kubwa la watafitiwa (Trochim, 2006). Mchakato wa kuteua sampuli kutoka katika kundi lengwa inajulikuana kama mbinu ya uteuzi wa sampuli. Kwa vile siyo rahisi kukusanya taarifa zote kutoka kwenye kundi zima, basi, mbinu yenye madhumuni maalumu na mbinu bahatishi zilitumika kukusanya data. Mbinu yenye madhumuni maalumu na dhamira zinahusisha uteuzi wa vitu kama sampuli unaofanywa na mtafiti kwa mtafiti kwa madhumuni maalumu

na dhamira kutegemeana na taarifa zinazohitajika kupatikana kwa ajili ya utafiti (Kothari, 1990; Babbie, 1992).

Sampuli ni istilahi inayotumika kumaanisha watu walioteuliwa kujibu maswali ya utafiti kutoka katika kundi (Kothari, 1990). Katika utafiti huu siyo rahisi kuhusisha walimu wote wa vyuo vikuu hivyo, katika makundi hayo mtafiti aliteua sampuli ambayo imejibu maswali aliyolenga kwenye utafiti huu.

Kothari (1990, 2004) anabainisha aina nane za usampulishaji ambazo ni: usampulishaji nasibu, usampulishaji usio nasibu, usampulishaji mwandamano, usampulishaji wa kimfumo, usampulishaji kikomo, usampulishaji kishada/kundi na eneo, usampulishaji mahuluti na usampulishaji nasibu tabakishi. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi, usampulishaji wa kimfumona usampulishaji wenye madhumuni maalumu.

#### 3.5.1.1 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu

Mtafiti alitumia mbinu yenye madhumuni maalumu kuteua sampuli ya utafiti huu. Uteuzi sampuli kwa kigezo cha madhumuni maalumu ni uteuzi wa sampuli kwa kuzingatia sababu mahsusi. Kombo na Tromp (2006) wanasema, ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu ambao anaamini kuwa ni raslimali anayoitegemea katika utafiti wake. Kwa hiyo, mbinu hii ilikuwa bora na ya muhimu katika utafiti huu kwa sababu baadhi ya watu katika kundi lengwa walikuwa na uwezo na ni raslimali kubwa katika data za utafiti huu kulikoni wengine. Kwa mfano suala la kiwango cha ufahamu wa fasihi, nadharia na uhakiki (kati ya

wanafunzi wanaosoma kozi ya ushairi na wale wasiosoma kozi hiyo, wanafunzi wanaosoma fasihi na wale wasiosoma fasihi, kati ya walimu wa kozi ya fasihi hususani ushairi na walimu wa isimu au wale wasio walimu wa ushairi) ilitofautiana kulingana na ubobezi katika fani husika. Kwa maana hiyo, mtu ambaye hakuwa na maarifa ya fasihi nadharia na uhakiki alionekana hafai katika kutoa data za utafiti huu. Powell na Connaway (2004) anasema kuwa katika uteuzi wenye madhumuni maalum sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo ambavyo vinahusiana na maswali ya utafiti kulikoni kigezo cha uteuzi nasibu au wa kubahatisha. Hivyo basi, Katika mbinu hii wahojiwa huteuliwa kwa madhumuni maalumu kutokana na nafasi zao kwa imani kuwa ndio raslimali ya data ya utafiti na mtafiti anawategemea ili kupata data toshelevu.

Sababu nyingine ambayo ilimfanya mtafiti kutumia mbinu hii ni kwamba: mtafiti alikuwa na taarifa juu ya kuwepo kwa makundi yenye ujuzi, maarifa na uzoefu katika fasihi ya Kiswahili na ushairi wa Kiswahili, makundi haya ndiyo raslimali ya data ya utafiti huu. Hivyo basi, mbinu hii ilitumika kuteua sampuli kutoka kwa walengwa wa utafiti huu. Kwa mfano, kwa kuzingatia kigezo hicho, wanafunzi wa fasihi waliteuliwa kwa kuzingatia kigezo kuwa wanauelewa juu ya nadharia na uhakiki wa fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi, wanafunzi hao walionekana kufaa katika kutoa data za utafiti huu tofauti na wale ambao hawajasoma kozi hiyo.

Aidha, walimu wa fasihi walionekana kufaa zaidi katika utafiti huu kwa sababu ilieleweka kuwa wana misingi ya nadharia za uhakiki na uchambuzi wa fasihi ya Kiswahili tofauti na walimu wa kozi za isimu.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wanaosoma ushairi wa Kiswahili waliteuliwa kwa kigezo kuwa wanaelewa nadharia mbalimbali za uchambuzi wa ushairi wa Kiswahili. Waliteuliwa kwa vigezo kuwa wana maarifa ya ushairi wa Kiswahili, historia na mabadiliko yake na hivyo wana uwezo na stadi za uchambuzi wa maudhui na fani katika mashairi. Kigezo hiki pia kilitumika kumtofautisha mwalimu wa fasihi aliyebobea katika ushairi kwa kuzingatia kuwa alikuwa na uzoefu na maarifa na uelewa juu ya nadharia za uchambuzi na uhakiki wa ushairi.

Kwa ujumla mbinu ya uteuzi kwa madhumuni maalumu ilimsaidia mtafiti kupata sampuli ya watu wenye uzoefu, stadi na maarifa katika nadharia na uhakiki wa fasihi na ushairi wa Kiswahili na isimu ya lugha kwa ujumla wake na hatimaye kupata data ambazo zimekuwa ni mhimili wa utafiti huu. Vile vile data zilizopatikana kwa makundi hayo zilimsaidia mtafiti kupata na kufanya majumuisho mahususi kulingana na malengo ya utafiti.

#### 3.5.1.2 Usampulishaji wa Kimfumo

Hutumia mbinu ya kuamua kigezi cha msingi kisha mtafiti huamua kuteua sampuli ya utafiti kwa kuchukua namba kwa kuzingatia vigawe linganifu kama vile 5, 10 au 15 kila baada ya kuchagua sampuli ya kwanza, ya pili na kadhalika. Ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu ambao anaamini kuwa ni raslimali anayoitegemea katika utafiti wake (Kombo na Tromp, 2006). Sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba mtafiti ana taarifa juu ya uwepo wa walimu wanaofundisha kozi ya fasihi hususani ushairi na wapo pia wanafunzi wanaojifunza kozi ya fasihi hususani ushairi. Hivyo basi, mtafiti anaamini kuwa kundi hilo ndilo

walengwa wanaoweza kutoa data na mtafiti anaamini kuwa utafiti huu unawategemea watu hao ili kupata data toshelevu.

#### 3.5.1.3 Usampulishaji Nasibu Tabakishi

Ni mbinu ya usampulishaji ambapo kila sampuli katika idadi kubwa ya kundi la watu ina fursa ya kuteuliwa kuwa sampuli ya utafiti. Utafiti huu ulitumia *usampulishaji nasibu tabakishi*. Mbinu hii ilitumika kuwateua wanafunzi wa sekondari na wanafunzi wa vyuo vikuu wanaosoma fasihi hususani kozi ya ushairi. Mtafiti aliteua mbinu hii kwa kuwa inazingatia uwakilishi sawa wa makundi mbalimbali ya kijamii. Kwa kutumia mbinu hii, watafitiwa 90 waligawanywa katika idadi isiyo sawa kwa kuzingatia kigezo cha umri.

Idadi ya watafitiwa haikulingana katika baadhi ya vigezo kwa kuzingatia kuwa wadau wa fasihi wanatofautiana kiidadi. Hii ina maana kuwa idadi ya walimu wa fasihi si sawa na idadi ya wanafunzi wa fasihi katika taasisi zilizoteuliwa kuwa sampuli ya utafiti. Wazungumzaji wa lugha yoyote wako katika makundi tofautitofauti na hujitambulisha kwa makundi yao kiumri. Uteuzi wa sampuli kama unavyoelezwa na Bryman (2004) ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Hivyo kwa kufanya hivi mtafiti alitumia jumla ya wahojiwa 100 waliotoa data katika utafiti huu ambapo wahojiwa waliteuliwa kwa kutumia kigezo cha jinsia. Hapa wahojiwa wa kike 50 na wa kiume 50. Aidha hadhira pia itazingatia kigezo cha jinsia ambapo kutakuwa na walimu ya kike 5 na walimu wa kiume 5. Wanafunzi wa fasihi 40 wa kiume na wa kike 40.

Kigezo cha jinsi kimezingatiwa kwa sababu kuna matumizi tofauti ya lugha baina ya jinsi mbili na kwamba kuna msamiati maalumu unaotumika katika mazungumzo na mawasiliano kwa ujumla yanayorejelea jinsi moja tu. Kombo na Tromp (2006) wanaielezea mbinu hii kuwa ni mbinu ambayo hutumia watu ambao ni hadhira tekwa, yaani watu ambao mtafiti anakutana nao bila kutarajia. Katika mbinu hii wahojiwa huwa ni wale watu ambao hutokea wakiwa wanapita au wanaonesha kupendezwa na utafiti husika. Sababu ya kuteua mbinu hii ni kwamba, inaweza isiwe rahisi kupata wahojiwa ambao walikuwa tayari kutoa data hasa katika maeneo ambayo hakuna mwamko wa kielimu. Hivyo basi, mtafiti alitumia mbinu hii kushirikisha hadhira ambayo aliokutana nao uwandani kwa wakati na muktadha huo.

Hivyo basi, kutokana na sampuli hiyo, kulikuwa na wahojiwa wa kudumu takribani 80. Sababu ya kuteua kuwa na idadi hii ya wahojiwa ni kutaka kupata data toshelevu na hatimaye kufanya majumuisho ya matokeo kutokana na sampuli hiyo. Mchangunuo wa wahojiwa ni kama ifuatavyo:

**Jedwari 3.2. Mchanganuo wa Sampuli ya Utafiti**

| **WAHOJIWA** | **JINSI** | | **JUMLA** |
|---|---|---|---|
| | **Ke** | **Me** | |
| Walimu wa fasihi | 5 | 5 | 10 |
| Wanafunzi wa fasihi Chuo Kikuu cha Dar es salaam | 15 | 15 | 30 |
| Wanafunzi wa fasihi Jangwani | 15 | 15 | 30 |
| Wanafunzi wa fasihi Shaaban Robert | 15 | 15 | 30 |
| **JUMLA KUU** | | | 100 |

***Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti***

Idadi ya watafitiwa 100 iliteuliwa kwa sababu ilitosha kutoa matokeo yanayoaminika. Vilevile, mtafiti aliteua idadi hii ya watafitiwa kwa kuzingatia muda

alionao wa kukamilisha utafiti huu kwa wakati. Aidha, mtafiti alizingatia kigezo cha umri katika kuwapata watafitiwa kutoka kila taasisi ili aweze kuchunguza kama makundi ya wafanafasihi kiumri yana mtazamo, maoni na mwelekeo tofauti kuhusu matumizi ya tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert.

## 3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data

Mbinu za ukusanyaji data ni njia anazochagua mtafiti kuzitumia kukusanya data kwa ajili ya utafiti wake (Kothari, 1990:7). Dawson (2002:14) anafasili mbinu za utafiti kuwa ni zana au njia zinazotumiwa na mtafiti katika ukusanyanji wa data.Mtafiti alichunguza matumizi ya tamathali za semi za Kiswahili kama zilivyojitokeza katika *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, *Hati* na *Pambo la Lugha* kwa kutumia mbinu mchanganyiko za ukusanyaji data. Katika kukusanya data za utafiti huu, mbinu nne za ukusanyaji data zilihusishwa ambazo ni: mbinu ya usaili, hojaji, mbinu ya majadiliano (mahojiano) na maktabani.

Lengo la kutumia mbinu hizi mchanganyiko lilikuwa kukamilishana kwa data ili kupata matokeo ya kuaminika. Mbinu hizi zilimsaidia mtafiti katika kufikia malengo ya utafiti wake. Mbinu zote zilitumika kwa kutegemeana na kukamilishana ili kupata data toshelevu.

### 3.6.1 Usaili

Usaili ni mbinu ya majibizano ya ana kwa ana au ya simu, kidijitali/barua pepe kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa kuhusu suala fulani linalochunguzwa (Kombo na Tromp, 2006:104; Mligo, 2012; Mlowezi, 2012).

Mbinu hii inahusisha uwasilishaji wa maswali kwa watu wanaojibu maswali na ambao watajibu kwa mdomo kwa wakati huo huo. Kulingana na maoni ya Kothari (1990) mbinu hii inaruhusu unyumbukaji katika mchakato wa kuuliza maswali, inamruhusu mtafiti kuuliza maswali ya ziada. Husaidia kugundua mahusiano magumu katika mahusiano ya kijamii na itamsaidia kuwa ana kwa ana na watoa hababari au data za utafiti. Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano maalumu ambapo wasailiwa waliuilizwa maswali ya msingi ya aina moja na yaliyokuwa katika mpangilio ulio sawa. Mtafiti aliandaa maswali yaliyolenga kukusanya taarifa za aina moja kwa kila kundi la watafitiwa. Mbinu hii ni nzuri kwa sababu watafitiwa watakuwa na uwezo wa kujibu maswali sawa na hii iliongeza ulinganishi katika kujibu maswali. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliweza kukusanya data ambazo zililenga kukidhi malengo mahsusi ya utafiti huu. Hivyo, katika utafiti huu, usaili ulitumika ili kupata data zinazohusiana na malengo mahsusi ya utafiti huu.

Kuna aina tatu za usaili ambazo ni usaili huru, usaili funge na usaili nusufunge. usaili huru hutumia maswali yanayomtaka mtafitiwa kutoa taarifa za kina kadiri anavyoelewa yeye mwenyewe. Usaili wa aina hii ulimsaidia mtafiti kukusanya taarifa nyingi zaidi na hata ambazo hazikuweza kupatikana kwa njia ya hojaji. Kwa kutumia usaili huru, mtafiti aliweza kubadili uelekeo wa namna ya kuuliza maswali ili majibu yalingane na malengo ya utafiti wake.

Kwa mujibu wa Walliman (2011:99), usaili funge ni maswali yaliyotayarishwa na mtafiti kabla ya mtafitiwa kuulizwa na kujibu. Majibu ya maswali hayo huandikwa

au kurekodiwa na mtafiti. Usaili funge huhitajia majibu mafupi ya kuchagua jibu sahihi au kujaza jibu moja fupi. Usaili funge husaidia kulinganisha majibu ya mahojiano mbalimbali yaliyofanyika na hutumia muda mfupi kupata taarifa zinazohitajika na mtafiti. Usaili nusufunge ni mbinu ambayo huacha nafasi kwa maswali mengine ya kujieleza, yaani maswali ambayo yako nje ya yale yaliyoandikwa. Usaili wa aina hii yalimsaidia mtafiti kupata taarifa ambazo hazikufafanuliwa vizuri na mtafitiwa kwa kutumia maswali elekezi kulingana na mahitaji ya utafiti. Vilevile, usaili nusufunge yalimsaidia mtafiti kupata taarifa za ziada kulingana na malengo ya utafiti wake.

Utafiti huu wa kuchunguza matumizi ya tamathali za semi na nafasi yake katika kusawiri ujinsia na nafasi ya mwanamke katika jamii ulitumia aina mbili za usaili, yaani usaili huru na usaili nusufunge. Mtafiti alikuwa na maswali ya kumwongoza kuwahoji watafitiwa. Uteuzi wa mbinu hii ulizingatia ukweli kwamba mbinu hii husaidia kupata taarifa za ziada ambazo si rahisi kuzipata kwa kutumia mbinu nyingine za ukusanyaji data. Mbinu hii pia ilisaidia kupata taarifa mbalimbali za watafitiwa kuhusu mtazamo wao kuhusu matumizi ya tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert na mchango wake katika kusawiri ujinsia katika ushairi wa Kiswahili na kuonesha nafasi ya mwanamke katika jamii hususan wakazi wa jiji la Dar es Salaam. Vilevile, mbinu ya usaili ilitumika kulinganisha na kujaziliza data ambazo zilipatikana kwa kutumia njia ya hojaji.

### 3.6.2 Dodoso

Hojaji ni orodha ya maswali na maelekezo yaliyoandaliwa na mtafiti ili mtafitiwa

aweze kujibu maswali hayo. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003), hojaji huandaliwa kwa lengo la kukusanya taarifa muhimu kutoka kwa watafitiwa. Aidha, Kothari (1990:100) anasistiza kuwa hojaji iliyoandaliwa vizuri ni ile ambayo maswali yake yamepangwa katika mtiririko maalumu ili mtafitiwa aweze kujibu maswali hayo kwa urahisi. Mtafiti alichagua njia ya hojaji kwa sababu njia hii huweka ulinganifu wa majibu yanayotolewa na watafitiwa wote. Njia hii ilirahisisha ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa watafitiwa wengi kwa muda mfupi. Vilevile, njia ya hojaji ilirahisisha kazi ya kufanya majumuisho ya majibu yaliyopatikana.

Mtafiti alitumia hojaji yenye maswali kumi na moja yaliyogawanywa katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ilihusu taarifa binafsi za mtafitiwa. Taarifa binafsi za mtafitiwa zilitumika katika uchanganuzi na ufafanuzi wa data. Sehemu ya pili ilihusu matumiazi ya tamathali za semi katika ushairi wa Shaaban Robert katika kazi zake za *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini, utenzi wa Hati* na *Pambo la Lugha*. Lengo kuu lilikuwa kupata taarifa zinazohusu tamathali za semi, aina za tamathali za semi, udhihirikaji wa ujinsia katika mashairi hayo na jinsi tamatahli za semi zinavyomchora mwanamke na kuonesha nafasi yake katika jamii. Hojaji zote ziliandikwa kwa Kiswahili na ziligawiwa kwa watafitiwa walioteuliwa kwa ajili ya ukusanyaji data.

### 3.6.3 Mbinu ya Maktabani

Mbinu hii ni mbinu kuu iliyotumika katika utafiti huu. Katika utafiti huu, mbinu hii ilitumika katika katika kukusanya data zilizopo katika vitabu vya mashairi ambavyo

viliteuliwa katika utafiti huu. mtafiti alisoma na kuchambua vitabu vya mashairi vya *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini, Hati na Pambo la Lugha* ili kubainisha tamtahali za semi zilizotumika katika mashairi hayo. Kwa kutumia mbinu hii ilikuwa rahisi kubainisha tamatahli za semi na maana zake katika muktadha wa utumizi. Mbinu zingine kama mbinu ya usaili, hojaji na majadiliano zilitumika kama mbinu jazilizi za mbinu hii. na

### 3.6.4 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi

Katika utafiti huu, mbinu ya majadiliano ya vikundi yalitumika kukusanya data za utafiti huu. Mtafiti alitumia majadiliano ya vikundi kwa kuwakusanya wanafunzi wa fasihi wanaosoma kozi ya ushairi. Makundi hayo yalihusisha watu saba hadi nane ambao waliwekwa katika chumba kwa muda tofauti. Kwa kila kundi mtafiti alifanya majadiliano ya dakika arobaini na tano hadi saa moja. Katika majadiliano hayo mtafiti alilenga kupata maoni, mtazamo na mielekeo juu ya ujinsia katika mashairi ya shaaban Robert na namna tamathali za usemi zilivyotumika katika kusawiri suala la ujinsia na nafasi ya mwanamke katika mashairi ya *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini, Hati na Pambo la Lugha* .

## 3.7 Uchambuzi wa Data

Data zilizokusanywa katika utafiti huu kwa kutumia mbinu za mahojiano, hojaji, na maktabani zilichanganuliwa na kufafanuliwa kimaelezo na kitakwimu. Njia ya kimaelezo ilitumika kufafanua aina ya tamathali za semi, ujinsia katika tamathali na usawiri wa nafasi ya mwanamke katika tamathali za semi kwa kutumia mashairi ya Shaaban Robert ambayo yanapatikana katika vitabu teule vya utafiti huu. Njia hii pia

ilitumika kuelezea sababu za matumizi ya tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert. Matokeo yaliyopatikana, baadhi yamewasilishwa kwa njia ya kimaelezo na kiulinganishi kati ya wanafasihi walimu na wanafunzi na watafiti wa fasihi ya Kiswahili hususan ushairi wa Kiswahili.

Utafiti huu ni utafiti ubora. Zipo mbinu mbalimbali zinazotumika kuchambua data za utafiti wa aina hii. Pamoja na mbinu zilizopendekezwa hapo juu, data ya utafiti huu ilichambuliwa pia kwa kutumia mbinu mbili, yaani *uchambuzi maudhui* na *uchambuzi linganishi*. Uchambuzi maudhui inaelezewa na Kombo na Tromp (2006) kuwa ni mbinu ya uchambuzi ambayo huziweka mada kulingana na jinsi zinavyofanana na kuhusiana. Dhana kuu au dhamira kuu hubainishwa na kuwekwa pamoja. Sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba ilisaidia kuweka maana zote zinazohusiana kutokana na data za dodoso na usaili ili kutoa mawazo ya jumla kulingana na malengo ya utafiti huu.

Kwa upande mwingine, uchambuzi linganishi hutumika kulinganisha data kutoka kwa watu tofauti. Katika kuchambua data mtafiti alifanya yafuatayo:

i) Kubainisha tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert.

ii) Kuchambua jinsi tamathali hizo zinavyosawiri ujinsia na maana zilizobebwa na tamathali hizo.

iii) Kuchambua na kuwasilisha data zilizopatikana katika hojaji, dodoso na usaili kwa kutumia chati na namba.

iv) Kubainisha na kuelezea kutofautiana au kufanana kwa wasanii wa kike na wale wa kiume katika uteuzi wa tamathali za semi kuashiria ujinsia.

## 3.8 Zana za Kukusanyia Data

Utafiti huu ulitumia zana zifuatazo za ukusanyaji data;

### 3.8.1 Matini

Matini tunazozizungumzia hapa ni matini andishi za mashairi ya Shaaban Robert ambayo mtafiti aliyakusanya ili kupata data anazokusudia hususan *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* na *Pambo la Lugha*.

### 3.8.2 Kompyuta na Notibuku

Hapa tunapozungumzia kompyuta tunarejelea kompyuta ya mkononi yenye programu ya kinasa sauti na notibuku za kuandikia kumbukumbu. Zana hizi ni muhimu sana katika kukusanyia na kuhifadhi data za awali kipindi cha mazungumzo. Katika utafiti huu zilitumika kukusanya na kurekodi data za dhana za mashairi, masimulizi ya maana za kiishara, dhima zake na umuhimu wake.

### 3.8.3 Kinasa Sauti

Kinasa sauti Kilitumika kurekodi sauti wakati wa mazungumzo baina ya mtafiti, hadhira na wasanii. Kwa kufanya hivi mtafiti aliweza kupata data zinazohusiana na mwelekeo wa jamii kuhusu suala la jinsia katika mashairi ya Shaaban Robert na sababu za uteuzi wa maneno katika mashairi hayo.

### 3.8.4 Kamera ya Kawaida

Kamera ilitumika kuchukua matukio katika muktadha na mazingira ya utafiti. Pia kamera ya kawaida ilitumika kuchukua picha mbalimbali wakati wa utafiti mtafiti alipokuwa uwandani na matukio mbalimbali katika eneo la utafiti.

### 3.8.5 Dodoso/ Hojaji

Hojaji tatu za maandishi ziliandaliwa kwa ajili ya wahojiwa. Hojaji ya kwanza ililenga kuchunguza uelewa wa maana za maneno kwa hadhira. Hapa mtafiti aliorodhesha baadhi ya maneno yanayotumika katika masahiri ya Shaaban Robert na kuwapatia wahojiwa ili watoe maana ya dhana hizo. Hojaji ya pili ililenga kuchunguza ujinsia na jinsi usawiri wake katika mashairi ya Shaaban Robert na hojaji ya tatu ililenga kuchunguza maana na mwelekeo wa jamii kuhusu suala la jinsia na jinsi linavyojitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert. Hojaji hizi zilitolewa kwa hadhira na wasanii.

### 3.8.6 Usaili

Kama ilivyokwisha elezwa hapo awali, maswali kwa ajili ya usaili yaliandaliwa kwa ajili ya wasanii na hadhira. Hapa kulikuwa na maswali ya usaili ambayo ni rasmi ambayo mtafiti aliyaandaa kabla ya kwenda uwandani na maswali hayo yaliulizwa kwa kila mhojiwa. Aidha, mtafiti aliuliza maswali ya ziada ambayo yaliibuka kulingana na muktadha.

## 3.9 Hitimisho

Sura hii imeajdili juu ya muundo na mbinu zilizotumika katika utafiti huu. Imeelezwa kuwa utafiti huu ulifanyika katika jiji la dar es salaam katika maeneo ya chuo kikuu cha dar es salaam walengwa wakiwa ni walimu na wanafunzi wa fasihi hususan ushairi wa kiswahili. Eneo lingine ni shule ya sekondari ya Shaaban Robert na Jangwani walengwa wakiwa ni wanafunzi wa fasihi. Aidha imeelezwa kwamba sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu tatu ambazo ni mbinu ya uteuzi

wa madhumuni maalumu, mbinu ya uteuzi nasibu tabakishi na mbinu ya usampulishaji wa kimfumo. Katika sura hii imeelezwa kuwa data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu nne ambazo ni mbinu ya maktabani, usaili, hojaji na majadiliano ya vikundi. Katika sura hii imeelezwa kuwa, data za utafiti huu zilichambuliwa, kujadiliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mikabala ya kimaelezo na kitakwimu ambapo taarifa za kiisimu zimewasilishwa kitakwimu katika majedwali na mkabala wa kimaelezo umetumia kufafanua tamathali za semi, usawiri wa ujinsia kwa kutumia tamathali za semi zilizomo katika mashairi ya Shaaban Robert kutoka katika vitabu vilivyoteuliwa na mtafiti. Vilevile, sababu za matumizi ya tamathali za semi katika ushairi wa Shaaban Robert zimeelezwa kwa kutumia njia ya kimaelezo.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data. Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa jinsia katika lugha ya mashairi ya Shaaban Robert katika kazi zake za fasihi za *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* ili kuonyesha jinsi gani lugha inatumika kujadili suala la ujinsia. Uchambuzi wetu ulijielekeza katika kuchunguza tamathali za semi zinazojitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert ndani ya vitabu teule na jinsi zinavyosawiri mahusiano baina ya wanawake na wanaume. Pia katika uchambuzi wetu, tumefafanua pia nafasi ya mwanamke katika jamii kama inavyojitokeza katika kazi teule za Shaaban Robert. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni: sehemu ya kwanza ni tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert, sehemu ya pili ni tamathali za semi na usawiri wa jinsia, sehemu ya tatu ni tamathali za semi na nafasi ya mwanamke na sehemu ya nne ni hitimisho.

## 4.2 Tamathali za Semi katika mashairi ya Shaaan Robert

Moja ya malengo mahususi ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha tamathali za usemi ambazo zinajitokeza katika mashairi ya *Pambo la Lugha*, *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Utafiti huu uligundua kuwa msanii ametumia tamathali za semi kwa kiasi kikubwa katika mashairi yake kama mbinu ya kisanii katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Lengo kuu la kutumia mbinu hii ni kuifanya kazi ya fasihi iwe yenye kugusa hisi na hivyo kuathiri mwitiko kwa njia chanya na kwa hivyo

kuipambanua kazi ya fasihi na kazi nyingine ambazo si za kifasihi (taz. Mulokozi na Kahigi,1979). Miongoni mwa tamathali za semi zilizojidhihirisha katika utafiti wetu ni: sitiari, tasifida, tashihisi na takriri.

**Jedwari 4.1: Idadi ya Tamthali za Semi Kiulinganshi**

| Aina ya Tamathali ya Usemi | Jumla |
|---|---|
| Sitiari | 57 |
| Tasifida | 61 |
| Tashibiha | 62 |
| Tashihisi | 72 |
| Takriri | 42 |
| **Wastani wa tamathali katika mashairi** | **299** |

***Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti***

Jedwali namba 1 linaonesha kuwa sitiari imejitokeza mara 57, tafsida mara 61, tashihisi mara 72, tashibiha mara 62 na takriri mara 42 . Matokeo haya yanadhihirisha matumizi ya tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert. Sehemu ifuatayo inazijadili tamathali za semi zilizojitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert kwa mifano kutoka katika muktadha wa mashairi husika.

### 4.1.1 Sitiari

Sitiari ni aina ya tamathali ya usemi ambayo hulinganisha vitu viwili bila kutumia vifananisho (taz. Akivaga na wenzake, 1982; Jilala, 2008; Omari, 2009). Sitiari ni moja ya tamathali za semi ambayo ilijidhihirisha katika mashairi ya shaaban Robert yaliyochunguzwa katika utafiti huu. Kwa mfano katika shairi la Amina Shaaban Robert anamfananisha marehemu mke wake (AMINA) na ua pale anaposema:

*AMINA umejitenga, kufa umetangulia,*

*Kama ua umefunga, baada ya kuchanua,*

*Nakuombea mwanga, peponi kukubaliwa,*

*Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.*

***Chazo: Shaaban Robert Katika Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini Uk. 4***

Katika mfano huo mtunzi ametumia neno ‘ua’ kama sitiari ambapo anamlinganisha mkewe Amina na ua. Sifa za ‘ua’ambazo ni uzuri, harufu nzuri na kuvutia zinahamishiwa kwa Amina. Aidha sifa kuu ya ‘ua’ambayo ni kuchanua, kupendeza na kuvutia na hatimaye hufunga, kunyauka na kufa kisha kudondoka chini zimefananishwa na uzuri wa Amina ambaye amefikwa na mauti. Mtunzi anajaribu kutumika tashibiha kuonesha uzuri wa Amina kwa kutumia neno moja kuelezea sifa nyingi alizokuwa nazo Amina.

Mfano mwingine wa sitiari ni katika utenzi wa *Hati* ambapo msanii anasema*:*

*Upishi mwema kujua,*

*Na mume kumridhia,*

*Neno analokwambia,*

*Kwako itakuwa taa.*

***Chanzo: Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk.6-20 na Pambo la Lugha Uk. 36-49.***

Katika mfano huo neno ‘taa’ limetumika kama sitiari kuonesha kuwa maneno ya mume ndiyo mwongozo wa mwanamke. Sifa za ‘taa’ kutoa mwanga palipo na giza

na kuangaza zimehamishiwa katika maneno ya mwanaume ambaye anayatoa kwa mkewe. Mifano mingine ya sitiari ni kama vile;

*Tumbo la rutuba,*
*Umepewa kama huba,*
*Uzae mama na baba,*
*Kustawisha dunia.*

*Tumbo hili ni dhahabu,*
*Huzaa wenye thawabu,*
*Na wengine wa ajabu,*
*Hupata kuzaliwa.*
*(Taz. Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk.16 katika ubeti wa 74).*

Katika mifano hiyo tunaona kuwa tumbo lenye rutuba ni sitiari ambayo imetumika kurejelea tumbo la mwanamke. Tumbo la mwanamke linafananishwa na ardhi yenye rutuba ambayo huzaa mazao mengi. Kwa uhalisia mwanamke hawezi kuwa na rutuba bali kinachokuwa na rutuba ni ardhi hivyo katika muktadha huu tumbo lenye ‘rutuba’ limetumika kisitiari kumrejelea mwanamke na uzazi. Aidha katika ubeti wa msanii amelifananisha tumbo la mwanamke na ‘dhahabu’. Kiuhalisia tumbo haliwezi kuwa dhahabu bali sifa za ‘dhahabu’ zinahamishiwa kwenye tumbo. Dhahabu ni kito cha thamani, chenye mvuto, kung’aa na kuvutia (taz. Jilala, 2008). Katika muktadha huu sitiari dhahabu imetumika kuonesha thamani ya tumbo la mwanamke ambalo huzaa watoto wa aina tofauti tofauti na kuongeza jamii.

Mifano mingine ya sitiari iliyojitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert ni pamoja na:

i) Hati iwe zumaridi (Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk. wa 7 ubeti wa 9)

ii) Hati hii ni lulu (Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk. wa 7 ubeti wa 10)

iii) Nakupa (hati) iwe hereni (Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk. wa 9 ubeti wa 26)

iv) Hati hii ni nuru (Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk. wa 10 ubeti wa 29)

Katika mifumo hiyo maneno zumaridi, lulu, hereni na nuru yametumika kisitiari kurejelea hali ambayo imeandikwa kwa ajili ya mwanamke. Hapa hati inafananishwa na ubora, thaamni na mwongozo katika maisha.

### 4.1.2 Tasifida

Hii ni aina ya tamathali ya usemi ambapo neno, kirai, kishazi au sentensi ambayo maana yake haitakiwi na haipendezi kutajwa hadharani; badala yake huondolewa na kuwekwa badala yake neno, kirai, kishazi au sentensi nyingine inayotumika kuelezea dhana ile ile (Senkoro, 2012; Wamitila, 2003). Wakati mwingine tasifida hujulikana kama usafidi. Tasifida zinakusudia kuficha maana halisi, kuburudisha, kupamba mazungumzo na kuwatenga watu wengine wasiohusika katika mazungumzo. Vile vile, tasifida hutumika kulinda maadili na heshima ya jamii, kuwatambulisha wazungumzaji wa lugha kimakundi na hata wakatimwingine kupotosha ujumbe wakati wa mawasiliano. Hivyo, tasifida ni ala ya utamaduni wa wazungumzaji wa

lugha kupitia lugha wanayozungumza. Neno, kirai, kishazi au sentensi inapotumika kama tasifida hupoteza maana yake ya msingi na kuchukua maana ya ziada au maana husishi kitamathali. Tamathali za semi hutegemea na hutawaliwa kwa kiasi kikubwa na utamaduni wa wazungumzaji wa lugha. Tunapenda kusisitiza pia kwamba mara nyingi tasifida huonesha ustaarabu wa mzungumzaji au mhusiaka wa tendo la mawasiliano.

Katika mashairi ya Shaaban Robert tamathali hii ya usemi imejitokeza kwa mfano katika ubeti wa 33 ukurasa wa 25 katika Utenzi wa Hati (*Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini*), msanii ametumia tasifida '*Neno analokwambia*' badala ya kutaja mathalani hata kama mumeo atataka kufanya mapenzi nawe usimkatalie. Tazama ubeti hapa chini:

*Upishi mwema kujua,*
*Na mume kumridhia,*
*Neno analokwambia,*
*Kwako itakuwa taa.*

***Chanzo: Utenzi wa Hati (Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini)***

Ubeti huu hasa mstari wa pili na wa tatu tafsida imetumika kama mbinu ya kupunguza makali ya maneno ya ujumbe mpana ambao baba alikusudia kumpatia binti yake. Baba hangeweza kusema waziwazi kuwa ni lazima kumkubalia mumewe kufanya mapenzi na kwamba ni muhimu kuonesha ufundi wa kufanya tendo la ndoa na mume wake. Hii inaonesha uwezo wa tamathali za usemi katika kuonesha pia umbali wa kijamii na kijinsia kiasi kwamba tunaona jinsi baba asivyoweza

kumweleza binti yake baadhi ya mambo kwa kutumia lugha ya kawaida.

### 4.1.3 Tashihisi

Tashihisi huvipa vitu uhai ambavyo kwa asili yake vitu hivyo havina uhai. Uhaishaji unaofanywa na tashihisi huvipa vitu visivyo hai uwezo wa kufikiri na kutenda kama binadamu (Senkoro, 2012; Wamitila, 2003). Mbinu hii imetumiwa pia na Shaaban Robert katika kuimarisha mtindo na fani ya mashairi yake katika vitabu teule. Mfano wa tashihisi katika mashairi ya Shaaban Robert ni:

i) Dunia ina aibu (Maisha yangu na Baada yaMiaka Hamsini uk. 7 ubeti wa 6)

ii) Itaongeza (Hati) uoni (Maisha yangu na Baada yaMiaka Hamsini uk. 9 ubeti wa 25)

iii) Hati iweke moyoni (Maisha yangu na Baada yaMiaka Hamsini uk. 9 ubeti wa 26) na kadhalika.

Katika data hizi tunaona kuwa dunia imepewa uwezo wa kuwa na aibu, hati kuongeza uwezo wa kuona na hati kupata uwezo wa kuingia moyoni. Katika uhalisia sifa za kuona, kutenda na kuhisi ni za kibinadamu. Dunia haina uwezo wa kuona aibu na pia hati haina uwezo wa kutenda jambo. Uchunguzi wa kina katika utafiti umebaini pia kuwa tashihisi kama hizo hapo juu zilitumika kusawiri ujinsia hasa hususan tabia na mwenendo anaopaswa kuwa nao mwanamke.

### 4.1.4 Tashibiha

Tamathali hii inatofautiana kidogo sana na sitiari. Tofauti iliyopo baina ya aina hizi za tamathali ni kwamba wakati ambapo sitiari inalinganisha vitu bila kutumia

viunganishi, tashibiha hulinganisha vitu kwa kutumia viunganishi (Senkoro, 2012). Mifano ya tashibiha zilizojitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert ni pamoja na:

*PANYA*

*Paka alitoka, uwanjani kujigamba,*

*Kuwa ana mamlaka, na nguvu kama simba,*

*Simba alicheka, akasema "Ewe pumba,*

*Hulingani na paka, wataradhia usimba.*

***(Pambo la Lugha uk. 1)***

Mfano huo unaonyesha matumizi ya tashibiha. Kwa mfano panya analinganisha nguvu zake na nguvu za simba kwa kutumia tashibiha 'kama'. Aidha, katika shairi la Amina msanii analinganisha kifo cha Amina na tabia ya ua kufunga baada ya kuchanua. Msanii anasema *'Amina umejitenga kufa umetangulia kama ua umefunga baada ya kuchanua'*.

### 4.1.5 Takriri

Takriri ni tamathali ya semi inayohusika na urudiaji wasilabi, neno, sentensi, wazo au aya nzima. Wataalamu wamebainisha aina mbalimbali za takriri kama vile takriri silabi, takriri neno, takriri sentensi, takriri ridhimu na takriri aya. Katika uchunguzi wake wa muziki wa kizazi kipya maarufu kama Bongo Fleva, Omari (2009) anabainisha kuwa katika muziki huo kuna matumizi ya takriri silabi, takriri sauti, takriri neno, takriri sentensi, takriri wazo na hata takriri mapigo kwa lengo la kuleta athari katika wazo au maana. Shaaban Robert katika shairi lake la *Amina*

linalopatikana katika *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* ametumia takriri wazo. Katika beti zote amezungumzia wasifu wa marehemu mke wake. Katika shairi hili kuna takriri mstari pia ambapo kituo ‘Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.’ Dhima ya takriri hii ni kusisitiza umuhimu na nafasi ya mwanamke katika jamii. Vilevile, katika *Utenzi wa Hati* kuna takriri neno (tazama ubeti wa 99) katika *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* ukurasa wa 35 na katika Pambo la Lugha ukurasa wa 49 katika utenzi huo huo ambapo msanii amerudia neno *peke* kuunda neno *pekepeke*.

Katika sehemu hii tumechambua na kujadili juu ya tamathali za semi amabzo zinajitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert. Utafiti huu umegundua kuwa msanii anatumia tamathali za semi kama mbinu ya kisanii kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Tamathali za semi amabzo zimeonekana kutumiwa zaidi katika mashairi hayo ni sitiari, tashibiha, tashihisi, tafsida na takriri. Sehemu inayofuata inachambua na kujadili kwa kina juu ya tamathali za semi na usawiri wa jinsia.

## 4.3 Tamathali za Semi na Usawiri wa Ujinsia

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kuibua namna tamathali za usemi zinavyosawiri mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanaume. Ingawa katika sehemu iliyotangulia tumekuwa tukigusia hapa na pale namna tamathali za semi zinavyosawiri ujinsia katika mashairi ya Shaaban Robert, katika sehemu hii tunakusudia kujadili kwa kina tamathali za semi na ujinsia katika mashairi ya Shaaban Robert kutoka vitabu vyake vya *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Katika utafiti huu iligundulika kwamba tamathali za semi

zinatumika kusawiri suala la ujinsia katika jamii. Wakati wa usaili asilimia 90 ya wahojiwa walipoulizwa endapo tamathali za semi zinatumika kusawiri suala la ujinsia walijibu ‘ndiyo’ wakati asilimia 10 tu ya wahojiwa walijibu hapana. Katika dodoso wahojiwa wote walijibu ndiyo ambao ni asilimia 100 ya wahojiwa. Matokeo haya yanathibitisha kuwa tamathali za semi katika mashairi ya Shaabn Robert yanasawiri suala la ujinsia katika jamii.

Kwa mujibu wa Knappert (1979: xiv), tendi simulizi nyingi za Kiafrika zilitungwa na watu maarufu waliojinaki kuwa wao binafsi au koo zao zilikuwa na uwezo katika medani mbalimbali za maisha kama vile uwindaji, kupigana mieleka na kupigana vita. Anaendelea kufafanua kuwa tendi nyingi ziliwasifia wanaume kuwa wana uwezo wa kufanya mambo mbalimbali na cha kushangaza ni kwamba hata washairi wanawake walipojitokeza walitunga mashairi yao yaliyoukweza mfumo dume katika jamii. Aidha, anachosisitiza Knappert (keshatajwa) kuhusiana na hali hii ni kwamba matumizi ya tamathali za semi ndiyo yaliyotimiza lengo hili la ushairi ambapo, sitiari zilitumiwa kumkweza mwanamme na kumdunisha mwanamke. Kwa hiyo, matumizi ya tamathali za semi katika kusawiri ujinsia yana historia ndefu.

Katika utafiti huu tulitumia mbinu ya hojaji, majadiliano ya vikundi na usaili ili kuchunguza namna tamathali za semi zinavyosawiri masuala ya kijinsia katika mashairi ya Shaaban Robert. Katika usaili ilielezwa kuwa tamathali za semi zinasawiri suala la ujinsia kwa kuonesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanamme katika jamii. Aidha matokeo haya hayakuwa tofauti na yale yaliyopatikana katika dodoso na majadiliano ya vikundi ambapo asilimia 90 ya

wahojiwa walieleza kuwa tamathali za semi katika mashairi teule yanasawiri suala la ujinsia.

Wahojiwa wakati wa majadiliano ya vikundi walitoa mifano ya sitiari kuwa zimetumiwa kusawiri suala la ujinsia. Tazama beti zifuatazo:

*PANYA*

*Paka alitoka, uwanajani kujigamba,*

*Kuwa ana mamlaka, na nguvu kama simba,*

*Simba alicheka, akasema "Ewe pumba,*

*Hulingani na paka, wataradhia usimba.*

***(Pambo la Lugha uk. 1)***

Wahojiwa walibainisha matumizi ya sitiari 'panya', 'simba', 'paka' na 'pumba' ambazo zimetumika kusawiri mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume. Kwa mfano, sitiari ya 'simba' kwa muda mrefu katika historia ya binadamu imekuwa ikitumika kumrejelea mwanamme shupavu anayeweza kukabiliana na janga lolote la kijamii kama vile vita au uvamizi wa aina yoyote unaoelekezwa katika jamii yake. Kinyume chake ni kwamba mwanamke amekuwa akihusishwa na viumbe duni ili kumchora kama kiumbe mwoga asiye na uwezo wa kukabiliana na hatari yoyote inayojitokeza katika mazingira yake.

Mwanamke amejengewa saikolojia hii kunakopigiwa chapuo na taasisi za kijamii kama ndoa, dini na kadhalika (Momanyi, 2003 na Senkoro, 2010). Kwa kutumia

sitiari msanii anaonyesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanamme kwa mfano ‘panya’ imetumika kisitiari kumrejelea mwanamke na ‘simba’ imetumika kisitiari kumrejelea mwanaume. Aidha nguvu na uwezo wa mwanamke na mwanamme zimetofautishwa kwa kutumika sitiari. Kwa mfano, katika shairi hili neno ‘pumba’ limetumika kisitiari kurejelea nguvu za mwanamke. Kwamba mwanamke ni dhaifu kama pumba ambazo haziwezi kuhimili mikiki, ni nyepesi na zinaweza kupeperushwa na upepo. Kwa kutumika sitiari hizi, Shaaban Robert ameonesha mahusiano yasiyowiana kifursa baina ya mwanamme na mwanamke. Mwanamme anaonekana ni mwenye nguvu, hodari na shupavu wakati mwanamke anaonekana ni dhaifu asiye na nguvu wala uwezo.

Aidha, thamani inayowekwa na Shaaban Robert juu ya mwanamke anavyohusiana na mwanamume ni thamani hasi. Hii ni kutokana na mbinu yake ya kisanaa ya kumnasibisha mwanamke na vitu duni kama mapambo ya mwilini au mimea inayoyazunguka mazingira. Mawazo haya hayatofautiani na mawazo ya Jilala (2010/2011) ambapo anaona kuwa vitu vya tahamani, mapambo, sifa za utoto, uzuri na utamu ni maneno yenye dhana hasi ya kumdhalilisha na kumdunisha mwanamke. Msanii huyu katika shairi lake la Amina anatumia tashibiha katika kuonesha mahusiano ya kijinsia baina ya wanawake na wanaume. Katika ubeti wa kwanza wa shairi hili anaeleza:

*AMINA*

*Amina umejitenga, kufa umetangulia,*

*Kama ua umefunga, baada ya kuchanu,*

*Nakuombea mwanga, peponi kukubaliwa,*

*Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.*

***(Pambo la Lugha uk. 4)***

Kitendo cha msanii huyu kumnasibisha mwanamke na 'kinashusha hadhi ya mwanamke kwa kiwango kikubwa. Jilala (2008 & 2010/2011) anaeleza kuwa matumizi ya maneno yenye dhana uzuri, thamani, utamu, mvuto na utoto kumrejelea mwanamke ni dhana zinazomdunisha mwanamke na kumfanya aonekane ni kiumbe dhaifu na tegemezi asiye na maamuzi binafsi ukilinganisha na sitiari ambazo humchora mwanaume kama jasiri, hodari, shupavu. Wakati wa majadiliano ya vikundi na wanafunzi wa fasihi mwaka wa tatu wanaochukua shahada ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam, utafiti huu uligundua kuwa matumizi ya sitiari 'simba' kumrejelea mwanaume hubeba dhana ya ujasiri, ushupavu na uhodari wakati sitiari 'ua' humchora mwanamke kama kiumbe dhaifu na tegemezi. Ilielezwa na wahojiwa kuwa, mwanamke asichukuliwe kama 'ua' au pambo lolote ndani ya nyumba kwani hata tafiti mabalimbali za kiuchumi zimeonesha kuwa mwanamke ndiye mzalishaji mkubwa katika uchumi na hivyo wanachangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa uchumi na pato la jamii au nchi yoyote. Aidha, huu ni ushahidi kuwa mbinu ya tamathali za semi inaweza kutumika kuyasawiri mahusiano ya aina yoyote baina ya wanawake na wanaume katika jamii.

Uchunguzi wa kina katika utafiti huu ulibaini kuwa tamathali nyingi zinazomrejelea mwanamke katika kusawiri ujinsia zinamdunisha mwanamke kwa kumchora kuwa

thamani yake inahusiana na vitu vya kawaida vinavyopatikaa katika mamzingira. Vitu hivyo ni kama vile pini, hereni, ua na akadhalika. Sitiari ‘ua’ kama ilivyotumika katika shairi la *AMINA* ubeti wa kwanza inasawiri ujinsia katika jamii za mfumo dume ambapo taasisi za kijamii kama siasa, uchumi na dini humtazama mwanamke kama chombo duni kwa sababu ananyimwa fursa ya kuzimiliki au kunufaika na taasisi hizo. Aidha, kwa upande mwingine sitiari ua inatumika kuonesha thamani ya mwanamke katika jamii hasa inapotumika kumrejelea mwanamke mrembo au mwamamke ambaye ni tumaini la jamii inayomzunguka.

Mahali pengine katika *Utenzi wa Hati* mwanamke anadhihirishwa kama kiumbe ambaye hatima ya maisha yake iko mikononi mwa mwanaume kiasi kwamba hatakiwi kumkatalia jambo lolote mumewe ingawa anahimizwa kukataa kama atatakiwa kufanya jambo ambalo liko nje ya utaratibu; suala linalozua mkanganyiko kwani vigezo au mambo yepi yasiyo halali hayajawekwa bayana na mshairi. Chunguza beti zifuatazo kutoka *Utenzi wa Hati:*

*Upishi mwema kujua,*
*Na mume kumridhia,*
*Neno analokwambia,*
*Kwako itakuwa taa.*

*Na mume msishindane,*
*Wala msinuniane,*
*Jitahidi mpatane,*
*Ndiyo maisha ya ndoa.*

*Fanya kila hali,*

*La mume kulikubali,*

*Ila lisilo halali,*

*Kukataa si hatia.*

***Chanzo: Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk.6-20 na Pambo la Lugha uk. 36-49.***

Aidha, utafiti huu uligundua kuwa sitiari hutumika kurejelea majukumu ya mwanamke katika jamii. Mwanamke anafananishwa na ardhi yenye rutuba yenye uwezo wa kuzaa mazao ya aina na ubora wa aina mbalimbali ambapo msanii anasema yeye (Bintiye) amepewa tumbo la rutuba ili azae watoto na kuukuza na kuendeleza ukoo wake. Kuhusu hili msanii anasema:

*Tumbo la rutuba,*

*Umepewa kama huba,*

*Uzae mama na baba,*

*Kustawisha dunia.*

*Tumbo hili ni dhahabu,*

*Huzaa wenye thawabu,*

*Na wengine wa ajabu,*

*Hupata kuzaliwa.*

*(Taz. Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk.16 katika ubeti wa 74).*

Utafiti umeonesha kuwa mwanamke anabebeshwa sifa njema na mbaya kuhusiana na watoto wanaozaliwa kama inavyojidhihirisha katika ubeti wa 73 na 74 (Utenzi wa

Hati). Kuna matukio mengi katika jamii zetu kwa wanawake kulaumiwa kuwa wao ni chanzo cha watoto kuzaliwa na ulemavu na wengine huwalaumu wanawake kuwa tabia mbaya za watoto ni matunda ya namna walivyolelewa na mama zao. Mtazamo huu ulielezwa pia na baadhi ya watafiti kuwa mwanamke huonekana kuwa ni chanzo cha matatizo na magonjwa katika jamii (taz. Mutembei, 2002; Mtazamo huu unawafanya washairi kama Shaaban Robert kuusawiri ujinsia katika jamii zetu kwa kumdunisha mwanamke.

Mifano mingine ya sitiari iliyojitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert inasawiri suala la ujinsia katika jamii. Kwa mfano :

i) Hati iwe zumaridi (Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk. wa 7 ubeti wa 9)

ii) Hati hii ni lulu (Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk. wa 7 ubeti wa 10)

iii) Nakupa (hati) iwe hereni (Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk. wa 9 ubeti wa 26)

iv) Hati hii ni nuru (Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk. wa 10 ubeti wa 29)

Sitiari hizo hapo juu zinasawiri mfumo dume kuhusu ujinsia katika jamii nyingi ambapo mwanamke anachukuliwa kuwa vitu vinavyomfaa ni vile vilivyo duni kama mapambo ya mwili wake na nguo tu. Tamathali hizi zinasawiri mfumo dume katika jamii nyingi ambapo mwanamke anapambwa kwa vitu kama vile hereni. Vitu hivi vimetumiwa na msanii kuonesha ujinsia kuwa kuna vitu ambavyo vina matumizi na

manufaa kwa wanawake au wanaume tu. Vitu hivi vimetumika hapa kuhimiza mwanamke kupokea maonyo ya kimila na desturi yaliyo katika mfumo wa wosia kwa kulinganisha wosia na vitu vinavyothaminiwa na wanawake kama vile hereni, zumaridi, lulu na kadhalika. Vitu hivi vimetumika kusawiri mahusiano tofauti ya wmanamke na mwanaume. Wakati mwingine wanawake wamefananishwa na vitu hivyo kama asemavyo Shaaban Robert katika Utenzi wa Hati katika ukurasa wa 15 wa diwani ya Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini ubeti wa 64 na Pambo la Lugha ukurasa wa 40 katika ubeti wa 64 vile vile:

*Mke ni nguo nyeupe,*
*Doa katika utepe,*
*Jihadhari usiipe,*
*Haihimili madoa.*

Katika mistari ya shairi hilo msanii anatumia sitiari ‘nguo nyeupe’, ‘doa’ kumrejelea mwanamke. Kutokana na data na mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa, mtafiti alibaini kwamba jamii zenye mfumo dume zinachukulia kuwa makosa ya kijamii yanaweza kufanywa na wanaume tu. Kosa lile lile likifanywa na mwanamke huchukuliwa kwa picha tofauti katika jamii. Kwa hiyo, mwanamke anategemewa kufanya matendo mema tu na ikitokea akafanya kosa hata kama ni kwa bahati mbaya jamii humchukulia kuwa hafai hata kuolewa. Ikitokea akaolewa mume wake huchukuliwa na jamii kuwa amepata hasara kubwa kwa kuungana na mtu ambaye ana dosari katika jamii. Matokeo haya hayapo tofauti na watafiti wengine ambao waligundua kuwa mwanamke katika jamii nyingi za kiafrika zenye mfumo dume humuona mwanamke kama chanzo cha matatizo na hata magonjwa kama vile

UKIMWI (taz. Kisekka, 1990; Schiapper, 1991; Mutembei, 2009; Jilala, 2008 & 2010/2011).

Kutokana na hali hii ya kusawiriwa kwa mwanamke kama kiumbe duni na hivyo kuonesha mahusiano hasi baina ya mwanamke na mwanamme, baadhi ya wanawake walianza kutunga mashairi yaliyolenga kufuta mtazamo potofu juu ya wanawake kwa lengo la kuinua hadhi na heshima yao katika jamii. Hata hivyo, wanawake waliotunga mashairi baadhi yao waligeuka kuwa vibaraka wa mfumo dume kwa kushangilia na kuunga mkono mfumo huo uliokuwa unamkandamiza mwamnamke na kumkosesha heshima yake kwa muda mrefu. Mfano mzuri ni shairi la Fatma binti Athman na wimbo wa Siti binti Saad. Washairi wanawake hawakufanya hivyo kwa bahati mbaya bali kilichotokea ni kwamba hali ya kimahusiano baina ya mwanamme na mwanamke iko jinsi ilivyo toka kuumbwa kwa ulimwengu. Kwa mujibu wa Cornwall (1994:20), mamalaka ya kimfumo dume yanahusiana sana na uimarishwaji utawala na ukiritimba wa wanaume dhidi ya wanawake kiasi kwamba mahusiano baina ya wanaume na wanawake yanachukuliwa na jamii kama tukio la asili. Kuhusu madai ya mwanazuoni huyu tunasisitiza kuwa mfumo huu wa mtiririko wa utawala na mamlaka wanawake hawatabaki kuwa watawaliwa wakati wote. Maana yake ni kwamba wakati wowote katika utamaduni fulani wa jamii jinsia zote mbili, yaani wanawake na wanaume wataunga mkono utawala unaoegemea mfumo dume na matokeo yake ni kwamba kundi linalotawala litahakikisha kwamba makundi yote yanayotawaliwa yanakubali na kufuata namna mambo yalivyo na kukubali kuishi kwa kufuata kanuni na taratibu kama zilivyowekwa na kundi linaloshika utawala au dola katika jamii.

Aidha, Shaaban Robert katika Pambo la Lugha anaonesha umuhimu na mchango wa mwanamke kijamii. Katika shairi la PEKE anaonesha kuwa mwanamume hajitoshelezi na kwamba nafasi ya mwanamke ni muhimu katika ukamilifu wa maisha ya mwanamume ndio maana mtunzi anaeleza kuwa:

*Siwezi kuishi peke, peke ni utelezi,*

*Naomba dua ifike, apokee Mwenyezi,*

*Ishuke baraka yake, akuvike wokozi,*

*Peke ina makeke, kilio na majonzi.*

***Chanzo: Pambo la Lugha uk.2***

Katika shairi hili msanii ametumia sitiari utelezi kurejelea ugumu wa kuishi peke bila mke. Hapa msanii anaonesha ni jinsi gani ilivyo vigumu na matatizo makubwa kuishi bila mke. Utelezi huweza kumuangusha mtu chini akaumia au kufa. Hivyo basi, hatari ya utelezi inahamishiwa katika hatari ya mwanamme kuishi bila mwanamke.

Weedon (1997) anafasili mamlaka kwa kueleza kuwa ni mahusiano kiutawala, na nguvu ambazo ni badilifu baina ya makundi yanayohusika katika jamii yenye mfumo fulani wa kimamlaka. Mamlaka hayo hujidhihirisha katika aina ya lugha inayotumiwa na wazungumzaji wake. Hivyo, kundi linalobahatika kumiliki aina ya lugha inayomiliki pia asasi muhimu kama elimu, siasa, uchumi na kadhalika linaweza kuamua mfumo upi utawale mahusiano baina ya wanawake na wanaume. Hivyo, katika hali inayojitokeza katika matumizi ya tashibiha ndani ya mashairi Shaaban Robert si bahati mbaya bali kinachotokea ni kwamba jamii iliyomkuza na kumlea msanii ilitawaliwa na mfumo dume ambao kwa karne nyingi imewekewa

mazingira ya kutamalaki na taasisi kama vile ndoa, siasa, utamaduni na dini.

Matokeo ya utafiti wakati wa mahojiano yalionesha pia kuwa kujikita kwa mfumo dume katika jamii ya waswahili kunakojidhihirisha katika ushairi wao hakutokani na nguvu za kimwili peke yake bali unatokana na uwezo wa kiuchumi na uhuru ulionufaisha tabaka tawala kupitia mamlaka ya wanaume dhidi ya wanawake na upendeleo wa kuwavamia wanawake kwa nguvu kwa lengo la kufanya nao mapenzi kulikokusudia kuthibitisha uanaume wa mvamizi. Kwa namna wazi kabisa (tunathubutu kusema hivyo katika utafiti huu tukitumia mifano linganishi ya ushairi linganishi wa mtindo wa ngoma ya *chagulaga* inayosemekana kuwa maarufu katika kabila la Wasukuma) sifa bainifu za mfumo dume zinajitokeza katika ushairi wa Kiswahili kwa kuwa jamii iliunga mkono mfumo dume ndani ya taasisi zilizowekwa katika jamii. Imebainika kuwa tanzu za fasihi kama vile ushairi uliotungwa na kuimbwa na makundi ya wanaume kutoka tabaka tawala waliomiliki dola na utajiri walihalalisha na kuendeleza mahusianao haya ya kijamii yaliyozalisha utawala wao.
Ili tuweze kuona mashiko ya madai haya chunguza beti za tenzi za Shaaban Robert hapa chini:

*Utenzi wa Hati*

*Leo nataka binti,*

*Ukae juu ya kiti,*

*Ili uandike hati,*

*Ndogo ya wasia.*

***Chanzo: Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk.36***

***/Pambo la Lugha uk.6***

*Utenzi wa Adili*

*Kijana lete kalamu,*

*Nina habari muhimu,*

*Napenda uifahamu,*

*Dadayo kasha zamuye.*

***Chanzo: Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini uk.21***

***/Pambo la Lugha uk.43***

Inavyoonesha msanii alikusudia kutoa wosia kwa watoto wake wote wawili lakini cha kushangaza ni kwamba alitoa ujumbe huu kwa upendeleo. Upendeleo huu unajitokeza anapotumia maneno ‘Ili uandike hati, Ndogo ya wasia’ lakini katika utenzi wa Adili anasema ‘Kijana lete kalamu, Nina habari muhimu.’ Sitiari ya *hati* kurejelea *wosia* imetumika kusawiri mahusiano ya kijinsia ambapo tunaona kuwa waosia unaomhusu mwanamke haupewi uzito unaostahili kiasi cha kuthubutu kusema *hati ndogo ya wasia* lakini mafunzo yenye maudhui yale yale yanapoelekezwa kwa mwanamume mwandishi anaona ni habari muhimu. Hivyo, ushairi wa Shaaban Robert umetumia tamathali za usemi kwa kiwango kikubwa katika kusawiri ujinsia.

Pia kwa mujibu wa Scott (1990), mahusiano ya kimamlaka yanabainishwa kwa kutumia nyaraka au nakala za nyaraka kuonesha mamlaka ya mtu zinazoonesha na kuhalalisha nafasi za watawala wa kada za juu na huimarisha utaratibu wa kutawala watu wa kada ya chini kiasi kwamba wanaume na wanawake wanaweza kuunganishwa kupitia nyaraka hizo za kiofisi zinazoakisi mfumo dume ambapo

wanaume huhalalisha utawala wao dhidi ya wanawake. Scott (keshatajwa) anatoa mfano wa jamii za kikabaila miongoni mwa Waswahili zilizokuwapo kati ya karne ya 18 na 19 zinazoelezwa kwa kina pia katika kazi za ushairi wa Kiswahili katika kuthibitisha hali hii. Hivyo, ukiritimba wa wanaume dhidi ya wanawake umeendelezwa na taasisi za kijamii kama ndoa.

Hali ya mahusianao baina ya wanaume na wanawake imezungumziwa na Parsons na Bales (1955) kwa kutumia *Nadharia Tete ya Mgawanyo wa Majukumu Kijinsia*. Kwa kutumia nadharia tete hii tunaweza kueleza kuwa Waswahili kama ilivyo kwa jamii nyingine ulimwenguni inaweza kujadiliwa na kufafanuliwa njia ijulikanayo kama *Nadharia Tete ya Majukumu Kijinsia*. Kwa mujibu wa nadharia tete hii, watu hujifunza stadi na kazi mbalimbali kutoka kwenye taasisi za kijamii na kuwafanya watende kama inavyokubalika kijamii na kama ifaavyo kutegemeana na jinsia zao. Nadharia hii ya kijamii inatambua mgawanyo wa majukumu ya kijamii baina ya wanawake na wanaume ambapo wanaume wanahima ya kutaka maendeleo, hufikiri kimantiki na kirazini, wana nguvu ya kutawala na hufanya mambo yao kwa malengo; hali iliyowafanya kutafuta kutawala, kuwa mahiri na kupenda mafanikio. Kwa upande mwingine, wanawake hawaoneshi hisia zao, ni wanyenyekevu, hujipenda au hujihusudu, wana mihemuko na ni wepesi wa kutosheka. Hata hivyo, nadharia hii imekabiliwa na upinzani kutoka kwa wanazuoni wenye mlengo wa kifeministi (Firestone (1972), Millett (1977), Showalter (1977), Chodorow (1978), Steady (1981), Ogundipe-Leslie (1984), Kristeva (1984; 1986)) kwa vile inapuuza uhalisia kuwa sifa bainifu za mfumo dume zimepewa nafasi kubwa na uzito kupindukia kuliko zile za mfumo jike na inachukulia kwamba jinsia ndio msingi pekee wa

utambulisho wa mtu kitu ambacho si kweli. Kuna vibainishi vingi zaidi ya jinsia ambavyo huwatambulisha watu binafsi au katika makundi yao kijamii (taz. Msanjila na wenzake, 2009). Tamathali za semi katika *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, Shaaban Robert anausawiri ujinsia kama walivyodai waasisi wa nadharia tete ya mahusiano ya kijinsia kwa kumchukulia mwanamke kuwa hatakiwi kutoa maneno makali hata kama anaonewa. Katika ubeti wa 54 wa shairi *Utenzi wa Hati* katika *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* tunakuta sitiari ya *pilipili* inayorejelea maneno mengi na makali toka mdomoni mwa mwanamke.

*"Ulimi wa pilipili,*
*Hutenga watu wawili,*
*Kuishi mbalimbali,*
*Hii hasara sikia."*

Utafiti huu uligundua kuwa matumizi ya neno *pilipili* limetumika kisistiari kurejelea tabia ya kuongea sana. Katika jamii zetu nyingi inachukuliwa kuwa mwanamke anayeongea sana hafai kuolewa kwa kuchukulia kuwa yeye ni mpoeaji wa maelekezo na taarifa kuhusu masuala yahusuyo ustawi wa familia.

Akieleza kinaganaga *Nadharia ya Mahusiano ya Kijamii* iliyoasisiwa na Jacques Lacan (1977), Weedon (1991:52) anafafanua kwamba taratibu zinazoongoza na kutawala katika mfumo dume ni sawa na taratibu za kijamii na kiutamaduni tunazoishi kama wahanga wa mahusiano ya kijinsia wenye urazini. Licha ya hali hii, taratibu hizi ndizo zinazoamua miundo ya lugha na kanuni za kijinsia zinazotawala pia matendo uneni yetu wakati wa mazungumzo. Lugha ina nafasi muhimu katika

kuimarisha taratibu zote za kijamii na kiutamaduni kwa sababu ndizo hueleza na kufasili nafasi ya mzungumzaji wa lugha husika. Kwa hiyo, maana ya *ujike* na *udume* inatofautiana kati ya jamii moja na jamii nyingine, kati ya utamaduni mmoja na utamaduni mwingine na inatofautiana pia baina ya lugha moja (Weedon 1991:22). Tofauti zote hizi zinategemea mabadiliko ya kihistoria kama inavyotokea tu katika vipindi mbalimbali vya kihistoria ambapo kunajitokeza aina tofauti za *udume* katika jamii ulimwenguni.

Kwa muda mrefu na katika vizazi vingi, fasihi ya Waswahili imekuwa ikitumika kuimarisha taratibu za mfumo dume na kuimarisha ujitokezaji wa *udume* katika matabaka na jinsia. Cornwall (1994:12) anaongeza kueleza kuwa katika ulimwengu huu hakuna *udume majumui* (*Universal Masculinity*) kwani mifumo na miundo ya *udume* hutofautiana baina ya jamii moja na jamii nyingine. Istilahi hii ina maana nyingi na maana tata zinazobadilikabadilika kutegemeana na muktadha na wakati. Hivyo, uchambuzi wa ushairi wa Waswahili hususan matumizi ya tamathali za semi katika kusawiri mahusiana ya kijinsia baina ya wanawake na wanaume umeonesha mwenendo huu ambapo *udume* una maana nyingi zilizoibuka katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa msimamo wa Shaaban Robert umekuwa ukibadilika kiasi kwamba msisitizo juu ya *ualfa* na *uomega* wa mwanamme katika mahusiano ya kijinsia unaonekana kuchukua mlengo wa kati na kusisitiza umuhimu na nafasi ya mwanamke katika jamii (rejea shairi la Mwanamke si Kiatu katika *Pambo la Lugha* uk. 19). Katika utafiti huu tunasisitiza kuwa lugha ni ndio silaha na malighafi inayotumika katika ushairi kuonesha hali na matukio mbalimbali katika jamii kwa kutumia seti ya silabi na vikumushi vya maana

na kwamba lugha pia ni mfumo wa kisitiari au kiishara. Mathalani, neno MWANAMUME limerasmishwa kwa muda mrefu na katika jamii nyingi katika kujenga uzoeshi wa kijamii kwa lengo la kumaanisha au kurejelea mamlaka au utawala. Maneno kama *uanaume* yamekuwa yakihusishwa pia na kiungo cha uzazi cha mwanamme. Vivyo hivyo, neno mwanamme linawakilisha umiliki na mamlaka katika tamaduni nyingi wakati ambapo neno mwanamke katika baadhi ya miktadha ya kijamii linapeleka ujumbe katika jamii unaohusishwa na udhaifu. Hii ndiyo sababu katika jamii za Kiafrika ni kawaida kusikia kuwa 'acha kulia kama mwanamke', au inapotokea kuwa mwanamme amepata tatizo hasa msiba husisitizwa kuvumilia asilie kwani yeye ni mwanamme na wakati mwingine unaweza kusikia mtu akihimizwa 'pambana kama mwanamme.' Kwa kuwa wanaume wameunganishwa na mifumo ya utawala kuna kaida ya kuwahusisha na taswira au picha ya alama na nembo za utawala. Mathalani, katika lugha ya Kiswahili kuna msemo '*Bunduki bila risasi itaua namna gani?*' Bunduki ni zana ya mamalaka na imekuwa ikihusishwa na wanaume kwa sababu wao mara nyingi ndio wanaoonekana kuibeba na kuitumia kwa matumizi mbalimbali.

Tafiti zilizofanywa katika isimujamii na wanaisimujamii kamavile Coates (1986), Johnson na Meinhof (1997), Holmes (1995), and Halliday (1978) zinaonesha kuwa wanaume wana namna ya kutumia lugha kwa lengo la kuendelea kumiliki lugha hiyo na vilongo vyake. Utambulisho wa *udume* unaweza kudhihirishwa kwa njia ya vitu vinavyoweza kupatikana kwa jitihada au kupotea na kunyang'anywa. Katika lugha ya Kiswahili kuna msemo pia '*Mume bila kazi si mume*'. Wakati mwingine msemo huu hufupishwa kama '*Mume ni kazi*' miongoni mwa Waswahili kama ilivyo katika

jamii nyingine, mwanaume ndiye mwenye jukumu la kutafuta mahitaji ya familia yake. Kama hana kazi au kipato kinachomwezesha kuingiza kipato, hawezi kuwa na uwezo wa kutimiza wajibu wake wa kijinsia kiasi kwamba heshima au hadhi yake kama mwanaume hutia mashaka. Kwa upande mwingine wanawake katika nafasi zao wana utamaduni wanaoutumia. Mathalani, baadhi ya maeneo ya nyumbani kama jikoni yamefanywa kuwa himaya yao kwa muda mrefu katika jamii za Kiafrika na jamii nyingine ulimwenguni. Ushairi wa Shaaban Robert unasawiri umiliki huu wa maeneo ya nyumbani unaofanywa na wanawake kwa kueleza kuwa:

*Mwanamke na ila, hapati wa kukubali,*
*Kusikia kwa muhula, mimi bado neno hili,*
*Wala hapana mahala, asipoonekana ghali,*
*Bibi ni mtawala, nyumbani kila mahali.*

*Japo nakaa mekoni, tungo hainishughuli,*
*Uliza mimi ni nani, Uelewe na asili,*
*Halafu uje wanjani, tuonyeshane kitali,*
*Ukiwa shiraziani, na mimi ni Mswahili.*

***Chanzo: Pambo la Lugha uk. 20***

Kasumba kama hizi zinaweka athari zake katika ushairi wa Kiswahili hii iligundulika katika utafiti huu kuwa sitiari ya *kiatu* ilitumika kuonesha ujinsia au mahusiano baina ya mwanaume na mwanamke. Kiatu kinachukuliwa kama kifaa ambacho binadamu anakitumia kumkinga na majanga mbalimbali na yeye ndiye anayepanga namna ya kukitumia. Sitiari hii inaonesha mahusiano ya kijinsia yasiyofaa baina ya mwanamke

na mwanamme. Tamathali hii ya usemi inatuonesha jinsi ushairi wa Shaaban Robert unavyosawiri mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme. Tazama beti zifuatazo kutoka katika shairi la '*Mwanamke si Kiatu*:'

*Vishindovyo si kitu, vyangu vikikabili,*
*Usilaghai watu, juu ya kitu cha mali,*
*Mwanamke ndichi kitu, bora hakina badili,*
*Ila kufanywa kiatu, hili hatalikubali.*

*Si wajibu kusema, mke hana fadhili,*
*Wapo waume si wema, tia katika akili,*
*Na mabaya yanauma, hapana wa kuhimili,*
*Ukivunja heshima mke naye hunakili.*

***Chanzo: Pambo la Lugha uk. 20***

Beti hizi zinatuthibitishia kuwa matumizi ya vipengele mbalimbali vya lugha katika ushairi ikiwa ni pamoja na tamathali za semi, zinaonesha mahusiano yasiyowiana baina ya mwanamke na mwana mme katika jamii nyingi za Kiafrika na mahali paengine ulimwenguni.

Katika jamii nyingi za Kiafrika, wanaume hawaruhusiwi kuingia jikoni kwa sababu kazi ya kupika siyo yao. Kutokana na hali hii, vifaa vya jikoni kama mwiko, kinu, ungo, ufagio na mchi mara nyingi havishikwi na wanaume. Kwa hiyo, kwa kuimarisha *udume* wa vifaa hivi, wanaume na wanawake hutengeana nafasi zao

kijamii. Uanzishwaji wa *udume* kwa kuwatenga wanaume katika baadhi ya maeneo ya majukumu ya kijamii huimarisha masuala ya kijinsia na kusaidia kuendeleza itikadi ya ukiritimba wa wanaume kwa wanawake katika mambo mengi. Hivyo, utambulisho wa kijinsia kwa muda mrefu umekuwa ukianzishwa na kuendelezwa kupitia mchakato wa ubaguzi na hufunzwa kwa wavulana katika hatua za awali kabisa za makuzi yao ili wanapokua waweze kuzingatie majukumu yanayoendana na jinsia yao. Vivyo hivyo, wasichana nao hufundishwa kaida za kijinsia zinazoendana na majukumu yanayowahusu katika jamii.

Chodorow (1978) aliwahi kueleza kuwa ili mvulana aweze kuamilia utaratibu wa majukumu ya kijinsia yanayomwangukia baba yake, anatakiwa kuacha kujitambulisha kwa kutumia jina la mama yake na kuepa kuandamana naye huku akikana sifa za *ujike* zinazohusishwa na mama yake. Wakati anachunguza sifa za utu, Doyle (1989) alifafanua sifa zinazoelezea sifa za mwanaume kama ni mtu anayejituma, mwenye malengo, ni mshindani, mbinafsi, anapenda kujitegemea, hulazimisha mambo yawe atakavyo yeye na anapenda kutawala.

Sifa hizi hujipenyeza katika mfumo wa kiishara au kisitiari ambapo lugha ina nafasi kubwa na hukitwa zaidi katika mamlaka yanayowiana na fasili ya *udume* ambapo Connell (1995) anaeleza kuwa hili ndilo *kundi kifani* linalotawala katika jamii husika. Kundi kifani hilo lilihitaji muundo ambao ungetumika kama njia ya kufasili na kutathmini mifumo na miundo mingine ya *udume* ulimwenguni. Jambo la kuzingatia hapa ni kwamba katika jamii ya Waswahili kama ilivyo katika jamii nyingine ulimwenguni, hali hii inajitokeza ikiwa tu mfumo dume umefanikiwa

kujikita na kuendelea kupitia kwa wanawake wenyewe kundi ambalo linakandamizwa. Kwa hiyo, wanawake katika jamii zinazofuata mfumo dume wamekubali utambulisho wa kijinsia na nafasi zao katika majukumu yao kijinsia. Hali hii inajidhihirisha bayana tunapochambua mashairi mengi ya Kiswahili si katika mashairi ya Shaaban Robert peke yake kwani mfumo dume ni suala mtambuka kwa jamii nyingi Afrika na ulimwenguni kwa ujumla.

Mfano mzuri unapatikana katika ushairi wa mshairi maarufu wa kike karne ya 19 kutoka Lamu, Mwanakupona binti Mshamu (1790-1860) aliyekuwa akiishi upwa wa kaskazini mwa Kenya kutoka jamii tawala ya kikabaila. Mshairi huyu alitunga *Utendi wa Mwanakupona*, shairi ambalo lilikuwa na beti 102 akitoa wosia kwa binti yake aliyeitwa Mwana Hashima binti Sheikh. Kwa kutumia lahaja ya Ki-amu alitunga shairi hili lililosheheni maelezo kuhusu majukumu ya mwanamke aliyotaka binti yake ayazingatie pindi atakapoolewa. Katika kazi hii, anamfundisha binti yake na wasichana wote wa wakati huo namna ya kuweza kuishi katika jamii ya mfumo dume unaosimamiwa na dini ya Kiislamu ambapo mke anatakiwa kumhudumia mumewe kikamilifu, kwa unyenyekevu na upendo wa hali ya juu. Ubeti ufuatao unathibitisha hali hii:

*Mama haya yasikize tafadhali*
*Sinipuze utaona nafuuze za*
*Akhera na duniya*

Wakati ambapo unyenyekevu ni maadili ya kidini, mwanamke anaonywa pia kuwa asipomhudumia mumewe kwa unyenyekevu ambao ni sehemu ya mila za kijamii

atapata dhiki duniani na hata baada ya kufa. Shairi hili linamfundisha pia lugha nzuri anayopaswa kuitumia na ufundi wa kumridhisha mumewe. Msisitizo wa matumizi ya lugha nzuri unakusudia kundeleza na kutimiza matakwa ya mfumo huu wa kijamii kama inavyoonekana katika ubeti ufuatao:

*Uonapo uso wake funua meno uteke*
*Akwambialo lishike illa kuasi*
*Jaliya*

*Mama sinoe ulimi nioleze wako*
*Umi naliowa nyaka kumi*
*Tusitete siku moya*

Kwa hiyo, matendo uneni yafaayo yalitakiwa ili mwanamke akubalike katika jamii na katika kundi lake la kijamii, yaani tabaka tawala la makabaila. Lugha itakiwayo hapa inamaanisha pia lugha inayoendana na jinsia yake. Katika mashairi ya Shaaba Robert hususani ubeti wa 28 na 54 katika kitabu chake cha *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* tunaona pia matumizi ya dini kama zana ya kulainisha tabia za mwanamke pamoja na lugha iendanayo na jinsia yake msanii anaposema:

*Dini mali ya roho,*
*Mwilini kama joho,*
*Unapoteza uroho,*
*Na anasa za dunia.*

*Ulimi wa pilipili,*

*Hutenga watu wawili,*

*Kuishi mbalimbali*

Nia yetu si kufanya uhakiki linganishi ila tuliona ni muhimu kuonesha picha halisi katika ushairi wa Kiswahili kuhusu nafasi ya tamathali za semi katika kusawiri ujinsia katika jamii zetu. Msichana anapofanya jitihada za kuwa mahiri wa kutumia lugha ya mazungumzo katika jamii yake huweka jitihada kubwa za kuhakikisha kuwa anazungumza kwa namna inayomtambulisha kama mwanamke au msichana wa nasaba au kundi linalokubalika na kutambuliwa na mfumo tawala wa jamii yake. Utaratibu huu unahitajia kwamba wanawake wanapaswa kuwahudumia waume zao kwa, kuonesha kuwa wanafurahia kutimiza wajibu wao huo na kwa kufanya hivyo wanapaswa kuzingatia kuwa wanawaridhisha waume zao kwa kuonesha uwezo wa kutimiza wajibu kupitia utekelezaji wa majukumu yao ya kijinsia ipasavyo ili waweze pia kuishi katika ulimwengu unaomilikiwa na wanaume kupitia mfumo dume unaolindwa na taasisi zake.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1982), picha ya mwanamke kupitia matumizi ya lugha kama tamathali za semi, ushairi wa watunzi wake kama vile Shaaban Robert na Mwanakupona inaoneshwa kuwa ni kiumbe mnyenyekevu asiyependa kupinga hali ya mambo kama yalivyo katika jamii yake na kama tukavyoona katika sehemu inayofuata; mwanamke amefanywa chombo cha kutimiza haja na tamaa za wanaume. Kwa hakika, ushairi wa Kiswahili umefanikiwa kuonesha hali halisi ya namna ambavyo udume ulivyopenyezwa kwa wanawake hasa wale wa tabaka la juu (taz. Mulokozi, 1982).

## 4.4 Tamathali na Semi Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke

Utafiti huu ulichunguza jinsi tamathali za semi zinavyosawiri nafasi ya mwanamke katika jamii. Ilielezwa katika majadiliano ya vikundi kuwa tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert husawiri nafasi ya mwanamke katika mamabo mbalimbali ya kijamii. Mambo yaliyotajwa ni: mwanamke katika asasi ya ndoa, mwanamke katika kufanya maamuzi, mwanamke katika elimu, mwanamke katika uzazi na malezi, mwanamke katika mapenzi, mwanamke katika utamaduni, mwanamke katika dini na mwanamke kama kiumbe muhimu katika jamii. Sehemu ifuatayo inajadili matokeo haya kwa mifano kutoka katika mashairi.

### 4.3.1 Mwanamke Katika Asasi ya Ndoa

Katika sanaa hii ya ushairi mwanamke amewekwa katika nafasi mbalimbali. Wapo wasanii waliomtweza mwanamke na wapo waliomkweza. Mwanamke ni neno la kidhahania, na kiutamaduni lililobuniwa na jamii kwa malengo mahususi ili liyakinishwe na mila au utaratibu wa jamii husika (Ruthven 1984). Tofauti kubwa kati ya mwanamke na mwanaume mbali na jinsi, ni ile ya mwanamke kunyanyaswa, na mwanaume ndiye mnyanyasaji. Wanazidi kueleza kwamba, mwanaume hashiriki kabisa katika kunyanyaswa ila yeye ndiye anayefaidika. Hiyo ndiyo sababu wanawake walitaka kujikomboa wenyewe bila kuwashirikisha wanaume, kwani walijiona wao ndio waathirika wakubwa wa unyanyasaji.

Kuhusu hali hii, sababu sio kukandamizwa bali kuelewa kuwa maisha ya kiukandamizwaji aishiyo mwanamke hayasababishwi na ujinsia tu bali pia na ubaguzi, umri, na utabaka. Urazini huo ndio uliomuinua mama Tau kutoka nyumbani

na kuanza kumsaka mume wake. Shaaban Robert ametumia sitiari na tashibiha katika kuonesha nafasi ya mwanamke katika jamii katika shairi lake la ‘Mume na Mke.’ Mshairi huyu anaeleza mahusiano ya kijinsia na nafasi ya mwanamke katika jamii kwa kueleza kuwa:

*Mwanamke ni mwili, damu yetu na mfupa,*

*Kweli ya neno hili, moyo umepiga chapa,*

*Na kila mwenye akili, yamkini hataapa,*

*Kuwa hii ni batili, leo isemwayo hapa.*

***(Pambo la Lugha uk.31)***

Ubeti huu unatuonesha kuwa nafasi ya mwanamke katika jamii ni kiumbe tegemezi kwani hata chimbuko la uwepo wake dunia ni sehemu ya damu na ubavu wa mwanaume. Mbiu hii inatolewa pia na misahafu ya kidini kama vile Biblia kwa kuna mafundisho yanayoeleza kuwa mwanamke ni ubavu wa mwanaume.

### 4.3.2 Mwanamke Katika Kufanya Maamuzi

Uwakilishi wa wanamke ni mdogo sana popote pale maamuzi yanapofanyika bila kujali ngazi au taasisi inayohusika. Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) (2001: 44-45), wanaeleza kwamba, tofauti ni kubwa kati ya wanawake na wanaume katika masuala ya kijamii yanayojitokeza serikalini katika ngazi ya uongozi na utoaji wa maamuzi. Licha ya ukweli kwamba, katiba ya mwaka 1977 pamoja na kufanyiwa marekebisho mwaka 1984 inatoa haki sawa kwa wanawake na wanaume kupiga kura na kutumikia umma, bado uwakilishi wa wanawake ni mdogo sana. Ufanyaji wa maamuzi katika ngazi ya kaya bado sio wa kidemokrasia, kwani wanawake na

watoto wa kike hawahusishwi. Mathalani, katika suala zima la siasa, mwanamke analazimishwa na mwanaume kumchagua kiongozi ambaye ni chaguo la mwanaume. Pullen (2006) anamuelezea Phillip Snouden ambaye mwanzoni alikataa kuwaunga mkono wanawake kushiriki katika kupiga kura, lakini baadaye aliwaunga mkono wanawake kupiga kura kwa sababu alishawishiwa na mke wake. Mwanzoni alikataa kwa sababu kihistoria umoja wa wafanyabiashara wanaume ndio waliokuwa na haki ya wafanyakazi ingawa sasa mfumo huo haupo. Mafeministi wanadai usawa wa kijinsia na haki ya kuchagua kuwa ni wa wote. Nafasi ya mwanaume ya kumtawala mwanamke imekuwa wazi kutoka hadithi moja hadi nyingine inayomdunisha mwanamke. Kipengele hiki ni muhimu sana kwani kinatoa fasili ya wanaume kama wanaume na wanawake kama wanawake.

Changamoto ya ubabe huo inayochukuliwa kama mabavu ya mwanaume ni kitambulisho kinachomuelezea mwanaume. Kwa sababu tu mwanamke huyu alilipiwa mahari wakati anaolewa, basi kila atakachokifanya lazima kiridhiwe na mwanaume. Mwanamke anapoteza haki yake ya msingi ya kumchagua kiongozi anayemtaka, kwa kuogopa kutalikiwa. Hata hivyo TGNP (2001) wanasema kwamba itikadi ya kawaida inayotumika ulimwenguni kote kuunda mahusiano ya kijamii ni ‘mfumodume’ ambao unabainisha dhima duni ya wanawake pamoja na jinsi wanavyonyanyaswa na kunyonywa. Itikadi hiyo ya mfumo dume inaathiri sana uchaguzi, kwani wanawake hawawezi kushindana na wanaume katika kuchagua wala kuchaguliwa. Kwa kutumia mbinu ya takriri wazo, Shaaban Robert anasisitiza kuwa ni upuuzi kuendelea kushikilia na kuamini kuwa mwanamke ni kiumbe duni kiasi kwamba haifai kumpa nafasi ya kushiriki katika kupanga mipango ya

maendeleo na kushiriki katika kufanya maamuzi juu ya masuala mbalimbali. Katika kukemea tabia ya kuwapuuza wanawake msanii huyu anasema:

*Kwa nguvu nakaidi, hoja hii ya kijinga,*
*Kisha nina jitihadi, mahali inapojenga,*
*Isistawi zaidi, sababu haina mwanga,*
*Giza lake uhasidi, huvutia watu janga.*

*Huvutia watu janga, wasipatane maneno,*
*Mwanamke kumtenga, kuwa duni ya kifano,*
*Na mimi hapa napinga, kufanya mapigano,*
*Kwamba huu ni ujinga, naupatiliza mno.*

***Chanzo: Pambo la Lugha uk. 32***

Kwa kutumia beti hizi msanii anatuonesha kuwa kuna haja ya kuhakiki mifumo yetu ya kijamii kwani inakwamisha maendeleo kwa kuwatenga baadhi ya wadu wa maendeleo kwa kuamini kuwa hawana mchango wowote katika kuleta maendeleo hayo. Hivyo, tamathali za usemi hapa zimetumika kumchora mwanamke kama kiungo muhimu katika ustawi wa jamii yoyote.

### 4.3.3 Mwanamke Katika Elimu

Elimu ni haki ya msingi kwa kila mtu - mwanaume na mwanamke. Sera za Elimu ya Msingi kwa Wote na Elimu ya Watu Wazima za mwaka 1974 kwa pamoja zimesaidia angalau kwa kiasi wanawake na wanaume kupata elimu japo ya msingi. Katika sanaa hii ya ushairi mwanamke anapewa nafasi na amesisitizwa kuzingatia

elimu katika wosia uliotolewa na mwanadishi. Wapo wanawake wengine waliozinduka na kuwa makini na unyanyasaji uliowanyima fursa ya kupata elimu katika siku za nyuma na jitihada za ukombozi zingali bado zinaendelea. Hawako tayari kupoteza haki zao za msingi kama kupiga kura, kwani wana haki ya kushiriki katika uzalishaji wa maarifa na wana haki ya kuwa sehemu ya maarifa hayo kama Macknonn (1991) anavyoeleza. Wanawake wamepata elimu juu ya uchaguzi wa viongozi na wanaujua wajibu wao kama wapiga kura. Kwao sio rahisi kukubali haki yao inyang'anywe mbele ya macho yao bali hupambana hata waone mwisho wao. Kuhusiana na hili msanii anatumia taswira ya wosia kama tamathali ya usemi kusisitiza umuhimu wa elimu kwa wanawake. Katika Pambo la lugha suala la elimu limejitokeza kama ifuatavyo:

*Hati hii ni nuru,*
*Shika nakuamuru,*
*Mungu atakunusuru,*
*Akuepushe na baa.*

*Elimu kitu kizuri,*
*Kuwa nayo ni fahari,*
*Sababu humshauri,*
*Mtu la kutumia.*

***Chanzo: Pambo la Lugha Uk. 38***

Takwimu za taarifa ya TGNP (2001) zinabainisha kwamba asilimia 25 ya wasichana huacha shule kabla ya kumaliza masomo. Sababu za wasichana kuacha masomo ni

kuolewa, mimba, utoro, mazingira mabaya kielimu, fikra potofu za wazazi, na msukumo wa kiuchumi. Aidha, mwanamke hapa anaonekana kuacha shule kwa sababu za kuolewa huku mwanaume akimdanganya kwamba atamsomesha. Hapo mwanzo wazazi hawakuona umuhimu wa kuwapeleka watoto wa kike shuleni kwani walijua wataolewa tu. Kwa hiyo wakiwasomesha hawataweza kuwasaidia wazazi wao ila watawasaidia waume zao. Kutokana na hilo hawakuona sababu ya kuwasomesha mabinti zao ila kuwaacha vivyo hivyo bila hata kujua kusoma na kuandika. Hilo lilikuwepo sana hasa katika miaka ya 1961 na kabla ya uhuru.

Kampeni za serikali za Elimu ya Watu Wazima zilizoanza baada ya uhuru ndizo zilizosaidia ongezeko la wanawake kujiunga na kisomo hadi kufikia asilimia 61 mwaka 1975 na hadi asilimia 90 kwa wanaume mnamo mwaka 1984. Kufikia mwaka 1988, kiasi cha wanawake waliojua kusoma na kuandika kilifikia asilimia 88 (TGNP 2001). Hay (2006) kama alivyonukuliwa na Pullen (2006) anaeleza kwamba elimu hasa elimu ya juu katika hisia au mawazo ya vijana wanawake haipo, kwani hufikiri kwamba haiwahusu. Anaona ni vema utamaduni huo uvunjwe miongoni mwa mabinti wadogo kwani wote wanastahili elimu sawa na vijana wa kiume. Hata kama mtoto huyo wa kike alipenda kusoma sana lakini ataishia kupenda na kutamani tu bila kutimiza tamaa yake ya kutaka kusoma.

Hali za wanawake zinakuwa mbaya kwa sababu hawana haki sawa na wanaume ya kupata umiliki wa rasilimali yoyote ikiwemo elimu. Tatizo sio kukosekana kwa chakula au mali katika ngazi ya familia, bali mwanamke hukosa nguvu na mamlaka katika umiliki wa rasilimali hizo. Ijapokuwa siku hizi wazazi wengi wanawapa

watoto wa kike nafasi ya kusoma lakini msanii hawezi kutoa jambo hewani tu lazima litakuwa na mizizi yake katika jamii. Hivyo katika jamii ni dhahiri kwamba bado wapo wazazi wasioona umuhimu wa kumsomesha mtoto wa kike. Kukosekana kwa elimu kwa wanawake wengi, na urazini juu ya suala la uzazi unakuwa mdogo au haupo kabisa kwa wanawake wengi. Tumwangalie mwanamke katika suala la uzazi ana uwezo wake wa utambuzi katika suala la afya ya uzazi.

### 4.3.4 Mwanamke Katika Uzazi na Malezi

Utafiti huu uligundua kuwa mwanamke katika suala la uzazi hathaminiwi kabisa na wala hapewi nafasi ya kupanga idadi ya watoto atakaozaa. Pia anapokuwa katika hali ya ujauzito, hapati matunzo yanayostahili ili aweze kupata afya, ila anaishi kwa kunyanyasika mpaka atakapojifungua. Amri ni sheria ambayo ikivunjwa kifuatacho ni adhabu. Hii ni kumnyima mwanamke haki yake ya msingi ya kupata huduma za afya na elimu ya uzazi (Bader, 1974). Wanaume wengi wanafanya hivyo kwa kuogopa gharama za uzazi wakati wake zao wanajifungua, ndio maana katika katuni hiyo hapo juu, mume anamwambia mke wake kuwa ili ajifungue kirahisi ni lazima ale mahindi tu. TGNP (2001) katika utafiti wao wanaeleza kwamba ukosefu wa chakula cha kutosha kwa wingi na ubora husababisha aina mbalimbali za utapiamlo na hata vifo- hasa inapochanganyika na ugonjwa. Hii hujitokeza kwa watoto na wanawake, kama vile wanawake wajawazito na wanaonyonyesha. Katika suala la afya hasa ya uzazi mwanaume hajihusishi, na hata ikiwa wapo wanaojihusisha ni wachache sana ukilinganisha na uhitaji wenyewe ulivyo. Data zinaonesha kwamba sehemu kubwa za vijijini zina viwango vya juu vya vifo zaidi ya mijini. Asilimia 52 ya wanawake wajawazito, wana magonjwa yanayoletwa na upungufu wa madini

joto. Kwa akina mama wajawazito ukosefu wa damu na utapiamlo vinapelekea watoto wengi kuzaliwa njiti, kuzaliwa na uzito mdogo na kufia tumboni (TGNP 2001:71). Malezi na matunzo ya mimba ni muhimu kwani hii itamuepusha mama mjamzito na maradhi madogo madogo ambayo yangeweza kumkuta na kusababisha kifo. Msanii anatumia tamathali za semi kuonyesha nafasi ya mwanamke katika suala la uzazi anatumia takriri wazo kuonesha nafasi ya mwanamke katika uzazi kwa kueleza:

*Tumbo la rutuba,*

*Umepewa kama huba,*

*Uzae mama na baba,*

*Kustawisha dunia.*

***Chanzo: Pambo la Lugha Uk. 41/ Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini Uk.16***

Aidha, utafiti huu uligundua kuwa suala la malezi ya familia ameachiwa jukumu mwanamke Mfano mzuri kupitia katika kitabu chake cha *"Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini"* mwandishi analionyesha hili pale anaposema,

*"Watoto wako wapende,*

*Katika moyo wako wagande,*

*Na uwezalo litende,*

*Liwafae baadaye" (Uk -30 ).*

Pia katika *"Utenzi wa Hati"* mwandishi Shaban Robert analionyesha jambo hili pale anaposema,

*"Kwa hivi una uzazi,*

*Kuuguza na ulezi,*

*Kutaka maangalizi,*

*Bora hati yakwambia" (Uk –16).*

Mifano hii inaonyesha kuwa mwanamke amepewa nafasi kubwa katika malezi ya familia tofauti na mwanamme. Msanii ametumia neno 'wagande' kuonyesha kwamba mwanamke anapaswa kuwapenda watoto wake na awaweke katika moyo wake.

### 4.3.5 Mwanamke Katika Mapenzi

Kuhusiana na suala la mapenzi, Shaaban Robert amemchora mwanamke kama kimbe mwenye fursa sawa na mwanaume katika kuimarisha mahusiano na furaha ya ndoa yenyewe (shairi la mapenzi katika Pambo la Lugha uk 7).

### 4.3.6 Mwanamke Katika Utamaduni

Katika utamaduni mwanamke amechorwa pia kwa hali ya kudhalilishwa, kuaibishwa kuonewa, kunyanyaswa na kukandamizwa. Kwa kuwa mwanamke tangu kale utamaduni ulimtaka awe mtu mnyenyekevu, mtiifu kwa mumewe, basi ameendelea kunyanyasika na kudhalilishwa. Simone de Beauvoir (1972) ni miongoni mwa wanawake wanaoipiga vita mitazamo ya kitamaduni inayomuona mwanamke kama kitu hasi na kama binadamu kielelezo. Utamaduni ndio unaoweka alama zinazoonesha nafasi na majukumu ya mwanamke na mwanaume. Kipengele cha utamaduni kinatengeneza mazingira ya kumkandamiza mwanamke asifikie ngazi za

juu za uongozi kwani wanaume hawaamini kama wanawake wanaweza kuwaongoza vizuri kabisa na kuyatimiza maamuzi ya wanaume na wanawake kwa usawa. Siku zote wanaume wanapata mashaka juu ya uongozi wa mwanamke katika suala la uongozi. Pia huweka alama ambazo hulingana na uthamani wa kijinsia. Hapa basi, wanaume ni wanajamii walio katika tabaka la juu na wanawake katika tabaka la chini. Kwa mfano, kazi zinazofanywa na wanawake hazionekani kuwa ni muhimu wala kuwa ni kazi za kimaendeleo. Hata kama zikionekana kuwa muhimu, muonekano huo hauelezewi katika ngazi ya jamii isipokuwa katika ngazi ya familia tu. Rosaldo (1986) anaona kuwa mwanamke wakati wote anachorwa katika mtazamo hasi na haoni kama kweli kuna ukombozi wa jinsia ya kike kutokana na mfumo wa utawala wa kiutamaduni ambao unamilikiwa na wanaume.

Kama asemavyo Balisidya (1982), fasihi simulizi inadhihirisha kwamba mwanamke alifundishwa tangu kale. Tena anajua kwamba akiisha kutolewa mahari hawezi kumkimbia mume wake wala familia ya mume wake hata kama ataonewa, atanyanyaswa na kukandamizwa. Lakini hata hivyo inampasa kuvumilia tu pale pale kwani yuko kwenye kifungo cha mahari ambayo wazazi wake hawawezi kuilipa tena. Katika jamii nyingine mwanamke anaonekana kama bidhaa kwa sababu ananunuliwa. Kiango (1982) katika uchambuzi alioufanya wa tamthiliya ya *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* anaweka bayana jinsi mwanamke anavyoonekana kama bidhaa mfano wa mbuzi na pindi anaponunuliwa huwa mali ya mnunuzi. Pia mtoto yeyote atakayezaliwa katika familia hiyo naye anakuwa mali ya mwanaume. Utafiti uliofanywa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), kama walivyonukuliwa na timu ya FEMA (2010), umehusisha ulipaji

mahari na unyanyasaji wa wanawake. Utafiti huo umeonesha kuwa unyanyasaji huo unaohusishwa na mahari ni kama vile wasichana kukatishwa masomo ili waolewe, kuvumilia vipigo na kupoteza haki ya kumiliki mali.

FEMA (2010) wanasema kuwa, ijapokuwa ni utamaduni wa Watanzania na Waafrika kwa ujumla kwamba, wanawake baada ya kuolewa wanatarajiwa kuhudumiwa na kulindwa na waume zao, lakini matokeo yake wanawake sasa wanakuwa hawana mamlaka katika jamii, wamebakia majumbani, na kuzaa watoto. Pia utamaduni unamnyanyasa mwanamke kwa sababu mwanaume katika jamii nyingi habebi wala kufanya kazi yoyote ile ambayo inaonekana kuwa ni ya akina mama. Wengine wanahofia kuchekwa na wengine ni ujeuri tu na kukosa huruma. York na wenzake (1991) wanaelezea ukombozi wa mwanamke katika mojawapo za kanuni za ukombozi wa mwanamke kwamba:

*Wanawake wote wanashiriki katika unyanyaswaji mmoja tofauti kubwa kati ya wanawake na wanaume (mbali na ujinsia) ni kwamba unyanyasikaji wa wanawake ni maalumu kwa faida ya wanaume ambapo wanaume ndio wanyanyasaji. [Tafsiri yangu]*

Kutokana na hilo ijapokuwa mwanamke analemewa na mambo mengi na kazi nyingi hawezi kulalamika wala kupinga unyanyasaji huo, kwa sababu utamaduni unamtaka awe na heshima na asiwe mbishi. Lakini York na wenzake (weshatajwa) wanaeleza kwamba mapambano ya ukombozi wa mwanamke yawe na uhuru na ya kujitegemea na yafanye kazi nje ya matakwa ya wanaume, na wanaume wasiwepo kabisa katika mapambano hayo.

Hata hivyo, wanaume wengine ni wakali na wakorofi hata kama wake zao wamewaomba kwa upole wawasaidie baadhi ya kazi nzito wanaweza hata kuwapiga wakidai kwamba wanawake hao hawana adabu tena ni jeuri. Lakini hata hivyo yote hayo yanasababishwa na mfumo dume uliopo katika jamii. Mfumo dume ni utawala wa kibaba, na mtazamo mkuu wa ustaarabu wetu unaoonea, unaotawaliwa, unaoundwa na kuongozwa na wanaume.

Hii ni kwa sababu ya kuwafanya wanawake kuwa wasaidizi wa wanaume katika nyanja zote za utamaduni, dini, familia, siasa, uchumi, sheria na sanaa. Birkett na Harvey (1999:1) nao wanaelezea kwamba mfumo dume umeasisiwa na wanaume ili kuwatawala wanawake na watoto katika familia na katika jamii kwa ujumla.

Nafasi ya mwanamke katika utamaduni imesawiriwa na msanii kwa kueleza yafuatayo:

*Majivuno hayafai,*

*Yanaleta uadui,*

*Japo mtu humjui,*

*Kumdunisha hatia.*

***Chanzo: Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini Uk.13***

Vilevile sitiari 'mtu mwongo ni msungo' katika ubeti wa 50 katika kaitabu cha *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* inasawiri nafasi ya mwanamke katika utamaduni wa jamii kama ya Waswahili ambao uongo kwao ni uadui katika kuleta mwafaka na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

### 4.3.7 Mwanamke Katika Dini

Katika utafiti huu iligundulika kuwa dini inatumika kuonyesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume. Dini inatumiwa kumkandamiza mwanamke kwa kumfanya awe tegemezi na mnyenyekevu kwa mwanaume. Wakati huo huo mwanaume anapewa nafasi ya pekee na mamlaka kwa mwanamke. Hili limejidhihirisha katika mifano ifuatayo;

Pia dhana hii ya *ustahimilivu* imejitokeza tena katika UTENZI WA HATI

*"Na mume msishindane,*

*Wala msinuniane,*

*Jitahidi mpatane,*

*Ndio maisha ya ndoa.(uk 11)*

Suala la kumcha mungu, pia mwandishi **Shaban Robert** kupitia ***"Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adili"*** anaonyesha kuwa jinsia zote mbili zinahitaji kumcha mungu ipasavyo katika kila siku ya maisha yao, Mwandishi analionyesha suala hili pale anaposema,

*"Shikamana na ibada,*

*Kutimiza kila muda,*

*Na kesho ina faida,*

*Ikisha hii dunia" (Uk -10 ).*

Vilevile mwandishi anaonesha umuhimu wa kumcha mungu pale anaposema,

*“Kwanza mche mungu,*

*Mtengeneza ulimwengu,*

*Juu akaweka mbingu,*

*Nyota zituangaze” (Uk – 10).*

Momanyi (2001) anasema kuwa dini ni imani zilizovyazwa na kuhimiliwa na mifumo ya kuumeni. Ni asasi ambayo huheshimiwa sana na waumini. Mernissi (1987: 19-21) anasema kwamba, mwanamke katika asasi hii huonekana kama kiumbe hatari, mdanganyifu na asiyeaminika. Katika dini ya Kiislamu mwanamke huonekana kama kiumbe anayepaswa kutengwa na mwanaume ili asimwingize katika majaribu au dhambi na hivyo huonekana kama kiumbe ambacho ni najisi kinachoweza kumnajisi mwanaume. Katika makala za Ufeministi wa Kiislamu zilizopo katika *Wikipedia Free Encyclopedia* zinaeleza kwamba mwanamke muislamu hawezi kukaa mbele ya wanaume kwa kuwa ataondoa udhu wa wanaume kwa kuwepo kwake hapo mbele. Imam an-Nawawi anasema kwamba, kama mwanamke atawaongoza wanaume katika maombi ya pamoja, maombi hayo kwa wanaume hayatakuwa kitu. Pia dini huko Saudia imemkataza mwanamke wa Kiislamu kula mbele za umma, kwa kuwa sehemu ya uso wake itaonekana, kwa hiyo katika migahawa mingi vizuizi vimewekwa ili kuwasitiri wanawake.

Hata hivyo Al-Hubri (2000:221) anapinga na kusema kwamba, sheria ya Kiislamu kuhusu mwanamke imetazamwa na wamagharibi kama mfumo dume na ukandamizaji. Wanazuoni hao wa Kimagharibi, wameegemea zaidi katika demokrasia na haki za binadamu na kwa namna fulani, inaonekana kuwa

ukandamizaji usio na matumaini kwa mwanaume, hususani katika nchi za Kiisalmu. Anasema kwamba hitimisho hilo si sahihi kwa kuwa wanawake wengi wa Kiislamu wako makini na dini yao na wanakubali kutatua matatizo yao kutoka katika mfumo huo. Naye Noordin (2008:143) anaeleza kwamba ufeministi wa Kiislamu unadai haki za mwanamke mpaka nyumbani. Anaeleza kuwa nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu, humwangalia mwanamke kwa heshima, usawa, haki, na taadhima. Lakini Taib, (2008:133) anasema kwamba fasihi haitoki katika ombwe tupu bali hutoka katika zao la jamii ambalo limejengeka na hali halisi ya maisha ya jamii husika, yaani mtu na mazingira yake ndio Alfa na Omega ya fasihi.

Mitazamo hiyo inapishana lakini kama Taib (2008) anavyoeleza kwamba fasihi haitoki katika ombwe tupu, kielelezo hicho kinamchora mwanamke kama kitu najisi mbele ya mwanaume. Pamoja na kwamba dini inamkandamiza mwanamke, lakini msanii anamuonesha mwanaume kugeukia pembeni na kamba ya kupimia imepita sehemu ambayo siyo ya kupimwa (kwenye msamba). Hapa ndipo msingi wa ucheshi ulipo. Mwanamke naye anaangalia upimaji huo na kushangaa kwa kuwa hapimwi kama inavyotakiwa ila fundi amegeuka na kupitisha kamba ya kupimia pembeni kabisa huku akiuliza umma kama saumu zinakubalika. Zilmann na Cantor (1976:105), wanasema kwamba pale inapotokea hitilafu, utofauti ambao haukutegemewa, mshangao, chuku, na hisia za uso huleta kicheko kwa mtazanaji au msomaji. Katika kilelezo hicho, tunaona kwamba kuna kuhitilafiana kati ya fundi na mteja, utofauti ambao haukutegemewa hivyo tunapata mshangao na kutufanya sisi wasomaji kucheka. Nafasi ya mwanamke katika dini inajitokeza kwa kuhimizwa kwake kuishika dini mfano wa joho, yaani kama ambavyo anaambatana na nguo

zake ili kujisitiri, basi dini nayo iwe vazi la roho yake. (taz. Ubeti wa 28 katika *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini).*

### 4.3.8 Mwanamke Kama Kiumbe Muhimu Katika Jamii

Utafiti huu uligundua kwamba pamoja na kuwa shaaban Robert katika mashairi yake anatumia tamathali za semi kumchora mwanamke na kuonyesha mahusiano tofauti ya mwanamke na mwanamme katika jamii. Utafiti huu uligundua kuwa msanii huyu ametumia tamathali za semi kuonyesha umuhimu wa mwanamke katika jamii. Kwamba mwamke ni mzazi, mlezi na pia mwanamme hawezi kuishi bila mwanamke. Hivyo mwanmke ni kiungo cha jamii. Kwa mfano katika shairi la *PEKE* lililopo katika ukurasa wa pili katika diwani ya Pambo la Lugha msanii anasema;

*PEKE*

*Mpenzi wangu mwanadani, tangu nilipoona,*
*Hali yako taabani, furaha moyoni sina,*
*Lepe kupata machoni, la usingizi nakana,*
*Poa tuwe furahani, kuishi peke siwezi.*

*Siwezi kuishi peke, peke ni utelezi,*
*Naomba dua ifike, apokee Mwenyiezi,*
*Ishuke Baraka yake, akuvike wokozi,*
*Peke ina makeke, kilio na majonzi.*

Katika mfano huo msanii anatumia sitiari utelezi urejelea upweke. Anasema peke ni

utelezi, hapa msanii anaufananisha upweke na utelezi. Msanii anaonyehsa hatari ya mwanaume kuishi peke yake bila mke kuwa ni sawa na utelezi ambao katika utelezi mtu huweza kuanguka.

Aidha kwa kutumika tamathali za semi, msanii anaonyesha umuhimu wa mwanamke na usawa wa mwanamke na mwanamme katika shairi la *mwanamke si kiatu*. Tazama katika mistari ifuatayo;

*MWANAMKE SI KIATU*

*Chama kutaka utii, kichekesho si kweli,*
*Chama hutaka ridhai, mapatano ya kamili,*
*Yapimwe yasirufai, mume kwa mke ratili,*
*Halidi natumai, bure umekwenda mbali.*

*Vyama tofauti, kila chama mbalimbali,*
*Utii huja kati, kwa chama cha serikali,*
*Mume na mke sharti, mapenzi yakabili,*
*Huchukiza tasiliti, kusema hili na lile.*

*Wanawake wana laana, jibu lako ufedhuli,*
*Tena mimi naona, lawama lastahili,*
*Kuwa hujui kunena, u mchache wa akili,*
*Wanawake bora sana, ni hazina ya awali.*

***Chanzo: Pambo la Lugha Uk. 19***

Katika ushairi huo tunaona msanii ametumia ishara ya ‘kiatu’ kuikosoa jamii juu ya mtazamo hasi kuhusu mwanamke na nafasi yake katika jamii. Katika uhalisia kiatu huvaliwa chini mguuni na mtu hukitumia kwa kukanyagia na kutembelea. Hivyo kumshusha hadhi mwanamke na kumuweka chini ya mwanaume ni sawa na kumgeuza mwanamke kuwa ni kiatu. Hivyo ishara hiyo imetumika katika kusisitiza umuhimu wa mwanamke katika jamii. Anachosistiza katika shairi la *Mwanamke si kiatu* ni kwamba mwanamke ana nafasi sawa na wanaume katika kushiriki kazi mbalimbali, kushiriki katika maamuzi na haki ya kurithi mali. Wakati wa mahojiano na watafitiwa, mtafiti alibaini kwamba mtazamo hasi juu ya wanawake bado upo ingawa nguvu yake imepungua sana.

Msanii pia natumia tamathali za semi kuonyesha umuhimu wa mwanamke katika maisha ya mwanamme. Tazama mifano katika mashairi haya Vilevile katika tawasifu yake ya Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini anasema;

*“Marehemu huyu alikuwa johari ya maisha, tegemeo na*
*mshauri mwema alinisaidia katika mambo mengi …” (Uk, 3)*

*“Hapana haja ya kudharau mwanamke.*
*Wanawake ni malaika*
*Makao yao sawa nayale ya pepo” (uk. 40).*

Katika mifano ya shairi hilo tunaona wanawake wanafananishwa na malaika ambao makao yao ni peponi. Hivyo sitiari ‘malaika’imetumika kumrejelea mwanamke ambapo sifa za malaika ni utiifu, upole, uzuri, unyeyekevu, uso hatia na wema.

Hivyo basi, sitairi hii imetumika kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii kuwa ni mpole, mnyenyekevu, mtii, aso na hatia na mwema. Aidha, Katika tawasifu yake ya *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* mwandishi anamwandikia utenzi mwanae Adili akimwonya na kumtaka awaheshimu wanawake kama alivyo muheshimu mama yake. Kuthibitisha hili mwandishi anasema;

*"Mke mpe heshima*
*Mheshimu kama mama*
*Mzaa watoto wema*
*Ulivyo zaliwa wewe "   ubeti. 62. (Uk. 31).*

Katika shairi hilo msanii anatumia tashibiha kulinganisha umuhimu wa mke na mama na kutaka wanaume wawaheshimu wake zao kama ambavyo wanawaheshimu mama zao.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii ambayo inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data imejadili juu ya data za utafiti huu. Katika utafiti huu imejadiliwa kuwa mashairi ya Shaaban Robert hutumia tamathali za semi ambazo ni sitiari, tashibiha, tashihisi, takriri na tafsida. Aidha utafiti huu uligundua kuwa tamathali za semi hutumiwa kusawiri mahusiano ya mwanamke na mwanamme ambapo utafiti huu umeonyesha kuwa kuna mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume katika nyanja zote; katika elimu, dini, uchumi, maamuzi na masuala ya kijamii. Tofauti hizi zinaonyeshwa kwa kutumia tamathali za semi ambazo zinamzungumzia mwanamke kwa namna ya pekee na zile zinazomzungumzia mwanaume. Mwanamke huchukuliwa kama kiumbe tegemezi

wakati mwanaume huonekana ndiye mwenye maamuzi na mamlaka katika jamii. Katika sura hii imejadiliwa kuwa mwanamke tamathali za semi zilizotumika katika mashairi ya shaaban robert zinaonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii. Nafasi ya mwanamke inaonekana katika: asasi ya ndoa, kufanya maamuzi, elimu, uzazi na malezi, mapenzi, utamaduni, mwanamke katika dini na mwanamke kama kiumbe muhimu katika jamii.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho amabyo inatoa muhtasiri, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inaelezea muhtasari wa matokeo ya utafiti huu, sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa jinsia katika lugha ya mashairi ya Shaaban Robert katika kazi zake za fasihi za *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* ili kuonyesha jinsi gani lugha inavyotumika kujadili suala la ujinsia. Utafiti huu uliongozwa na malengo mahususi matatu. Kwanza, kubainisha tamathali za semi zilizotumika katika Mashairi ya Shaaban Robert katika vitabu vya Pambo la Lugha na Maisha yanga na Baada ya Miaka Hamsini vilivyoandikwa na Shaaban Robert. Pili, kujadili jinsi tamatahli hizo zinavyosawiri mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamume. Tatu, kujadili nafasi ya mwanamke katika jamii kama inavyosawiriwa na tamathali za semi zinazopatikamna katika mashairi ya Shaaban Robert katika Pambo la Lugha na Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini. Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo; Ni tamathali zipi za usemi zinazojitokeza katika mashairi ya Shaaban Robert ya *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*?, Tamathali hizo zinasawiri vipi mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme? Je, Mwanamke anapewa

nafasi gani katika tamathali za semi zilizotumika katika mashairi ya *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*?

Utafiti huu ulifanyika katika jiji la Dar es Salaam na ulichunguza maoni, mtazamo na uelewa wa walimu na wanafuzi wa fasihi hususani ushairi wa Kiswahili kwa kujielekeza katika ushairi wa Shaaban robert. Nia kuu ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza tamathali za semi na dhima zake kijamii, kisiasa na kiuchumi na jinsi zinavyoukilia miundo ya kijamii kwa kutumia lugha.

Utafiti huu ulitumia watafitiwa 299 waliotumika kama sampuli ya utafiti huu. Watafitiwa walichaguliwa kwa kuzingatia kigezo cha elimu kutoka vitengo taasisi teule kwa kuzingatia kuwa makundi ya jamii kielimu huwa na matumizi tofauti tofauti ya lugha katika kujitambulisha kwake. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji data za utafiti huu maktaba, usaili, majadiliano ya vikundi na dodoso. Utafiti huu ulitumia pia mkabala wa uwandani na mkabala wa maelezo katika ukusanyaji data.

Utafiti huu umeonesha kuwa wazungumzaji wa Kiswahili wanatumia tamathali za semi kwa lengo la kuleta athari fulani katika mawasiliano yanayofanyika. Utafiti ulionesha kwamba tamathali za semi zinaonesha matabaka yaliyopo katika jamii na kwamba kupitia lugha inayozungumzwa yaani aina ya tamathali za semi huonesha nafasi ya kijamii na mamlaka aliyonayo mzungumzaji wake. Vilevile tamathali za semi zinaonesha mgawanyo wa majukumu kijinsia baina ya wanawake na wanaume. Kwa hiyo, tamathali za semi ni silaha ya kijamii ianyoweza kutumiwa na tabaka

lenye nguvu kuhalaisha na kuendeleza maslahi yake kwa kuweka mfumo unaowapendelea kupitia lugha (tamathali za semi wanzozungumza).

Katika utafiti huu ilibainika kuwa katika kazi za Shaaban Robert kuna matumizi ya tamathali za semi kama vile: Sitiari, takriri, tashihisi, tasifida na tashibiha. Iligundulika kuwa tamathali hizi zinatumika kama njia ya kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

Aidha utafiti huu uligundua kuwa, tamathali za semi husawiri swala la ujinsia kwa kuonyesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume. Kwa kutumika tamathali za semi mwanamke husawiriwa kama kiumbe dhaifu, tegemezi na asiye na maamuzi binafsi ukilinganisha na mwanaume ambaye huonekana kuwa ni jasiri, hodari, shupavu na mwenye maamuzi binafsi. Vile vile, utafiti huu uligundua kuwa, matumizi ya tamathali za semi husawiri nafasi ya mwanamke katika jamii. Kwa kutumika tamathali za semi nafasi ya mwanamke inajibainisha katika: asasi ya ndoa, kufanya maamuzi, elimu, uzazi na malezi, mapenzi, utamaduni, dini na mwanamke kama kiumbe muhimu katika jamii.

## 5.3 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, utafiti huu umegundua kuwa, tamathali za semi hutumika katika kusawiri masuala ya kijiinsia katika mashairi ya Shaaban Robert. Utafiti huu umegundua kuwa mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume yanaelezewa kupitia tamathali za semi na hivyo tamathali za semi hutumika kumchora mwanamke tofauti na jinsi zinavyotumika kumchora mwanaume.

Mwanamke huchorwa kama kiumbe dhaifu, tegemezi na asiye na maamuzi binafsi ambaye anapaswa kumnyenyekea na kumtii mwanaume. Adiha mwanaume amechorwa kama kiumbe shupavu, jasiri, hodari na mwenye maaumuzi binafsi katika jamii,. Mwanaume anaonekana hata katika dini ana maamuzi na mamalaka juu ya mwanamke. Hivyo lugha kupitia kipengele cha tamathali za semi huonyesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanamme. Utafiti huu umedhihirisha kuwa mwanamke anapewa nafasi tofauti na mwanaume ambazo zinadhihirishwa kupitia kipengele cha tamathali za semi. Mfano Kwa kutumika tamathali za semi nafasi ya mwanamke inajibainisha katika: asasi ya ndoa, kufanya maamuzi, elimu, uzazi na malezi, mapenzi, utamaduni, dini na mwanamke kama kiumbe muhimu katika jamii.

Aidha, utafiti huu umechangia katika kuongeza maarifa mapya katika taaluma ya fasihi hususan ushairi wa Kiswahili katika kubainisha nafasi ya tamathali za semi katika kusawiri masuala mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na mahusiano baina ya wanawake na wanaume. Hii ni kwa sababu utafiti huu umebainisha aina za tamathali za semi zinazotumiwa katika mashairi ambayo pia ni tamathali ambazo hutumiwa katika mawasiliano ya kawaida ndani ya jamii. Matokeo ya utafiti huu yatawasaidia wataalamu wengine wa fasihi kuweza kujua imani, hisia, mtazamo, maoni, matatizo na falsafa ya Waswahili inayodhihirishwa na tamathali za semi.

Vilevile ni rahisi kuwasaidia kutatua matatizo yanayowakabili wazungumzaji wa Kiswahili baada ya kuelewa dhima na nafasi ya tamathali za semi katika kusawiri mahusiano ya kijinsia. Kwa kuelewa ujumbe unaopatikana katika tamathali za semi

ni rahisi kusaidia kuondoa mitazamo potofu na miundo ya kiutawala inayowanyima fursa watu wengine wa kundi fulani kushirika katika mipango ya maendeleo na kuwa sehemu ya maamuzi hayo.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umechunguza matumizi ya tamathali za semi katika ushairi wa Kiswahili wa Shaaban robert na dhima yake katika kusawiri mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme. Utafiti huu ungeweza kuchunguza vipengele zaidi ya hivi, lakini kutokana na muda mfupi katika kumwezesha mtafiti kukamilisha utafiti huu kwa wakati, utafiti huu umeishia kushughulikia vipengele hivi tu. Kwa hiyo, watafiti wengine wanaweza kufanya utafiti juu ya taaluma ya ushairi kuhusu vipengele kama vile uhusiano wa tamathali za semi na utamaduni wa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili, matumizi ya tamathali za semi katika nyimbo za kubembelezea watoto, uhusiano wa aina ya tamathali za semi katika nyimbo za jadi kwa kuzingatia ngoma ya Lizombe na kadhalika.

Aidha, utafiti huu unapendekeza kufanyike utafiti mwingine kulinganisha usawiri wa ujinsia katika mashairi mengine ama kazi zingine za fasihi ili kuona kama mwanamke anasawiriwa katika uduni kama ilivyo katika mashairi ya Shaaban Robert.

# MAREJELEO


Abeid, K.A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abu-Lughod, L. (1986). *Veiled Sentiments*. Berkeley: University of California Press.

Akivaga, S.K. na Odaga, A.B. (1982). *Oral Literature*. Nairobi: Heinemann Educational Books.

Alembi, E. (1991). *Don't be Long John*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Atwood, M. (1976). *Selected Poems* (1965-1975). Boston: Houghlin Mifflin.

Babbie, E (1992). *The Practice of Social Research*. 6th edition. Wadsworth Publishing Company.

Balisidya, N. (1982). "The Image of the Woman in Tanzanian Oral Literature: A Survey". In *Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI, 49 (2), 1-31.

Best and Kahn, J. (1993). *Research in Education*. New York: Allyn Bacon Inc.

Borg, W.R and Gall, M.D, (2003). *Educational Research: An Introduction***.** Longman London .

Briggs, Charles (1992). "Since I am a woman, I will chastise my relatives":

Gender, reported speech, and the (re)production of social relations in Warao ritual wailing. *American Ethnologist* 19(2): 337-61. Brown, Penny 1979.

Brossard, N. (1977). *These Mothers Or*: The Disintegrating Chapter (1983) by Barbara Godard. Toronto: Coach House Quebec Translations.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (2nd Ed.). Oxford: Oxford University Press.

Chodorow, N (1978). *Feminism and Psychoanalytic Theory*. New Haven, Yale: California Press.

Coates, J. (1986). *Women, Men and Language*. New York: Longman.

Cohen, L, Manion, L and Morrison, K. (2000). *Research Methods in Education*. 5th edition. London: Rutledge Falmer.

Connel, R.W. (1995). *Masculinities*. Cambridge, UK: Polity Press.

Cooper, H. (1998). *Synthesizing Research: Aguide for Literature Reviews* (3rd Ed.). Thousand Oaks, CA: Sage.

Coplan, D. (1987). "Eloquent Knowledge: Lesotho Migrants' songs and the Anthropological Experience". *American Anthropologist*, 14 (3) 413-33.

Dawson, C. (2002). *Practical Research Methods*. New Delhi: UBS Publishersa' Distributors.

Doyle, J. (1989). "Constructive Belief and Rational Representation": *Computational Intelligence*. 5(1) 1-11.

Feld, S. (1982). *Sound and Sentiment: Birds, Weeping, Poetics, and Song in Kaluli expression*. University of Pennsylvania.

FEMA(2010) http://www.feminahip.or.tz/fileadmin/femina/newsletters/Femina_Wire_Issue_5.pdf

Firestone, S. (1972). *The Dialectic of Sex: The Case for Feminist Revolution*. New York: William Morrow and Company.

Fleming, J. (1978). *Forever Feminine*: Women's Magazines and the Cult of Femininity. London: Heine-mann.

Halliday, M.A.K. (1978). *Language as social semiotic. The Social Interpretation of Language and Meaning*. London: Edward Arnold.

Hirsch, M. (1998). "Projected Memory: Holocaust Photographs in Personal and Public Fanatsy". In Bal et al 1998.

Holmes, J. (1995). *Men, Women and Politeness*. London: Longman.

Holmes, J. and Meyerhoff, M. (eds.) (2003). *The Handbook of Language and Gender*. Oxford: Blackwell Publishers.

Harmondsworth: Penguin Books (b) Parkes, Colin Murray (1975). *Bereavement: studies of grief in adult life*. Harmondsworth: Penguin Books.

IDAF for South Africa and UNESCO in Books (1988). A Cartoon History Comics & Magazines, Non-Fiction, Politics & Government.

Inyani, S.K. (2002). Utafiti wa Kiswahili na Maswala ya Uana: UTAFITI WA KISWAHILI. Nairobi. Downtown Printing Works ltd

Jilala, H. (2008). 'The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania.' MA Dissertation (Unpublished), University of Dar es Salaam.

Johnson, S. & Meinhof, U (eds.) (1997). *Language and Masculinity*. Oxford: Blackwell Publishers.

Kahigi K.K. (1994). 'Lugha Katika Vitabu Vya Watoto.' Katika *Kioo cha lugha: Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu, Na. 1. (uk. 21-36).

Khatibu, M.S. (1985). (Review) 'Utenzi wa Mwanakupona'. Katika *MULIKA*. Dar es Salaam. TUKI. 17, 46-52.

Kiango, S. (1982). "Tamthiliya (Tamthiliya) za Kiswahili: Dhamira Chapwa na Usuli katika Uchapwa". In *Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. 49/2, 33-56.

Kombo, D. K. and D. L. Tromp (2006*). Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C. K (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C.R. (1993). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C. R (2001). *Research Methodology: Methods and Techniques*. Ed. New Delhi: Wiley Eastern.

Kothari,R.C. ( 2004). *Research Methodology. Methods and Techniques* New Delhi:New Age International (P) Limited, Publishers.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse*. Nairobi: Heinemann

Kristeva, J. (1984). *Revolution in Poetic Language*. New York: Columbia University Press.

Lacan, J. (1977). The Morror Stage as a Formative of a Function of the I as Revealed in Psychoanalytic Experience". London: Tavistock.

Lakoff, G. and Johnson, M. (1980). *Metaphor We Live By*. Chicago: University of Chicago Press.

Larson, C.R. (1973). "Pop Pulp Goes Soft Core in Nairobi." Journal of Popular Culture, 7: 606-8.

Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. New York: Longman Group Inc. Limited.

Lofland, J. and Lofland, L. H. (1984). *Analyzing Social Settings*. Belmont, CA: Wadsworth Publishing Company, Inc.

Low, R.N. (2011). "Athari ya Lugha katika Kuibua Dhamira: Mifano Kutoka Nyimbo za Kizazi Kipya Zihusuzo UKIMWI, Tasinifu ya M.A. Kiswahili". Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Maclaughlin, A. na Braxton (1990). Wild Women in Whirlwing: Afro American Culture and Contemporary Literary Renaissance, New Brunswick: Rutgers University Press.

Mazrui, A. (1981). *Kilio cha Haki.* Nairobi: Longman.

Mernissi, F. *(*1987*). Beyond the Veil: Male-Female Dynamics in Modern Muslim Society*. Indiana: Indiana University Press.

Middleton, J. (1992). *The World of the Swahili.* New Haven: Yale University Press.

Millett, K. (1977). *Sexual Politics*. London: Virago.

Mligo, S. E. (2012). Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti Wenye Mantiki. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).

Mlowezi, D. (2012). 'Lugha ya Vijana wa Dar es Salaam na Utambulisho wao: Mifano kutoka Kiswahili.' M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mohamed, S.A. (1983). "Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii ya Tanzania. Katika *Mulika*. Dar es Salaam. TUKI. 15, S. 3-13.

Momanyi, C. (1991). "Matumizi ya Taswira kama kielelezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al-Inkishafi". M.A. Thesis. Nairobi. Kenyatta University.

Momanyi, C. (1998). "Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili". Ph.D. Thesis.

Nairobi. Kenyatta University (Unpublished).

Momanyi, C. (2001). Nadharia ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike na Uhakiki wa Kifasihi: *Kioo cha lugha.* Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Momanyi, C. (2007). “Patriarchal Symbolic Order: The Syllables of Power as Accentuated in Waswahili Poetry.” *The Journal of Pan African Studies*, Vol.1, no. 8.

Msanjila, Y.P., Kihore, Y.M. na Massamba, D.P.B. (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mugenda, O. M. and Mugenda, A. G. (2003). *Rearch Methods*: *Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi: Acts Press Kenya.

Mulokozi, M. and Kahigi, K.K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M.M na Sengo, T.S.Y. (1995). *History of Kiswahili Poetry* (A.D 1000-2000). Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Mulokozi, M. (1982). “Protest and Resistance in Swahili Poetry: 1600-1885, In *KISWAHILI Vol.49/1,* Dar es salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. TUKI. Dar es Salaam.

Mutembei, A. (2009), UKIMWI katika fasihi ya Kiswahili 1982-2006. Dar es Salaam: TUKI.

Nabhany, S.A.and A. Abubakar (1972) *Sanaa ya Utungo*. Nairobi: Heinemann.

Nicholas, J. (2005). “Address to Friends of Adelaide University” State Library of South Australia.

Njozi, H.M. (1990). “Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics.” In *KISWAHILI Vol. 57*, Dar es Salaam: TUKI.

Oculi, O. (1968). *Prostitute: African Writers on African Writing.* Nairobi: EAPH.

Ogechi, N.O., Shittemi, N.I., Simala, K. I. (2008). *Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*.Moi University Press.

Ogundipe-Leslie (1984). “Not Spinning on the Axis of Maleness”. Robin Morgan (ed.) *Sisterhood is Global*. *New York:* Achor Press/Doubleday.

Omari, S. (2009). “Tanzania Hip Hope Poetry as Popular Literature” Ph.D (Literature). University of Dar es Salaam.

P’ Bitek, O (1974). *Song of Malaya in Two Songs*. Nairobi: EAPH.

Parsons, T., & Bales, R.F. (1955). *Family, Socialization and Interactin Process*. Glencoe, IL: Free Press.

Ponera, A. (2010). *Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert*, Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Pullen, A. (2006). *Managing Identity*. Basingstoke: Palgrave.

Rosaldo, R. (1986). “From the Door of His Tent: The Fieldworker and the Inquistor. In Clifford, J; Marcus, G. (eds.) (1986). The Writing Culture: *The Poetics of Politics of Ethnography*. Berkeley, Los Angeles: University of Calfonia Press, pp. 77-97.

Ruthven, K.K. (1984). *Feminist Literary Studies: An Intreoduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

Sanger, W. (1937). *The History of Prostitution*. New York : Eugenics Publishing House.

Senkoro, F.EM.K (1982). *The Prostitute in African Literatue*. Dar es Salaam. DUP.

Scott, J.C. (1990). *Domination and the Arts of Resistance: Hidden Transcripts*. New Haven: Yale University Press.

Sheezer, J. (1987). “A Discouse-centred Approach to Language and Culture”. *American Anthropologist*, 89, 295-309.

Showalter, E. (1977) ."The Female Tradition." In *A Literature of Their Own: British Women Novelists From Brontë to Lessing*, pp. 3-36. Princeton, N.J. : Princeton University Press.

Standt, K. (1976). “The Characterization of Women in Soyinka and Armah, Ba Shiru,” 8: 63-9.

Steady, F.C. (ed.) (1981). *The Black Africa Cross-Cultulary*. Cambridge: Schenkman Publishing Company.

Trochim, B. (1999). *Bill Trochim’s Center for Social Research Methods.* http://trochim.human.cornell.edu/.28/9/2012.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasih:, Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Walliman, N. (2011). *Research Methods*: *The Basics*. Milton Park: Routledge.

Weedon, C. (1997). *Feminist Practice and Poststructualist Theory* (2nd Edn.). Oxford: Blacwell.

Wolkoff, G. (2011). “Visuality and Experimentalism: Two Commented Examples in Contemporary Portuguese Poetry”. *Via panoramic: Revista Electronica de Estudos Anglo Americanos/An Aglo-American Studies Journal.*

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO I: Dodoso Kwa Ajili Ya Walimu Na Wanafunzi Wa Fasihi

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Usawiri wa Jinsia Katika Lugha ya Mashairi: Mifano Kutoka Mashairi ya Shaaban Robert.** Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa jinsia katika lugha ya mashairi ya Shaaban Robert katika kazi zake za fasihi za *Pambo la Lugha* na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* ili kuonyesha jinsi gan lugha inavyotumika kujadili suala la ujinsia. Nitashukuru sana wewe kama mwanafasihi ya Kiswahili utaweza kujibu maswali ya dodoso hili kwa makini, uwazi na ushirikiano wa hali ya juu. Nitafurahi ikiwa utaijaza hojaji hii kwa tarehe tulizokubaliana. Tumia bahasha niliyokupa kuifunga hojaji yako kwani taarifa utakazotoa ni siri na zitatumiwa na mtafiti kwa ajili ya utafiti tu na si vinginevyo. Aidha, nakuomba usiwe na hofu yoyote katika ujazaji wa hojaji hii maana majibu utakayotoa yatatunzwa kwa siri. Usiandike jina lako mahali popote.

**Sehemu ya Kwanza**

**Taarifa Binafsi za Mtafitiwa**

1. Umri…………………………………………………
2. Jinsi….………………………………………………
3. Kazi (Kitengo)..................................…………………
4. Kiwango cha elimu…………………………………
5. Uraia……..…………………………………………
6. Mahali unakoishi……..……………………………

7. Lugha yako ya kwanza ni…………………………

**Sehemu ya Pili**

**Taarifa Kuhusu Matumizi ya Tamathali za Semi katika Mashairi ya Shaaban Robert**

8. Mashairi ya Shaaban Robert yamesheheni tamathali za semi nyingi. Tamathali hizo zinasawiri ujinsia au mahusiano ya kijinsia katika muktadha halisi wa maisha ya kila siku. Taja angalau tamathali za semi nane ulizowahi kukutana nazo wakati unasoma kazi za ushairi zilizoandikwa na Shaaaba Robert.

   i) ............................................................................
   
   ii) ..........................................................................
   
   iii) .........................................................................
   
   iv) .........................................................................
   
   v) ..........................................................................
   
   vi) .........................................................................
   
   vii) ........................................................................

9. Kuna miundo ya aina mbalimbali ya tamathali za semi. Kwa kuzingatia tamathali za semi zinazopatikana katika mashairi yaliyoambatanisha na hojaji hii, taja miundo ya tamathali za semi unayoifahamu.

   i) ............................................................................
   
   ii) ..........................................................................
   
   iii) .........................................................................
   
   iv) .........................................................................

v) ..............................................................................

10. Taja nafasi ya mwanamke kama inavyobainishwa na tamathali za semi za mashairi yaliyoambatanishwa na hojaji hii.

    i) ..............................................................................
    ii) ............................................................................
    iii) ...........................................................................
    iv) ............................................................................
    v) ..............................................................................

11. Je, ni athari zipi zinaweza kusababishwa na tamathali za semi katika kuimarisha mahusiano ya kijamii baina ya wanawke na wanaumu endapo zitatumiak katika mazingira halisi?

    i) ..............................................................................
    ii) ............................................................................
    iii) ...........................................................................
    iv) ............................................................................
    v) ..............................................................................
    vi) ............................................................................
    vii) ...........................................................................
    viii) .........................................................................
    ix) ............................................................................
    x) ..............................................................................

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**KIAMBATISHO II**: **Mwongozo wa Maswali ya Usaili kwa Ajili ya Walimu na Wanafunzi wa Fasihi**

1. a) Una umri gani?

   b) Kiwango chako cha elimu?

   c) Lugha ya kwanza ni ipi?

   d) Ulianza kuitumia lugha ya Kiswahili ukiwa darasa la ngapi?

   e) Umezaliwa wapi?

   f) Una muda gani tangu uajiriwe katika mgodi huu?

2. Miongoni mwa mambo yanayoweza kutambulisha mahusiano ya kijinsia katika kazi mbalimbali za kidfasihi ni pamoja na tamatahli za semi. ni aina gani za tamathali za semi ambazo zimejitokeza katika Mashairi uliyopewa?

   i) ..................................

   ii) .................................

   iii) .................................

   iv)

3. Tamathali za semi zilizotumika katika mashairi ya Shaaban Robert zinasawiri masuala ya kijinsia?

4. Je ni mahusiano ya aina gani yanayojitikeza katika tamathali za semi zilizotumika katika mashairi ya Shaaban Robert

5. Je. Mwanamke anapewa nafasi gani na Shaaban Robert kupitia tamathali za semi?

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**KIAMBATISHO III: Maswali ya Mwongozo wa Majadiliano ya Vikundi**

1. Unafikiri ni kwa nini Shaaban Robert ametumia tamathali za semi kwa wingi katika mashairi yake?
2. Je, unadhani tamathali za semi zilizotumika zinasawiri suala la ujinsia katika jamii?
3. Jadili tofauti za kijinsia baina ya mwanamke na mwanaume kama ambavyo zinasawiriwa katika mashairi ya Shaaban Robert.
4. Je, tamathali za semi zinasawiri nafasi ya mwanamke katika jamii?
5. Jadili nafasi ya mwanamke kama ambavyo inasawiriwa na tamathali za semi katika mashairi ya Shaaban Robert

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**